# Nipashe

Ijumaa Aprili 5, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579884

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter ... etz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Askari polisi ajiua kwa risasi kisa kukosa mtoto

UKURASA 2


Mfuko wa Ubunifu ulivyoanika mahali kona ya maendeleo iliko — Ukurasa 14

SIDO yakusanya wahitimu kwa mazito ya ujasiriamali — Ukurasa 19

BUFE

Ijumaa Aprili 5, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Chuo Utalii chabun[i] mradi uliobeba sura tatu za neema

Utalii wa Utamaduni ulivyosafisha ujangili Mikumi, ukakaribisha uchumi mpya vijijini

Ashton Balaigwa, Morogoro

UJANGILI ni changamoto inayoikabili sekta ya utalii nchini na athari yake imepunguza baadhi ya wanyama kama tembo na faru ambao kihisitoria ni vivutio vikubwa vya biashara nje na ndani ya nchi.

Hiyo imeifanya serikali kuchukua hatua kuweka mikakati ya kuanzisha operesheni maalumu za kuwabaini wanaojihusha na ujangili. Unaelezwa ni matokeo ya vijana kukosa kazi ya kukimu maisha yao, hivyo wanahamia katika kuua wanyama.

Mikumi ni moja ya hifadhi tatu za Kanda ya Kusini iliyopo wilayani Kilosa kati ya 16 zinazosimamiwa na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Hifadhi hiyo iliyopo mkoani Morogoro, ilikuwa ikikabiliwa na tatizo la ujangili kutokana na kupitiwa na barabara kuu ya Dar es Salaam hadi Zambia kipande cha kilomita 50 unaotoa mwanya kwa majangili wanaotoka vijiji jirani na hifadhi hiyo.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

Habari katika picha — Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Takwimu za Biashara Ukurasa 2

UKURASA 13

# Spika: Hatujapewa ripoti za CAG Assad

• **Ametoa** kauli hiyo ripoti ikitakiwa kuwa imewasilishwa bungeni kabla ya Alhamisi... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

### TAREHE MPYA UCHAGUZI SERIKALI MITAA YATAJWA

SERIKALI imesema Uchaguzi wa Serikali za Mitaa sasa umepangwa kufanyika Oktoba katika halmashauri zote 185 badala ya...

**UKURASA WA 7**

### BUNGE LAWATOSA WABUNGE MIKOPO

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai amesema kwa sasa Bunge litalazimika kutowadhamini tena wabunge kuchukua mikopo benki baada...



Baadhi ya wajane wakiwa katika kongamano lililoandaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (hayupo pichani), jijini humo, jana, kwa ajili ya kutatua kero zao. Habari Uk. 5. **PICHA: MICHUZI BLOG**

## Mbunge CUF sasa 'ajilipua' kumfuata Maalim Seif

UKURASA 4

## Lema kifungoni hadi mwaka 2020



• **Kamati** yasema aliiambia isimwonee huruma, wala kumsamehe...*Ukurasa 3*

**MICHEZO** **SIMBA, MAZEMBE ZAWASHIANA MOTO** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Tarehe mpya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yatajwa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imesema Uchaguzi wa Serikali za Mitaa sasa umepangwa kufanyika Oktoba katika halmashauri zote 185 badala ya Novemba mwaka huu ilivyokuwa imepangwa awali.

Vilevile, imesema imekamilisha maandalizi ya kanuni zitakazotumika kusimamia uchaguzi huo ambao ni wa sita kufanyika nchini tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana hutoba yake kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za ofisi yake na Ofisi ya Bunge kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema serikali itahakikisha uwapo wa usalama na utulivu katika kipindi chote cha uchaguzi huo.

"Serikali imeshakamilisha uhakiki wa maeneo ya utawala ambayo yatashiriki kwenye uchaguzi huo kwenye halmashauri zote 185. Lengo la uhakiki ni kujiridhisha na usahihi wa maeneo hayo kwa idadi na majina ili kufanikisha maandalizi ya bajeti na mahitaji mengine muhimu ya uchaguzi huo," alisema.

Waziri Mkuu alitoa wito kwa wadau na wananchi kujiandikisha na kujitokeza kwa wingi kwenye upigaji kura ili kutumia haki yao kidemokrasia ya kuchagua au kuchaguliwa.

Kuhusu Uchaguzi Mkuu wa mwakani, Majaliwa alisema Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imeanza maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura pamoja na uhakiki wa vituo vya uandikishaji wapigakura.

"Hadi sasa, kanuni za uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura zimeandaliwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 792 na 793 ya Desemba 28, mwaka jana.

"Uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapigakura nao umekamilika ambao kwa upande wa Tanzania Bara, vituo vimeongezeka kutoka 36,549 vilivyokuwapo mwaka 2015 hadi kufikia vituo 37,407 mwaka jana, sawa na ongezeko la vituo 858," alisema.

Waziri Mkuu alisema kwa upande wa Zanzibar, vituo vimeongezeka kutoka 380 mwaka 2015 hadi kufikia vituo 407 mwaka jana, huku akitoa wito kwa wananchi wenye sifa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha mara zoezi litakapoanza.

Akielezea mafanikio yaliyopatikana katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Waziri Mkuu alisema serikali imeendelea kubaini mtandao wa wasambazaji na watumiaji wa dawa za kulevya.

Alibainisha kuwa hadi Januari mwaka huu, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, imefanikiwa kukamata watuhumiwa 11,617 wakiwa na dawa hizo aina mbalimbali kama vile heroine, cocaine, bangi na mirungi. Vilevile, Majaliwa alisema ekari 59 za mashamba ya bangi ziliteketezwa nchini katika mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza na Dodoma.

Waziri Mkuu alibainisha kuwa watumiaji 6,500 wa dawa za kulevya wanapata huduma za tiba ya methadone katika vituo mbalimbali vilivyopo nchini.

Ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Mkuu aliliomba Bunge liidhinishe Sh. bilioni 148.886 kwa ajili ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake.

# Spika Ndugai: Bunge halijapewa ripoti za CAG

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SPIKA Job Ndugai, amesema Bunge halijapewa ripoti ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2017/18.

Juzi, CAG, Prof. Mussa Assad, alisema tayari ameshaikabidhi ripoti hiyo kwa Rais na kinachosubiriwa kwa sasa ni kuwasilishwa bungeni kama inavyoelekezwa na Katiba na sheria za nchi.

Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inamtaka CAG kuwasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa.

Kwa mujibu wa ibara hiyo, baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye mkutano wa kwanza wa Bunge utakaofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika mkutano huo kabla ya kupita siku saba tangu siku ulipoanza.

Mkutano wa Bunge la Bajeti unaoendelea jijini Dodoma ulianza Jumanne Aprili 2, mwaka huu, hivyo ripoti ya ukaguzi ya CAG kwa mwaka wa fedha 2017/18 inapaswa kuwasilishwa bungeni kabla ya Alhamisi ijayo, yaani siku ndani ya siku saba tangu kuanza kwa mkutano (siku za mwishoni mwa wiki na sikukuu hazihesabiki).

Katika mkutano wake na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Spika Ndugai aliulizwa kama Bunge litapokea ripoti ya CAG kwa mwaka 2017/18 iliyotiwa saini na Prof. Assad, akaeleza kuwa chombo hicho cha kutunga sheria bado hakijapatiwa ripoti hiyo na mamlaka husika.

Alisema haoni sababu ya kuzungumza kama Bunge litapokea na kuifanyia kazi ripoti hiyo ya CAG ama la kwa kuwa haijapelekewa.

"Kitu ambacho sijaletewa, kwanini nianze kufanya mpango na wewe? Kusema kwamba kikija hivi itakuwa hivi, hicho kitu mimi sina mkononi, kwanini tuongelee 'hypothesis' (nadharia) niseme ndiyo au siyo. Kasome katiba inasemaje, katiba imesema kila kitu kuhusu hilo eneo," Spika Ndugai alisema.

Spika Ndugai alisema Bunge halijakataa kufanya kazi na Ofisi ya CAG, bali mtu anayeitwa Prof. Mussa Assad ambaye ametiwa hatiani na kamati yake kwa kulidharau na kulidhalilisha.

Alisema Ofisi ya CAG ni muhimu kwa utendaji wa Bunge na wataendelea kushirikiana nayo na mpaka sasa maofisa wa ofisi hiyo wako bungeni wanatekeleza majukumu yao.

Alisema walikwazwa na kauli ya Prof. Assad kwamba Bunge ni dhaifu ilhali linashirikiana naye kwa kiwango kikubwa na ofisi yake inashiriki katika utekelezaji wa shughuli za chombo hicho cha kutunga sheria.

Jumanne, Bunge lilipitisha azimio la kutofanya kazi na Prof. Assad baada ya Kamati yake ya Kudumu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuwasilisha taarifa kuhusu shauri dhidi ya mtaalamu huyo wa ukaguzi wa hesabu aliyefikishwa mbele yake mwanzoni mwa mwaka akikabiliwa na tuhuma za kudharau, kudhalilisha na kushusha heshima na hadhi ya chombo hicho cha kutunga sheria.Katika mkutano wake wa jana na waandishi wa habari, Spika Ndugai pia alifafanua kuhusu uamuzi wake wa kuzuia wabunge wanaosusa vikao vya Bunge kufanya mahojiano na vyombo vya habari kwenye Viwanja vya Bunge.

Alisema agizo lake hilo limelenga kukomesha tabia ya baadhi ya wabunge kuharibu makusudi shughuli za Bunge na kutengeneza mazingira ya kuonyesha kwamba wanaonewa ilhali wana nafasi ya kueleza hisia zao ndani ya Ukumbi wa Bunge.



Kaimu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ziara inayoendelea ya ujumbe wa Taasisi ya Habari ya Kimataifa (IPI) yenye makao makuu yake Vienna nchini Austria. Kushoto ni Mkuu wa DW Akademia Carsten von Nahmed na Makamu Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Khadija Patel. **PICHA: JOHN BADI**

# Askari polisi ajiua kwa risasi kisa kukosa mtoto

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ASKARI Polisi wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Gideoni Kijelengwa (30), amedaiwa kujiua kwa kujipiga risasi kichwani na kufariki dunia papo hapo kwa madai ya kuishi ndani ya ndoa miaka mitano bila kupata mtoto.

Tukio hilo limetokea jana saa 1:30 asubuhi wakati askari huyo akiwa lindo kwenye benki ya Access Wilaya ya Kahama na kabla ya kujiua alimtumia ujumbe mfupi mkewe kuwa amechoka kuishi, kutokana na kutopata mtoto ndani ya ndoa yao na kuamua kujipiga risasi na kusababisha kifo chake papo hapo.

Akitoa taarifa kwa vyombo habari, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, alisema askari huyo alikuwa ameoa mwalimu na baada ya kuona hawaja jaliwa kupata mtoto ndani ya ndoa yao kwa muda wa miaka mitano, ndipo alipoamua kujipiga risasi shingoni ambayo ilisambaratisha kichwa chake.

"Kabla ya kujiua askari huyo alimtumia ujumbe mke wake kuwa amechoka kuishi kutokana na kukaa ndani ya ndoa bila ya kupata mtoto ndani ya miaka mitano, na kwenye ujumbe huo pia alimwonyesha mali za viwanja vilipo na kisha akajipiga risasi na kufariki hapo hapo," alisema Abwao.

Alisema askari huyo ni mkazi wa Muleba mkoani Kagera, na Jeshi la Polisi limeshaanza taratibu za kuusafirisha mwili huo kwenda kwao kwa ajili ya maziko.

# HABARI KITAIFA



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola (kushoto), akizungumza na Kamishna Jenerali wa Idara ya Uhamiaji, Dk. Anna Makakala (katikati) na Balozi wa Ethiopia nchini, Yonas Yosef, baada ya kufungua mkutano wa kupitisha mpango juu ya kushughulikia hali ya uhamiaji na kuimarisha ushirikiano, uliofanyika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Lema tena kifungoni hadi 2020

**Na Sanula Athanas**, DODOMA

MBUNGE wa Arusha Mjini, Godbless Lema (Chadema), amesimamishwa kuhudhuria mikutano mitatu ya Bunge baada ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kumtia hatiani kwa kutamka maneno yaliyolenga kulidhalilisha na kukidharau chombo hicho cha kutunga sheria.

Mbunge huyo mwenye historia ya kukaa mahabusu gerezani kwa kipindi kirefu kuliko wabunge wote wa Bunge la 11, alilalamikiwa kwa kumuunga mkono Mbunge wa Kawe, Halima Mdee (Chadema) ambaye pia aliunga mkono kauli ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad kuhusu "udhaifu wa Bunge".

Jumanne iliyopita, Lema wakati akichangia hoja ya kamati hiyo dhidi ya Mdee, aliunga mkono kauli ya CAG Assad kwamba Bunge ni dhaifu huku akinukuu maneno aliyoyatoa mbunge mwenzake (Mdee).

Kutokana na kitendo hicho kilichotafsiriwa kuwa ni kulidharau na kulidhalilisha Bunge, Naibu Spika, Dk. Tulia Akson, aliagiza Lema afikishwe mbele ya Kamati ya Maadili kuthibitisha kauli yake vinginevyo achukuliwe hatua za kinidhamu.

Uamuzi huo wa Dk. Tulia ulikaziwa na Spika Job Ndugai juzi, akieleza kuwa

INAENDELEA UK. 8

# JPM afungua kituo cha afya cha mil. 500/-

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli jana alimaliza ziara yake ya siku tatu mkoani Mtwara kwa kufungua Kituo cha Afya cha Mbonde katika Wilaya ya Masasi na kufungua barabara za Mangaka - Nakapanya - Tunduru na Mangaka - Mtambaswala.

Kituo cha Afya cha Mbonde kilichojengwa kwa gharama ya shilingi milioni 500 ni miongoni mwa vituo vya afya vipya 13 vilivyojengwa mkoani Mtwara na ni miongoni mwa vituo vipya 352 vilivyojengwa nchi nzima katika kipindi cha miezi 18 iliyopita vikiwa na uwezo wa kutoa huduma za matibabu mbalimbali ikiwamo matibabu ya upasuaji.

Akiwa kituoni hapo, Rais Magufuli amejionea miundombinu yake ikiwamo wodi za kulala wagonjwa, maabara, vyumba vya upasuaji vyenye vifaa vya kisasa na majengo mapya.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alimshukuru Rais Magufuli kwa kuendelea kutilia mkazo uwekezaji katika miundombinu ya kutolea huduma za afya pamoja na kutoa maelekezo yenye manufaa ikiwamo kuagiza ununuzi wa vifaa ufanyike moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji, hali iliyosaidia kuokoa gharama za ununuzi zikiwamo mashine za usingizi ambazo zimenunuliwa kwa shilingi milioni 50 badala ya shilingi milioni 100 kwa kila mashine moja.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, alisema serikali imefanikiwa kujenga vituo vya afya 352 na hospitali 67 nchi nzima katika kipindi cha miezi 18 ikilinganishwa na hospitali 77 zilizokuwa zimejengwa tangu Uhuru, na kwamba katika bajeti ijayo vituo vya afya vingine 27 vitajengwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza baada ya kufungua Kituo cha Afya cha Mbonde Rais Magufuli alimpongeza wananchi wa Masasi kwa kupata kituo hicho na ameeleza kuwa serikali imetumia shilingi bilioni 184 kujenga vituo vyote 352 nchi nzima kwa lengo la kuhakikisha Watanzania wanapata huduma za uhakika za matibabu jirani na maeneo wanayoishi.

Alipongeza Wizara ya Afya na Tamisemi kwa kuhakikisha ujenzi wa vituo vya afya

INAENDELEA UK. 8

# Nassari atoa kauli hatima Arumeru

**Na Enock Charles**

ALIYEKUWA Mbunge wa Arumeru Mashariki, Joshua Nassari (Chadema), amesema anakubaliana na uamuzi wa chama chake kutosimamisha mgombea katika jimbo hilo kwa kuwa kusimamisha mgombea ni sawa na kubariki uovu na uonevu kwa wananchi.

"Ukisimamisha mgombea maana yake unabariki huo uovu na uonevu," Nassari alieleza wakati akizungumza na Nipashe.

Kauli ya Nassari ni ya kwanza kuitoa tangu Katibu Mkuu wa chama hicho Dk. Vincent Mashinji, Jumatatu hii kutoa msimamo wa chama hicho kutoshiriki katika uchaguzi mdogo wa kujaza nafasi hiyo, baada ya Nassari kupoteza sifa za kuwa mbunge.

Dk. Mashinji alinukuliwa na gazeti moja nchini akisema Chadema haitashiriki uchaguzi huo, na mtazamo wa chama hicho upo katika uchaguzi mkuu wa mwakani.

Pia alipoulizwa kama Nassari ataamua kuwania kupitia chama kingine, alisema kinachomweka mtu katika chama ni itikadi na si madaraka.

"Kama anakuwa ndani ya chama kwa ajili ya madaraka anaweza kuondoka," Dk. Mashinji alisema.

Kadhalika, Nassari alipuuza madai ya kuwa ana mpango wa kukisaliti chama hicho kwa kuuza jimbo hilo kwa chama kingine na kudai

INAENDELEA UK. 8



MAHOJIANO MAALUM

# Mbunge CUF 'ajilipua' kumfuata Maalim Seif

## ■Adai Bunge limekosea kuazimia kutofanya kazi na CAG Assad

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

JUMANNE iliyopita, siku ya kwanza ya Bunge la Bajeti linaloendelea mjini Dodoma, Bunge lilipitisha azimio la kutofanya kazi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad.

Uamuzi huo wa kwanza kutolewa dhidi ya Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika historia ya Bunge la Tanzania, ulifikiwa baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuwasilisha taarifa yake bungeni kuhusu shauri la CAG Assad kulalamikiwa kulidharau na kulidhalilisha Bunge kutokana na kauli yake ya mwanzoni mwa mwaka huu New York, Marekani kwamba "Bunge ni dhaifu".

Mbunge wa Chambani, Yussuf Salim Hussein (CUF), ni miongoni mwa wabunge wachache waliopata nafasi ya kuchangia hoja ya Kamati ya Maadili kuhusu pendekezo la Bunge kuazimia kutoshirikiana na CAG Assad.

Katika mchango wake, Hussein alimpongeza Prof. Assad kwa kusema ukweli na kutoisumbua kamati kwamba hicho ndicho alichokisema na hakuona sababu yoyote ya kumtia hatiani maana ameshasema alichokisema na ndiyo taaluma yake.

"Tunapokosolewa lazima tukubali kukosolewa, sisi ni binadamu, hakuna aliyekamilika, kamati haijamtendea haki Prof. Assad, kwani sisi ni nani hadi tusikosolewe? Lazima tukubali, kama ni udhaifu tunao kwa sababu sisi ni binadamu, tuangalie sasa udhaifu huu uko wapi na nini tufanye," Hussein alisema.

Baada ya kupitishwa kwa pendekezo hilo la Kamati ya Maadili, Nipashe ilizungumza na Salim mjini Dodoma kuhusu uamuzi huo na mambo mengine ya kitaifa.

Katika mahojiano hayo, mbali na sakata la CAG Assad, mbunge huyo pia aliweka wazi kuwa atajiunga na chama cha ACT-Wazalendo kungana na aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad, ambaye alijiunga nacho mwezi uliopita, ikiwa uongozi wa chama chake cha sasa utamtimua.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na mbunge huyo:-

**SWALI:** Bunge limepitisha azimio la kutofanya kazi na kushirikiana na CAG Assad ambalo wewe ulilipinga vikali wakati wa kulijadili bungeni. Nini kauli yako kuhusu uamuzi huo wa Bunge?

**HUSSEIN:** Kwanza; wabunge tumekurupuka na huo uamuzi. Kama Bunge haliwezi kufanya kazi na CAG, litafanyaje kazi? Waseme wazi Bunge haliwezi kufanya kazi na Prof. Assad, lakini siyo CAG.

La pili naloweza kusema ni kwamba Prof. Assad ni mtu anayejiamini. Na mimi nilifikiri kutoka ile miaka ya '60, '70 hakuna tena wanaume wanaojiamini ndani ya Tanzania, kumbe bado wapo.

Prof. Assad anajiamini kama alivyokuwa anajiamini Abdallah Said Mwamwindi, ambaye alijaribu kuchezewa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa miaka hiyo na Mwamwindi akaamua alichokiamua.

Mwamwindi alichezewa kama alivyotaka kuchezewa Prof. Assad na kamati hii ya Bunge (Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge), lakini aliamua alichokiamua. Kumbe Tanzania bado wapo wanaume.

Cha tatu; Prof. Assad anahukumiwa na Bunge hili kwa sababu wameelekezwa kwa sababu ya msimamo wake. Hahukumiwi kwa sababu ya kitu kingine chochote. Huo ndiyo msimamo wangu. Wabunge hawawezi kufanya kazi na CAG au hawawezi kufanya kazi na Prof. Assad? Waamue moja, hapo wafafanue.

**SWALI:** Unafikiri uamuzi huu wa Bunge kupitisha azimio la kutofanya kazi na CAG Assad una madhara yapi kwa nchi na Bunge lenyewe?

**HUSSEIN:** Kwanza; Bunge hatuwezi kumtoa kwa mujibu wa Katiba, hatuwezi kumtoa sisi. Sasa, wanaposema hawawezi kufanya kazi na Assad, Bunge litafanyaje kazi na yule ndiye Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali? Bunge litafanyaje kazi sasa? Ni dhahiri kwamba Bunge litashindwa kufanya kazi.

Lakini, kama nilivyoeleza mwanzo, hii ni 'system' (mfumo). Kuna kitu ambacho kimepangwa kwamba hawamtaki Assad, siyo CAG. Bunge kufanya kazi na CAG ni lazima, bila hivyo, Bunge litafanyaje kazi? Haliwezi kufanya kazi.

Kwa hiyo, tunapingana na Katiba ya nchi, tunapingana na sheria za nchi. Bunge hatuwezi kumwondoa, na hata Rais hawezi kumwondoa, kuna utaratibu wake wa kumwondoa ulioelezwa kikatiba. Kwa hiyo, huo ndio ufuatwe basi tuone.

**SWALI:** Kuondoka kwa Maalim Seif CUF, kumekiathiri vipi chama hicho kwa mtazamo wako?

**HUSSEIN:** CUF imekufa, haipo. Wewe unaiona CUF? Itadumu labda kwa sababu ya hivi 'vi-ruzuku' kwa huu mwaka mmoja na nusu uliobakia wa uhai wa Bunge. Baada ya hapo, CUF haipo.

Tulikuwa tukisema bungeni mle kwamba 'mnachokoachokoa' kutaka kuiua CUF, CCM na serikali zake, mnataka kuiua CUF kumbeba (Dk. Mohamed) Shein kule Zanzibar. Muiue CUF ili mumbebe Shein Zanzibar, lakini CUF siyo jina, CUF ni wanachama, ni watu.

Tulilisema hilo na limedhihirika; Maalim katoka na watu wote wametoka. Sasa wao wanahangaika tu, si walitaka chama, wameachiwa chama, sasa kwanini wanababaika?

**SWALI:** Maalim Seif katoka CUF na wewe unasema chama kitakufa. Msimamo wako ni upi -- kubaki CUF au kumfuata Maalim Seif?

**HUSSEIN:** Msimamo wangu mimi uko wazi; mimi ni mbunge, sawa! Mimi ni mbunge, lakini sibaki CUF, kama nitamaliza kipindi changu, sawa! Sikumaliza, mimi naenda zangu ACT-Wazalendo. Wala sitafuni maneno katika hilo. Alipo nipo, shusha tanga, pandisha tanga, safari iendelee. Mimi siwezi kuwa mnafiki.

Kwa hiyo, ni mbunge sasa hivi kwa sababu wananchi wamenichagua, lakini nikiambiwa leo ondoka, basi naondoka, wala sina tatizo, kabisa!

**SWALI:** Kwa hali ya sasa ya siasa nchini, matumaini ni makubwa kiasi gani kwamba utarejea bungeni baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwakani?

**HUSSEIN:** Nina uhakika kwa asilimia 100. Kama kutakuwa na uchaguzi huru na wa haki katika nchi hii, basi nina asilimia 100 kwamba siyo mimi tu, wabunge Zanzibar tutarudi hapa. ACT ama chama chochote tutakachoamua kwenda sisi, si wamesema wanataka kukifuta chama cha ACT, wakifute...

Chama chochote tutakachoamua kwenda sisi, tuna uwezo wa kurudi hapa bungeni zaidi ya wabunge 35 wa upinzani kwa siasa zinavyokwenda. Wazanzibar ni waelewa zaidi ya wanavyofikiriwa na watawala na Chama Cha Mapinduzi.

**SWALI:** Ni jambo lipi unalojivunia kwa wananchi wa jimbo lako katika kipindi hiki cha ubunge?

**HUSSEIN:** Mimi nachojivunia ni kwamba wananchi wangu wananikubali. Mpaka sasa naenda kwa maagizo yao. Hata sasa hivi wakiniambia rudi, narudi kwa sababu nimeaminiwa na zaidi ya asilimia 98 ya wananchi wa jimbo langu. Wamenipa kura na najivunia.

Si kwamba wananikubali tu, bali wananiamini na ninawatendea haki kwa kutenda ambacho niliahidi kuwatendea wakati nilipoomba kura kuwa mbunge. Kwa hiyo, sina deni kwao katika kipindi changu cha ubunge.

**SWALI:** Jimbo la Chambani linakabiliwa na changamoto ipi kubwa kwa sasa na hatua gani zimechukuliwa kuitatua?

**HUSSEIN:** Changamoto kubwa ni kwamba majimbo tunayoongoza wapinzani, serikali hawataki kufanya shughuli zozote za maendeleo. Kwa hiyo, utakuta sisi wabunge ndiyo tunaopeleka maji, si jukumu letu.

Sisi wabunge ndiyo tunaopeleka umeme, si jukumu letu, tunaotengeneza barabara, si jukumu letu, shule, hospitali, mambo yote hayo unafanya mbunge kama mbunge. Fedha za Mfuko wa Jimbo, lakini fedha zangu mfukoni inabidi zitumike.

Kwa mfano, mimi fedha za Mfuko wa Jimbo napewa Sh. milioni 24 kwa mwaka, lakini natengeneza barabara ya Sh. milioni 60, hizo nyingine natoa wapi? Napeleka maji kwa Sh. milioni 80, natoa wapi?

Kwa hiyo, Mfuko wa Jimbo mimi sisemi kwamba haunisaidii, unanisaidia, lazima niwe mkweli, unasaidia. Sh. milioni 24 ninazopewa zinanisaidia, lakini mimi mwenyewe nafanya juhudi za kupeleka.

Lakini, nakupa ushahidi ya kwamba tangu mimi niwe mbunge, nina miaka mitano sasa -- ile miwili na hii mitatu sasa (amekuwa mbunge tangu Juni 2013), serikali haijafanya chochote ndani ya jimbo langu, si ya Muungano, si ya Mapinduzi.

Kunapokuwa na sherehe zao za Mwenge, wanashindwa hata mradi mmoja wa kuonyesha au kufungua, waje waniombe mimi miradi yangu wafungue kwa sherehe zao za Mwenge ama wakamwombe mtu binafsi amejenga nyumba yake nzuri, wanasema kwamba nyumba za kimaendeleo.

Hawana mradi wowote ambao umefanywa na serikali ambao wao watakuwa na uwezo wa kwenda kuufanyia kazi. Huu ni ushahidi wa kwamba serikali zote hazijafanya lolote katika kipindi chote ambacho mimi nimekuwa mbunge ndani ya jimbo langu.



Mbunge wa Chambani, Yussuf Salim Hussein (CUF).

## HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji (kulia), akiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Biashara ya DCB, Prof. Lucian Msambichaka (katikati) pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Godfrey Ndalahwa, baada ya hafla, ambapo benki hiyo ilitangaza matokeo ya zoezi la uuzaji wa hisa zake zilizouzwa kuanzia Novemba 12, 2018 hadi Januari 31 mwaka huu. DCB imetangaza kufanikiwa kuuza hisa 36,635,435 ikilinganishwa na hisa 33,913,984 zilizotarajiwa kuuzwa ikiwa ni sawa na asilimia 108. Hafla hiyo hiyo ilifanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zahanati yateketea, hema lawa mbadala

**Na Restuta Damian,** MISSENYI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, imeamua kujenga mahema ili kusaidia wananchi wa Kijiji cha Nyakere, Kata ya Mabale kuendelea kupata baadhi ya huduma baada ya zahanati yao kuteketea kwa moto.

Akizungumza na Nipashe, Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Hamisi Abdallah, alisema tatizo la moto huo limetokea usiku wa kuamkia jana majira ya saa nne usiku.

Abdallah alisema chanzo cha moto huo ni mtungi wa gesi uliokuwa ukitumika kuwasha jokofu la kuhifadhia chanjo kulipuka na kusababisha vifaa vingine kushika moto ambavyo havijajulikana thamani yake.

Aidha, alisema hatua inayochukuliwa na halmashauri kwa kushirikiana na wilaya hiyo ni kujenga mahema ili kuendelea kutoa huduma za kinamama na watoto.

"Hapa halmashauri itakaa na kuangalia jinsi ya kusaidia wananchi kuwapatia huduma hasa kinamama na watoto, huku wengine wakitembelea taasisi au vijiji jirani kufuata huduma," alisema Abdallah.

Alisema kuwa vifaa vilivyoungua kwenye zahanati hiyo ni vitanda, dawa na vifaa vya kitabibu, hali inayosababisha huduma kusimama hadi pale ujenzi mpya utakapo fanikishwa.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kitongoji cha Butulage ambaye ni shuhuda wa moto huo, Jawadu Ibrahimu, alisema wananchi walifika na kuanza kuzima moto huo, lakini jitihada hazikuweza kufanikiwa. Hata hivyo Ibrahim alisema kulingana na jiografia ya kijiji hicho, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halikuweza kufika ndipo walianza kutumia maji na mchanga.

Naye katibu Tawala wa Wilaya hiyo Abdallah Mayombo aliyefika eneo hilo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya Missenyi, Kanali Denis Mwila, alisema kuwa kamati ya ulinzi na usalama itafanya uchunguzi na kubaini chanzo hicho.

# Umati wajane wamiminika kwa Makonda haki mirathi

**Na Mary Geofrey**

MAELFU ya wajane wa Mkoa wa Dar es Salaam wamemiminika katika ukumbi wa mikutano wa Mlimani City, kuitikia wito wa Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda, kwa ajili ya kuwasilisha kero zao ili zitafutiwe ufumbuzi.

Kutokana na idadi hiyo kuwa kubwa kulinganisha na matarajio, wanawake wengi walishindwa kuenea katika ukumbi huo na wengine kujikuta wakiishia nje, wakinyeshewa na wengine kukata tamaa na kurudi nyumbani.

Aidha, changamoto kubwa zilizoonekana kuwakabili wajane wengi waliohudhuria kongamano hilo ni kudhulumiwa mali, mirathi, tatizo la uchumi na malezi.

Nipashe lilishuhudia pia wanawake ambao walifika hapo kwa matarajio ya kupata fedha na wengine kupata ufumbuzi wa papo kwa papo pamoja wakilalamikia wimbi la watu wengi na eneo lililotumika.

Akizungumza katika kongamano hilo, lililowakutanisha wanasheria, asasi za kutetea wanawake kikiwamo, Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), Chama cha Wajane (Tawia) na watetezi wa haki za binadamu, Makonda alisema lengo la kongamano hilo ni kuwapa elimu, msaada wa kisheria na kutafutia suluhu changamoto zinazowakabili.

**INAENDELEA UK. 8**

# Uamuzi wa JPM wakuna w'biashara

**Na Mary Geofrey**

JUMUIYA ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT), imempongeza Rais John Magufuli kwa kuiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuangalia upya viwango vya ulipaji kodi kwa lengo la kuziba mianya ya ukwepaji kodi.

Kauli hiyo ya JWT wameitoa jana jijini Dar es Salaam baada ya Rais Magufuli kutoa agizo hilo Ikulu Jumatatu alipokuwa akiwaapisha Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha atakayeshughulikia Sera, Adolf Ndunguru na Naibu Kamishna Mkuu wa TRA, Msafiri Mbibo.

Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma wa JWT, Stephen Chamle, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa, wanaunga mkono kwa kuwa wafanyabiashara wa kati na wadogo ndio waathirika wa mifumo ya kodi nchini.

Alisema katika mkutano wa wadau kwenye mabadiliko ya Sheria za Kodi Mwaka wa Fedha 2019/20 walitoa mapendekezo ikiwamo kuanzishwa kanda za kibiashara ambazo zitavutia uwekezaji kutoka nchi za Afrika Mashariki.

"Hii itasaidia kuvutia biashara kubwa Tanzania na tunapendekeza maeneo yatakayofaa ikiwamo Kariakoo, Mwanza, Tanga, Songwe, Mtwara, Dodoma pamoja Kigoma," alisema Chamle.

Chamle alisema kwa upande wa Forodha walishauri serikali itazame upya kodi elekezi kwa bidhaa zote zinazoingia ndani ya nchi kama ilivyo kwenye magari.

Aliongeza kuwa kodi elekezi ikirudi na kusimamiwa kwa dhati zitakata kabisa mzizi wa rushwa uliokithiri na ukwepaji kodi uliopo kwenye Idara ya Forodha.

Akizungumzia kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), alisema walipendekeza kuondoshwa kwenye maduka na irejeshwe kwenye vyanzo vya bidhaa kama viwandani, mipakani, bandarini, viwanja vya ndege na wasambazaji wakubwa.

"Ili kuziba pengo dogo litakalojitokeza, kiwango cha VAT kutoka asilimia 18 hadi 21 na kuondoa msururu wa kodi, udanganyifu wa nyaraka na kuliacha soko kuwa huru na itachochea ustawi wa biashara nchini," Chamle alisema.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ulinzi watoto muhimu kudhibiti udhalilishaji

**MATUKIO** ya udhalilishaji wa wanafunzi hususan katika shule za msingi yameendelea kuripotiwa kwa kasi ya kutisha katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Ni vitendo ambavyo vinaonekana kutendeka na kushamiri pengine kutokana na kutokuwapo utaratibu wa kuwafuatilia watoto pamoja na kuwalinda.

Ulinzi wa watoto ni muhimu kuanzia nyumbani, njiani na shuleni, hivyo jukumu la kuwalinda wasidhurike linaanzia kwa wazazi, walimu na jamii nzima.

Umuhimu huo unatokana na kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji dhidi ya makundi ya watoto na wanawake vikiwamo ubakaji, ulawiti na unajisi.

Matukio mengi ya aina hii yamekuwa yakiripotiwa katika vyombo vya usalama na mengine hayaripotiwi katika mamlaka husika kutokana na sababu mbalimbali.

Tumeamua kulizungumzia suala hili kutokana na kuripotiwa tukio la zaidi ya wanafunzi 20 wa Shule ya Msingi Nyasubi katika Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, kuripotiwa kufanyiwa matukio ya udhalilishaji, huku wengine wakifanyiana wenyewe kwa wenyewe. Vitendo hivyo vimetajwa kuwa ni ubakaji, unajisi na ulawiti.

Inadaiwa kuwa mtoto wa shule ya awali alinusurika kubakwa na mtu asiyejulikana baada ya kukutwa na wasamaria wema akiwa ameshavuliwa nguo ili kufanyiwa kitendo hicho, na kwamba wasamaria wema walimkuta mtoto akiwa katika nyumba ambayo haijaisha bila nguo na kuamua kumchukua hadi shuleni kwao na kumkabidhi kwa mwalimu mkuu wa shule hiyo. Ilielezwa kuwa mwalimu huyo alichukua jukumu la kumpeleka hospitali kwa ajili ya uchunguzi na kubainika alikuwa hajaingiliwa.

Kwamba mkuu wa shule hiyo alitoa taarifa hiyo katika kikao maalumu cha shule kilichojumuisha wazazi, walimu pamoja na watu wa dawati la jinsia kutoka Jeshi la Polisi, kilichoitishwa na kamati ya shule ili kujadili tatizo hilo ambalo limeibuka shuleni hapo la wanafunzi kufanyiwa vitendo vya ulawili, ubakaji na unajisi. Alibainisha kuna mtoto wa miaka minne aliyekuwa akitoka nyumbani kwenda shuleni na kukutwa njiani akitembea mwendo wa kunyong'onyea, huku kinyesi kikimtoka na alipoulizwa alisema kuwa, aliitwa na vijana waliokuwa katika jengo ambalo halijaisha na kumfanyia vitendo hivyo.

Hata hivyo, alisema, pamoja na kumwita mzazi wa mtoto huyo kwenda shuleni kwa ajili ya kuambiwa tukio lililompata mwanawe, mzazi huyo hakuitikia wito huo.

Kuhusu ulawiti, shule ilifanya uchunguzi na kuwabaini watoto 15 waliolawitiwa, kati yao 12 walionekana wakihusika na vitendo hivyo kwa njia moja au nyingine, na tisa walikutwa na uzoefu wa kujamiiana, mmoja akiwa tayari sugu katika masuala hayo.

Ofisa wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Polisi Kahama, Koplo Njile, alisema kuwa watoto zaidi ya 20 wana madhara ya kulawitiwa, huku kesi nyingi za matukio hayo ni kutoka katika shule hiyo na shule za msingi Kilima, Korogwe na Mhongolo.

Hakika ni matukio yanayosikitisha, lakini jambo la msingi ni wazazi, walimu na jamii kushirikiana katika jukumu la kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya udhalilishaji.

Tunakubaliana na ofisa huyo wa dawati la jinsia kwamba vitendo hivyo vimekuwa vikiongezeka kila siku kutokana na wazazi kutofika shuleni kufuatilia maendeleo ya watoto wao, badala yake wakiwaachia majukumu hayo walimu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa na kazi nyingi.

Tunawahimiza wazazi watambue kuwa wao wanawajibika zaidi katika jukumu la ulinzi wa watoto wao, hivyo wawe mstari wa mbele kuhakikisha watoto wao wako salama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tujipange kupitia jukwaa 'Naweza' kutetea afya zetu

Na Mary Geofrey

**WIKI** iliyopita Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, walizindua jukwaa lijulikanalo kama Naweza mkoani Iringa.

Jukwaa hilo la mawasiliano ya afya kwa watu wazima linalenga kuleta mabadiliko chanya ya tabia kwa jamii, pia ya kusaidia kufikisha ujumbe na taarifa zitakazowajengea uwezo Watanzania, wabadilishe tabia zao za kiafya.

Pia, linalenga kuimarisha afya ya kila mmoja, familia na afya ya jamii nzima, pia kumuwezesha Mtanzania kujitambua kuwa, anaweza kujiwekea nia ya kuishi maisha bora zaidi.

Jukwaa hilo linalenga kutoa huduma jumuishi za afya kwa pamoja, katika kubadilisha tabia katika maeneo muhimu matano ya afya ambayo ni Ukimwi, Malaria, Afya ya Uzazi kabla baada ya kujifungua, Afya ya Mama na Mtoto na Kifua Kikuu (TB).

Lingine ni kwamba linawasogeza walengwa kufikiwa na mawasiliano ya kuwahamasisha kubadili tabia, kulingana na mahitaji na vipaumbele vya wakati husika wa maisha yao, kama vile kipindi cha ujauzito au wakati wa malezi ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Kwa msingi huo, linatoa uhakika wa kuwafikia watu wazima na kuhakikisha wanapata taarifa kikamilifu, wanahamasika na kupata maarifa yatakayowawezesha kubadili tabia zao kiafya, kwa wakati na uhitaji wao.

Naweza inalenga kuhakikisha taratibu zinazozuia mapokeo na mwendelezo wa tabia hizo chanya, pia zinalengwa kupitia jukwaa.

Hivyo, litafanya kazi kupitia mifumo yote ya mawasiliano, vikiwamo vyombo vya habari, uhamasishaji jamii, mawasiliano ya ana kwa ana baina ya watu na mitandao ya kijamii.

Martha Shakinyau, ni mwakilishi kutoka Wizara ya Afya, Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, anayeeleza kwa kina kuwa lilianzishwa kujenga na kuimarisha uzoefu wa nchi katika mawasiliano yanayolenga kubadili tabia katika jamii kwa usahihi, ili kuiwezesha serikali kufanikisha mikakati ya afya, kulingana na vipaumbele vya taifa.

Anataja vipaumbele hivyo vinajumuisha malengo kama vile kupunguza maambukizi vya Ukimwi, vifo vitokanavyo na uzazi, vinavyohusu watoto wachanga, malaria na kifua kikuu.

Katika hilo tumefahamishwa, Tanzania imejitahidi kubuni namna mbalimbali za kuhamasisha jamii kwa jitihada kubwa na kwa wakati husika kupitia kampeni za mara kwa mara.

Naweza itaunganisha jitihada za wadau wote wanaotekeleza miradi ya mawasiliano ya kubadili tabia katika jamii, ikijikita kutoa elimu na maarifa kwa jamii, familia na vikundi rika, ili kuwapa ari ya kuboresha afya zao na kuishi maisha ya furaha, yakiratibiwa na kuunganishwa chini ya jina moja na jukwaa moja.

Naweza imejikita na vipaumbele vya mikakati ya kiafya ya serikali kwa ukaribu, ikitilia mkazo maeneo ya afya yanayoakisi malengo, mikakati na juhudi za serikali.

Martha anasema tabia chanya ambazo Naweza inazipa kipaumbele, zimetokana na makubaliano ya wadau muhimu, zikiendeleza mikakati iliyoainishwa katika machapisho rasmi ya kitaifa na maamuzi ya kisera.

Anataja maeneo muhimu yatakayowezeshwa na jukwaa mkakati wa taifa wa kuboresha afya ya uzazi, kinamama, watoto wachanga na vijana nchini, akitaja mkakati wa nne wa taifa wa kudhibiti Ukimwi wa mwaka 2018 hadi 2020 na Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Malaria wa mwaka 2014 hadi 2020.

Anasema Mkakati wa Taifa wa Tano wa Mwaka 2015 wa kutokomeza Kifua Kikuu na Ukoma ni maeneo ambayo watagusa kwa kina.

Jukwaa hilo linaoanisha njia mbalimbali za kufikia walengwa na mawasiliano ya kiafya chini ya jina moja Naweza. Ni jukwaa linalotofautiana na kampeni nyingine za afya, zinazolenga maeneo mahususi ya kiafya, huku shughuli zikifanyika kwa kipindi maalum.

Naweza sio mbadala wa kampeni zilizopo za afya, Isipokuwa itahakikisha programu hizo zinaendelezwa na kukuzwa zaidi kama vile ile kampeni ya taifa ya Jiongeze.

Tukiungana na Martha, hii ni fursa ya kuzungumza na watu binafsi, familia au kaya na jamii kwa namna chanya, kupitia nyenzo kama vile kadi mahususi za ushauri zinazotolewa vituo vya huduma za afya, maigizo katika ngazi ya jamii na vipindi vya redio vya kila wiki ili kuwashawishi wapokee na kukubali tabia chanya za kiafya.

Jukwaa hilo la watu wazima linalenga watu wenye umri kati ya miaka 18 hadi -45 na jukwaa la vijana ni kwa nye umri wa miaka 15 hadi 24 na kwamba litaelekezwa kupitia magonjwa malaria, kifua kikuu, mama na mtoto, huduma za afya ya uzazi kabla na baada ya ujauzito, VVU na Ukimwi.

# Bunge lawatosa wabunge mikopo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema kwa sasa Bunge litalazimika kutowadhamini tena wabunge kuchukua mikopo benki baada ya kubaini baadhi yao wanapata changamoto ya msongo wa mawazo kutokana na madeni makubwa.

Sambamba na hilo, amesema madeni hayo yanaweza kusababisha wakati mwingine fedha za walipa kodi kutumika kulipa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, alisema katika mtihani mkubwa ambao Bunge linao kwa sasa ni madeni ya zaidi ya Sh. bilioni moja yaliyokuwa ya wabunge wa Chama cha Wananchi (CUF) waliotimuliwa.

"Katika mtihani tulionao ni huu wa wabunge wale nane sijui 10 wanadaiwa zaidi ya bilioni moja na hawana uwezo wowote wa kulipa na mikataba ile ipo ovyo ovyo kama watakazia wale jamaa kuna kiwango fulani cha fedha ya walipa kodi inaweza kutumika kulipa madeni ya ovyo," alisema.

Alisema wamebaini tatizo hilo kuwa na sera ya ovyo ya mikopo ndani ya Ofisi ya Bunge ya kudhamini wabunge na kwamba watabadilisha ili kudhibiti hali hiyo.

"Ndio maana ninasema ukweli ninachosema ni ukweli watu wanaweza kunilaumu wakafanya hivi lakini ninachoeleza ni ukweli bahati mbaya nchi yetu sasa hivi ndio hiyo taarifa zinazoenda sio zile sahihi."

"Lakini tumejifunza huko mbele vitu hivi havitakuwapo kwa sababu taasisi za kukopa siku hizi ni nyingi nenda kakope mwenyewe wakikupa mahela yao mtaishia mahakamani huko wenyewe mtajuana kama Mtanzania mwingine yeyote anavyokuwa treated kwenye masuala ya mikopo," alisema. Aliongeza "Sio tu kwa sababu umekuwa mheshimiwa unachukua tu mahela ya watu halafu just like that sio huyo peke yake (Lema) ni wengi, lakini reaction ya mtu katika matatizo inatofautiana.

Ndugai alisema anaweza asiwe peke yake anayedaiwa lakini inaelekea ina mchanganyika sana.

"Ni maoni yangu mimi, lazima uangalie hivi hii tabia unayoiona ni ya mtu wa kawaida mara siogopi risasi hujawahi kupalazwa unaweza kusema huogopi risasi wewe apo mi naogopa ukiona huogopi una tatizo," alisema.

Alieleza kuwa mtu ambaye ni timamu anawezaje kusema hivyo.

"Tungekuwa na utaratibu tungempeleka Mirembe wakampime ila hatuna utaratibu wa kulazimisha hilo. Kuna watu wana madeni makubwa mara 10 ya hayo lakini hayamchanganyi mtu, na hili suala sisi Bunge 'next time' niwepo nisiwepo tutawarithisha watakaokuwapo," alisema.

# Madiwani walia njaa, wampa DED siku 30 kuwalipa posho

**Na Ibrahim Yassin,** MOMBA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba mkoani Songwe, wamempa siku 30 Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Adrian Jungu, awe amewalipa posho zao za miezi 15 pamoja na kupeleka makato yatokanayo na madeni waliyokopa benki.

Wakizungumza kwenye kikao cha baraza la madiwani, walisema kitendo alichokifanya mkurugenzi huyo cha kutowalipa posho zao ni ukiukwaji wa sheria za utumishi.

Colleta Mwaselela, Diwani wa Mkomba (CCM), aliibua hoja hiyo akitaka kujua sababu za mkurugenzi huyo na timu yake kutowalipa fedha zao wakati ni haki yao ya kikatiba.

Alisema kwa kipindi chote cha miezi 15 wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu kutokana na kutopata malipo yao, hali iliyowalazimu kuuza kuku ili kupata fedha za mafuta ya pikipiki ili kuwafikia wananchi kupokea kero zao vijijini.

"Mimi pia nilikopa benki, lakini sikukopa asilimia 100, kuna fedha ambayo inabaki baada ya benki kukata fedha zao," alisema na kuongeza:

"Lakini kiasi hicho sipati na hata benki pesa hazijapelekwa, tunataka mkurugenzi atueleze fedha ziko wapi na kwanini kafanya hivyo."

Norasto Simbeye, Diwani wa Mpapa (CCM), alisema kukosekana kwa malipo hayo kumewaweka katika hali ngumu kwa wananchi kwa kutowafikia kutokana na ukata, hivyo aliiomba halmashauri iwalipe fedha zao ili kuwafikia wananchi.

Prosper Nyalali, Diwani wa Kamsamba (Chadema), alisema ni kitendo cha mkurugenzi kutowalipa fedha zao kimewaathiri kwa kuwa wanaishi, na kumtaka alithibitishie baraza sababu na ni lini atalipa fedha hizo.

Mathew Chikoti, mwenyekiti wa halmashauri hiyo, alikiri kutokulipwa na kueleza kuwa madiwani wenzake walikuwa wakimueleza tatizo hilo ambalo hata yeye alisema alifuatilia bila mafanikio, hoja zao zina mashiko.

"Kutokana na hali hii ninamuagiza mkurugenzi alipe fedha zote wanazodai madiwani ili wakafanye kazi ya kuwatumikia wananchi kwa moyo mmoja...kitendo hiki si kizuri, naomba kisijirudie tena kinadhalilisha madiwani," alisema Chikoti.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri hiyo, Adrian Jungu, alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo, na kusema atazilipa fedha hizo kama alivyotakiwa.

Alisema kuwa tatizo la upungufu wa vyanzo vya mapato ya ndani ni moja ya changamoto iliyopelekea madiwani wasilipwe kwa wakati.

"Nimepokea maagizo ya baraza, na nitajitahidi kuzilipa fedha hizo kwa muda huo, pia naomba madiwani na watendaji tuendelee kubuni na kuibua vyanzo vipya vya mapato kwa kuwa hali ya ukusanyaji wa mapato Momba ni changamato," alisema.



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, akizungumza na wafuasi wa chama hicho kwenye ofisi ndogo zilizopo Barabara ya 20 jijini Tanga, ikiwa ni muda mfupi baada ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Tanga kuzuia mkutano wao. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Jela miaka 30 kumpa ujauzito mwanafunzi

**Na Happy Severine,** MASWA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, imemhukumu kifungo cha miaka 30 mkazi wa Kijiji cha Igunya, Sunzu Mpangala (27), baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kumbaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa sekondari.


Mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Tumaini Marwa, mwendesha mashtaka Inspekta Nassib Swedi, alidai kuwa mtuhumiwa alitenda kosa hilo Juni 16, mwaka jana, majira ya saa 11 jioni huko katika kijiji cha Igunya Kata ya Shishiyu.

Swedi alidai kuwa mtuhumiwa huyo alikuwa akimfundisha mwanafunzi huyo wakati wa likizo akiwa anasubiri ajira serikalini baada ya kuhitimu shahada ya elimu kutoka Chuo Kikuu cha UDOM. Mwendesha mashtaka alidai kuwa mtuhumiwa alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu namba 60 A(3) cha Sheria ya Elimu Sura ya 353 kama ilivyofanyiwa marekebisho ya sheria ndongo namba 2 ya mwaka 2016.

Mtuhumiwa alipopewa nafasi ya kujitetea, alikiri kutenda kosa hilo na kuiomba mahakama ijaribu kumpunguzia adhabu kwa kuwa hana wazazi na anategemewa na familia.

Hata hivyo, Swedi alipinga hoja hiyo na kuiomba mahakama itoe adhabu kali kwa mtuhumiwa huyo ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia kama hizo kwa kuwa wamekuwa wakikatisha ndoto za wanafunzi.

# Umati wajane wamiminika kwa Makonda



INATOKA UK. 5

"Nimekuja kuwatia moyo, kuwapa tumaini na kusema na mioyo yenu na nimeamua kuwaomba viongozi wa kiroho na watu waliobobea katika mambo haya, kuwasaidia kuondokana na manyanyaso na kuonewa," alisema Makonda.

Alitaja sababu ya kuwapo kwa unyanyasaji kwa wajane ni kutokana na upungufu wa sheria, upungufu wa wanasheria wenyewe na kuahidi kuwa baada ya kusikiliza malalamiko hayo watatoa mapendekezo kwa viongozi wa ngazi za juu kuhusu maeneo ambayo wamebaini yana changamoto ili zipatiwe ufumbuzi.

Makonda (pichani) alisema pia atashughulika na suala la mirathi ili kuwapo kwa sheria madhubuti zitakazosaidia kutokuwapo na malalamiko na kero zinazowatesa wajane hasa katika siku za usoni. Kupitia kongamano hilo, wajane wote waliofika, walipewa fomu ambazo walitakiwa kujaza kuhusu tatizo linalomkabili, hali ya kesi ilipofikia, namba ya simu na eneo anapopatikana, walioamua kujitolea kufanya kazi hiyo bila malipo yoyote.

Kadhalika aliwasihi wajane hao kutokubali kuwatelekeza watoto wao kwa sababu kuna mambo mengi mabaya yanayoendelea mitaani ambayo yataharibu maisha yao.

Mkuu huyo wa mkoa pia aliwasihi wajane hao kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kwa ajili ya kuwa na uhakika wa matibabu pindi watakapougua ili kuwapunguzia mzigo.

Naye mwanafunzi wa Sheria katika Shule ya Sheria, Allan Charles, alisema wametoa msaada wa kisheria kwa wanawake hao na idadi kubwa wanakabiliwa na changamoto ya kudhulumiwa nyumba, mashamba, mali na tatizo la uchumi." Mwenyekiti wa Chama cha Wajane Wilaya ya Kinondoni (Tawia), Ester Shoni, alisema wajane waliofika hapo wengi hawana uelewa wa namna ya kutafuta haki zao. Alisema pia wamewaelekeza namna ya kueleza matatizo yao katika fomu walizopewa na pia kusikiliza maelekezo ya namna wanaweza kupata haki zao.

# Lema tena kifungoni hadi 2020

INATOKA UK. 3

huenda Lema ana msongo wa mawazo kutokana na kuwa na deni litokanalo na mkopo wa Sh. milioni 644.

**TAARIFA YA KAMATI**

Pendekezo la Bunge kuazimia kumfungia Lema kuhudhuria mikutano mitatu, lilitolewa jana asubuhi na Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Emmanuel Mwakasaka.

Mwakasaka alisema wakati wa mahojiano, Lema aliieleza kamati kwamba anaunga mkono maoni yaliyotolewa na CAG Assad na Mdee ambao Kamati iliwakuta na hatia ya kulidharau na kulidhalilisha Bunge.

"Kwa hali hiyo, kamati iliona kwamba naye (Lema) ametenda kosa hilo kwa mujibu wa Kifungu cha 26 (e) cha Sheria ya Haki, Kinga, Maadili na Madaraka ya Bunge Sura ya 209 pamoja na 74 Fasihi 1A na B ya kanuni.

"Katika uchunguzi wake, kamati ilirejea katiba, kanuni, sheria na taratibu na uamuzi mbalimbali na video iliyomrekodi Lema akizungumza.

"Kamati ilijiridhisha kwamba Lema alitamka kwa makusudi maneno kuwa Bunge ni dhaifu akilenga kulidhalilisha Bunge. Kamati ilitilia maanani na kufuatilia kwa kina na ushahidi wa Lema mbele ya kamati ikiwamo kwa kukiri."

Alisema kamati iliona Lema alitenda kosa la kudharau na kulidhalilisha Bunge, hivyo ilimtia hatiani kwa kuwa kitendo alichokifanya kinapaswa kupigwa vita ili kulinda heshima ya Bunge.

Alisema na kwa kuwa Aprili 2, mwaka huu, Lema alipokuwa akichangia hoja ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri lililokuwa likimkabili Halima, alinukuliwa akilieza Bunge kwamba yeye ni mbunge wa vipindi viwili na anathibitisha kwamba Bunge ni dhaifu.

"Kiti kwa mamlaka yake yanayoainishwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kilimpeleka Lema mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa ajili ya uchunguzi wa kauli yake iliyoonekana kudharau Bunge kwa kuliita dhaifu," Mwakasaka alisema.

Aliongeza kuwa pendekezo la kumfungia Lema mikutano mitatu limetolewa na kamati yake kwa kuzingatia ni mara ya pili kuitwa mbele ya kamati hiyo. Mara ya kwanza Lema alitiwa hatiani na kamati hiyo kwa makosa ya kudharau Bunge na mamlaka ya Spika kwa kufanya vurugu bungeni Januari 27, 2016 na alipewa adhabu kwa kusimamishwa kuhudhuria vikao vyote vya mkutano wa tatu wa Bunge la 11.

"Na kwa kuwa Lema akiwa mbele ya kamati hakujutia kosa lake wala kuomba radhi kwa kitendo chake cha kudharau Bunge, bali aliendelea kusisitiza kuwa Bunge hili ni dhaifu, jambo ambalo linadhihirisha alidhamiria kutenda kosa hilo, na kwa kuwa Lema ni mbunge mkongwe kwa vipindi viwili, ana uelewa mkubwa wa kuzijua kanuni za namna ya Bunge linavyoendeshwa, kitendo alichofanya ni ukosefu wa heshima kwa mamlaka ya Bunge na kutokuwa na uwajibikaji wa pamoja.

**MICHANGO YA WABUNGE**

Baada ya kamati kutoa pendekezo la kupitisha azimio hilo, Spika Ndugai alitoa fursa kwa wabunge kuchangia, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika (Chadema), akilitaka Bunge lisiunge mkono pendekezo hilo akidai limekiuka kanuni za chombo hicho.

Mnyika alisema Lema alitoa kauli hiyo akiwa bungeni na kwamba mbunge huyo analindwa kwa misingi ya kanuni, hivyo akichukuliwa hatua itakuwa ukiukwaji wa kanuni na kuminya uhuru wa mbunge.

Alisema wakati Lema akitoa kauli hiyo, alipaswa kusimamama mbunge kumtaka athibitishe madai yake au afute kauli na kama asingefanya hivyo, ndipo afikishwe kwenye Kamati ya Maadili.

Mbunge wa Viti Maalum, Mariam Kisangi (CCM), alisema kwa kawaida uamuzi wa Kamati ya Maadili unazingatia maelezo ya shahidi, lakini kama Lema akifika mbele ya kamati na akaendeleza ubabe, anapaswa kuchukuliwa hatua.

Mbunge wa Tabora Kaskazini, Almasi Maige (CCM), alisema Lema, akiwa mbele ya kamati, alisema maneno mengi na kuiambia kamati ifikishe salama kwa Spika kwamba hakubaliana na namna anavyoendesha Bunge.

Maige alisema Lema tofauti na walivyotarajia kwamba angejitetea na kuomba radhi, aliitaka kamati isimwonee huruma wala kumsamehe huku akitoa maelezo mengi kuthibitisha kwamba Bunge la 11 ni dhaifu.

**KAULI YA SPIKA**

Baada ya wabunge kuchangia hoja hiyo, Spika Ndugai aliwahoji kama wanaunga au kupinga pendekezo hilo, wabunge wengi wakaridhia Lema kufungiwa mikutano mitatu.

Alitoa onyo kwa Lema kuwa popote aliko, akithubutu kulisema vibaya Bunge kwa lengo la kulidhalilisha au kulishushia hadhi kwa kuwa ataitwa tena kwenye Kamati ya Maadili huku akisisitiza kuwa ana uhakika hatachaguliwa tena kuwa Mbunge wa Arusha Mjini na mbunge huyo analijua hilo.

Wakati Bunge likichangia pendekezo la kamati kumpa adhabu Lema, wabunge wa Chadema walitoka kwenye Ukumbi wa Bunge kususa mjadala huo.

**WAANDISHI WAONYWA**

Kutokana na kitendo hicho, Ndugai aliagiza wabunge wote waliosusa mjadala huo wasirejee tena ukumbini hadi leo, huku akipiga marufuku wabunge hao kufanya mahojiano na vyombo vya habari kwenye Viwanja vya Bunge.

# JPM afungua kituo cha afya cha mil. 500/-

INATOKA UK. 3

unafanyika vizuri na amebainisha kuwa pamoja na kujenga miundombinu hiyo pia imejenga nyumba 306 za watumishi wa afya, imeajiri madaktari 11,200 na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na hospitali nyingine za rufani hali iliyowezesha nchi jirani kuitegemea Tanzania kwa matibabu.

Aidha, Rais Magufuli alikubali ombi la Mbunge wa Lulindi, Jerome Bwanausi, la kujengwa kwa kilometa 40 za barabara ya lami kati ya Mpeta na Newala na pia ameahidi kutoa gari la wagonjwa kwa ajili ya kituo cha afya cha Mbonde baada ya gari lililokuwapo kuchomwa moto wakati wa vurugu.

Rais Magufuli aliiagiza Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhakikisha viwanda vyote vya korosho vilivyobinafsishwa lakini havifanyi kazi vinanyang'anywa haraka na amemtaka Naibu Katibu Mkuu wa Viwanda, Ludovick Nduhiye kutoondoka Mtwara mpaka ahakikishe agizo hilo limetekelezwa.

# Nassari atoa kauli hatima Arumeru

INATOKA UK. 3

kuwa hizo ni propaganda zilizopangwa makusudi na wapinzani wake wa kisiasa.

"Wapuuzeni ni propaganda za maadui," Nassari aliweka wazi kuhusiana na madai yanayotolewa na baadhi ya watu.

Machi 14, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliitarifu Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwa Jimbo la Arumeru Mashariki lipo wazi kutokana na Nassari kupoteza sifa za kuendelea kuwa mbunge, ya kutohudhuria vikao vya mikutano mitatu vya Bunge mfululizo bila ruhusa ya Spika.

Mikutano ambayo Nassari anadaiwa kutohudhuria ni wa Septemba 4 hadi 14, 2018, Novemba 6 hadi 16, 2018 na Januari 29 hadi Februari 9 mwaka huu.

Hata hivyo, baada ya uamuzi wa Ndugai, Nassari alifungua shauri Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma kupinga uamuzi huo, lakini Ijumaa iliyopita mahakama hiyo ilitupilia mbali shauri hilo na kukubaliana na uamuzi wa Spika.

Jumapili NEC ilitangaza kuwa jimbo hilo lipo wazi baada ya tume hiyo kupokea barua kutoka kwa Spika na kutangaza mchakato wa uchaguzi mdogo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa NEC, Jaji Semistocles Kaijage, fomu za wagombea zitatolewa kuanzia Aprili 15 hadi 19 na kampeni zitaanza Aprili 20 hadi Mei 18.

# Wakazi wa Dar wahofia nyumba zao kubomolewa

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wakazi 50 wa eneo la Goba Kinzudi, Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam, nyumba zao zipo hatarini kubomolewa baada ya kudaiwa kuvamia shamba la Dorothy Kafanado na kujenga makazi yao.

Shamba hilo linadaiwa kununuliwa na Kafanabo mwaka 1992, lakini aliliacha bila kuliendeleza, hivyo wananchi hao kuvutiwa na kuamua kuvamia na kujenga nyumba zao.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe walisema viwanja hivyo walipewa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Yusuph Makamba.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye eneo hilo juzi, Kafanabo alisema eneo hilo alilinunua mumewe kwa ajili ya kujenga, lakini cha ajabu wananchi walivamia, hatua iliyoibua mgogoro.

"Ninaiomba serikali inisaidie ili kuhakikisha haki yangu inapatikana, kwa sababu hili ni eneo langu halali, lakini limevamiwa na wananchi," alisema Kafanabo.

Hata hivyo, wananchi wanaodaiwa kuvamia eneo hilo wamejitetea kwamba eneo lao lina ukubwa wa ekari 2.5, wakati mlalamikaji akisema lina ukubwa wa ekari 4.5.

"Tulienda serikali ya mtaa kwa ajili ya kusuluhisha mgogoro huu, ambapo huyu mama alisema ekari 2.5 ndiyo zake na watendaji wa serikali za mitaa walikuja na kupima, lakini cha ajabu amegeuka na kutaka ekari 4.5 wakati za kwake ni 2.5 na barua ya serikali za mitaa ipo," alisema Daniel Mushi, mmoja wa wanaodaiwa kuvamia eneo hilo.

Alisema kinachoshangaza ni kuona watendaji wa kata wanamkingia kifua, huku wakijua wanachokifanya sio sawa na kwamba kinaweza kuleta mgogoro.

Mkazi mwingine wa eneo hilo, Denis Mnuni, alisema kila mwananchi aliyenunua eneo hilo amefuata taratibu za kisheria na hati wanazo, hivyo wanashangaa kuona anadai hekari 4.5 wakati alizoandikisha serikali ya mitaa ni ekari 2.5.

"Serikali za mitaa tumeandikisha ana ekari 2.5 na zimepimwa na watendaji wa mtaa, lakini hapa kuna ekari 4.5 ambazo zimejengwa nyumba zaidi ya 35 na viwanja zaidi ya saba, hivyo basi kama anataka ni vema akagombana na waliojenga kwenye eneo lake la ekari 2.5, badala ya kuingiza migogoro kwa watu wasiohusika," alisema Mnuni.

Ofisa Mtendaji Kata wa Goba, Asia Mwenda, aliwataka wananchi hao kuwasilisha hati zao za viwanja pamoja na mlalamikaji ili waweze kuzipitia na kutoa uamuzi.

"Ninawaomba wananchi wote waliojenga kwenye eneo hili kuwasilisha hati zenu mlizonunulia viwanja ili tuweze kuzikagua, kwa sababu mlalamikaji ameshawasilisha hati zake," alisema Mwenda.

Aliongeza kuwa yeye hana uamuzi wa mwisho katika usuluhishi wa mgogoro huo na kuwa zipo mamlaka nyingine ambazo zitakaa na kuamua.



Taka zinazozalishwa na wafanyabiashara wa Soko la Kawe, jijini Dar es Salaam zikiwa zimetapakaa hadi njiani baada ya kizimba kujaa, kitu ambacho ni hatari kwa afya. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wataalamu Afrika wapata mafunzo vyanzo vya mionzi

**Na Mwandishi Wetu**

WATAALAMU wa ulinzi na usalama wa vyanzo vya mionzi kutoka katika nchi sita za Afrika wanashiriki katika mafunzo ya wiki mbili ya utoaji mafunzo ya ulinzi na usalama wa vyanzo vya mionzi yanaoendeshwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) kwa ushirikiano na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU).

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano cha Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, Peter Ngamilo, amesema mafunzo hayo yanafanyika jijini Arusha na watu 25 wanashiriki mafunzo hayo kwa lengo la kupata ujuzi wa namna ya kufundisha wataalamu mbalimbali wanaohusika na ulinzi na usalama wa vyanzo vya mionzi katika nchi zao.

Ngamilo amesema kuwa baada ya mafunzo hayo wakufunzi hao watakuwa na uwezo wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wenzao wa idara mbalimbali za kitaifa katika nchi zao katika kuhakikisha kuwa vyanzo vya mionzi vinatumika kwa njia zilizo salama na halali.

"Wakufunzi hawa waliopo kwenye mafunzo wakitoka hapa watakuwa na uwezo wa kuandaa na kufanya mafunzo ya ulinzi na usalama wa vyanzo vya mionzi kwa wadau mbalimbali katika nchi zao, pia watatumika kama wataalamu katika kushughulikia matukio yoyote ya maafa ya vyanzo vya mionzi iwapo yatatokea katika nchi za Bara la Afrika," Ngamilo alisema.

Hata hivyo, alisema vyanzo vya mionzi visipodhibitiwa vinaweza kutumika katika vitendo vya kigaidi na kuleta madhara makubwa kwa jamii na kuathiri shughuli za kimaendeleo na kiuchumi.

Aidha, alisema wakufunzi hao wanajengewa uwezo wa kutoa mafunzo ya kubaini usafirishaji haramu wa vyanzo vya mionzi hasa kwa wataalamu wa mamlaka za ulinzi na usalama ikiwamo polisi, walinzi waliopo mipakani na wasimamizi wa teknolojia ya nyuklia, maofisa forodha na wataalamu wa kupambana na majanga ya nyuklia.

Alizitaja nchi wanazotoka washiriki wa mafunzo hayo kuwa ni pamoja na Burundi, Uganda, Congo (DRC), Zambia, Ghana na wenyeji Tanzania.

# Maswa kujenga viwanda viwili

**Na Happy Severine,**
MASWA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu imetiliana saini na SUMAJKT mkataba wa ujenzi wa viwanda viwili.

Mkataba huo utahusu ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza chaki na kiwanda cha kutengeneza vifungashio.

Miradi hiyo ni ya kimkakati ambayo wilaya hiyo iliomba na kuidhinishiwa na serikali kiasi cha Sh. bilioni 8.2 na hadi sasa wamepokea Sh. bilioni 4.09, hivyo kuanza ujenzi wa viwanda hivyo.

Mkataba huo ulitiwa saini jana mjini Maswa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Fredrick Sagamiko na Meneja Operesheni Mradi Kanda ya Ziwa, Kapteni Fabian Buberwa. Viongozi kadhaa walishuhudia akiwamo Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, Paul Maige.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo Dk. Sagamiko alisema halmashauri imefikia uamuzi huo baada ya SUMAJKT kushinda zabuni walioitangaza kulingana na vigezo ambavyo waliviweka.

Alisema ujenzi huo ambao unatarajia kukamilika kwa miezi minne kuanzia sasa, na utagharimu zaidi ya shilingi bilioni 3. Ujenzi wa kiwanda cha chaki utagharimu Sh. 1,518,644,000 na ujenzi wa kiwanda cha vifungashio Sh. 2,182,711,000.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri, Maige, alilitaka shirika hilo kumaliza kazi hiyo kwa muda ambao wamekubaliana katika mkataba ili viwanda hivyo vianze kazi ya uzalishaji kwa kuzingatia ni sehemu ya vyanzo vyao vya mapato ya ndani.

"Ni vizuri sasa SUMAJKT mkamaliza ujenzi huu kwa wakati kwa sababu fedha za ujenzi zipo, hivyo ni vizuri mkamaliza kwa wakati ili vianze uzalishaji mara moja," alisema.

Kapten Buberwa alisema watahakikisha ujenzi huo unakamilika kwa wakati kama walivyofunga mkataba na kuahidi kufanya kazi kwa weledi mkubwa.

# Malipo ya viongozi mitaa, vijiji, vitongoji yafafanuliwa

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, amesema serikali inalipa posho ya wenyeviti wa vitongoji, vijiji na mitaa kwa kutumia asilimia 20 ya mapato ya ndani inayorejeshwa na halmashauri kwenye ngazi za msingi za serikali za mitaa.

Waitara alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Alfredina Kahigi, aliyetaka kujua wenyeviti wa vitongoji, vijiji na mitaa hupata posho ya Sh. 20,000 kwa mwezi kiasi ambacho ni kidogo ukilinganisha na kazi kubwa wanayoifanya.

"Je, serikali ni lini itaongeza posho kwa wenyeviti hao?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Waitara alisema kiasi hicho cha fedha kinategemea hali ya makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri yanayokusanywa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa sura 290.

Alifafanua kuwa mkakati uliopo ni kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha makusanyo katika vyanzo vilivyopo kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ili kujenga uwezo wa kulipa posho kwa viongozi hao.

Naibu Waziri huyo alisema viwango cha posho inayolipwa vinatofautiana kati ya halmashauri moja na nyingine kulingana na uwezo wa kifedha uliopo.


"Serikali inatambua kazi kubwa na nzuri inayofanywa na wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji katika shughuli za maendeleo, kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wa wenyeviti wa serikali za vijiji, mitaa, vitongoji na wajumbe wa serikali za vijiji pamoja na wajumbe wa mitaa za mwaka 2014 zilizotolewa kupitia Tangazo la Serikali Na. 322 na Na. 323," alisema.

Alieleza kuwa sifa zinazomwezesha mkazi wa mtaa, kijiji na kitongoji kuchaguliwa kuwa mwenyekiti au mjumbe wa serikali za mitaa ni pamoja na kuwa na shughuli halali inayomwingizia kipato. Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji kuwa viongozi hao hawana ofisi za kufanyia kazi na serikali ina mpango gani wa kuwajengea ofisi za kufanyika kazi ikiwa ni pamoja na wajumbe kupewa posho.

Akijibu maswali hayo, Waitara alisema kwa sasa mpango wa ujenzi wa ofisi ni wa halmashauri na vijiji hivyo anaamini watafanya hivyo kwa kutumia fedha walizojiwekea.

Alisema kama kuna sababu ya kulipwa posho watalipwa kulingana na mapato ya chini ya halmashauri na vitongoji.

"Kama kuna uwezo wa kulipa walipane, kama hawana uwezo basi wafanye kazi ya kuhakikisha fedha zinapatikana ili walipane posho maana ni kazi yao," alisisitiza.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisoma Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Serikali yawatangazia neema makandarasi

BUNGE limeelezwa kuwa serikali tayari imeshatoa zaidi ya Sh .bilioni 44 kwa ajili ya kuwalipa makandarasi wa miradi ya maji na zingine Sh. bilioni 44 zinatarajiwa kulipwa kabla ya Bunge la Bajeti kuisha.

Hayo yalibainishwa bungeni jana na Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Jumaa Aweso, wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Iramba Mashariki (CCM), Allan Kiula.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni lini hati za malipo za makandarasi zitalipwa kutokana na kazi kusimama katika Jimbo la Mkalama.

Pia katika swali la msingi, mbunge huyo alisema pamoja na mambo mengine, sera ya serikali ya awamu ya tano ni kuongeza asilimia za upatikanaji wa maji vijijini.


"Je, lini serikali itafanya utafiti wa vyanzo vya maji katika Jimbo la Mkalama ili kuwa na uhakika wa rasilimali hiyo na ni lini serikali itatoa fedha za kutosha kuwapatia majisafi wananchi wa jimbo hilo?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Aweso alisema katika mwaka wa fedha 2018/19 serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji imetenga kiasi cha Sh. milioni 450 kwa ajili ya kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo kame ya mikoa ya Singida, Mwanza, Tabora na Shinyanga.

"Utafiti huo utahusisha pia Wilaya ya Mkalama ambapo Sh. milioni 50 zitatumika," alisema.

Hata hivyo, alisema pamoja na utafiti unaotarajiwa kufanyika serikali imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya maji katika vijiji vya Ndunguti, Kinyangiri, Ipuli na pia inatekeleza miradi ya uchimbaji wa visima 24 katika maeneo mengine tofauti.

Aweso alisema ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama imetengewa kiasi cha Sh. bilioni 1.36 kwa mwaka wa fedha 2018/19.




**Habari zote na Augusta Njoji,**
DODOMA

# Ujenzi barabara ya Ifakara kuanza

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeshakamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya barabara kutoka Ifakara-Kihansi yenye urefu wa kilomita 126 ili kujenga kwa kiwango cha lami.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Elias Kwandikwa, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mlimba (Chadema), Suzan Kiwanga.

Katika swali lake, Kiwanga alihoji ni lini serikali itajenga barabara kutoka Ifakara hadi Mlimba mpakani mwa mkoa wa Njombe kwa kiwango cha lami kwa kuwa imekuwa kero kubwa kwa wananchi wa jimbo hilo.

Akijibu swali hilo, Kwandikwa alisema barabara ya Ifakara-Mlimba-Taweta-Madeke yenye urefu wa kilometa 220.22 inaunganisha mkoa wa Morogoro na Njombe katika kijiji cha Madeke.

"Barabara hii ni ya changarawe na udongo ambapo sehemu kubwa inapitika vizuri isipokuwa maeneo yanayohitaji kuimarishwa ili nayo ipitike wakati wote wa mwaka," alisema.

Kwandikwa alisema kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo serikali imeshakamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya barabara kutoka Ifakara Kihansi kilomita 126 ikiwa ni hatua ya awali ya kuanza mipango ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

"Hatua hiyo itawezesha kuunganisha sehemu ya barabara hiyo na kipande cha barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 24 kilichojengwa hapo awali kati ya Kihansi na Mlimba," alisema.

Kufuatia kukamilika kwa hatua hiyo, Naibu Waziri huyo alisema serikali imeanza kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Aidha, alisema katika mwaka wa fedha 2019/20 kipande kilichobaki kati ya Mlimba hadi Taweta kimewekwa kwenye mpango ili kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

"Serikali itaendelea kutenga fedha za matengenezo ili barabara hii iweze kupitika wakati wote wa mwaka wakati fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami zinatafutwa," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, Mhandisi Tumaini Magessa (kulia), akikagua machimbo mapya ya dhahabu Magwendwa, Kijiji cha Meresa, Kata ya Sunya, mpakani mwa Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Waswekwa rumande saa 48 kwa kumpelekea DC wito

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAFANYAKAZI wawili wa Kampuni ya Green Miles Safaris Ltd, waliompelekea Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, hati ya wito wa kuitwa na mahakamani wameishia kuswekwa rumande saa 48.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Ramadhan Mohammed, alisema alitumwa na ofisi yake kupeleka hati ya Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara ya Dar es Salaam kwa Mwaisumbe katika kesi namba 29 iliyofunguliwa na Green Miles Safaris Ltd, ambaye mkurugenzi wake ni Awadhi Ally Abdallah.

Mohammed, alidai yeye pamoja na mfanyakazi mwenzake, James Joseph, baada ya kufika ofisi ya masjala ya Mkuu wa Wilaya, karani wa masjala alikataa kuipokea.

Alisema alipowasiliana na ofisi yao Dar es Salaam, aliambiwa awasiliane na mwenyekiti wa kijiji, mtendaji ambao kwa pamoja wataipeleka hati hiyo nyumbani kwa Mkuu wa Wilaya.

Hata hivyo, alisema walimkuta mtendaji wa kijiji ofisini kwake, lakini naye alikataa kuipokea au kuwapa ushirikiano wa kwenda nyumbani kwa Mkuu wa Wilaya.

Alisema wakati wanatafakari nini cha kufanya na wakipata chakula cha mchana, ghafla likapita gari moja kuwachukua na kwenda nao kituo cha polisi ambako walijikuta wakiwekwa rumande.

Alisema hawakuelezwa kosa lao nini, lakini waliambiwa kuwa Mkuu wa Wilaya ndiye aliyetoa amri ya wao kuwekwa rumande.

Alisema waliwekwa rumande saa 7 mchana Jumatatu hadi Jumatano saa 6:30 walipoachiwa.

Akizungumzia suala hilo kwa njia ya simu jana, Mkuu wa Wilaya Mwaisumbe alisema alipata taarifa ya watu hao kusambaza barua za uchochezi kwa wenyeviti wa vijiji. Alidai barua hizo za uchochezi ziliamsha hasira ya watu ambao wangeweza kuhatarisha usalama wao, hivyo akaona ni vema wakawekwa sehemu salama zaidi.

Kuhusu hati ya kuitiwa mahakamani, alisema hajapewa, hajaiona na wala hana habari kama anatakiwa kupewa.

Hata hivyo, kwa mujibu wa hati hiyo iliyosainiwa na Naibu Msajili wa Mahakama hiyo, Machi 27, mwaka huu, Mwaisumbe anatakiwa mahakamani hapo Aprili 10, mwaka huu, binafsi au wakili wake au yeyote ambaye atapewa mamlaka ya kwenda kwa niaba yake.

Hati hiyo imeonya iwapo atashindwa kufika mahakamani siku iliyotajwa, mahakama itaendelea na kesi dhidi yake na hukumu kutolewa pasipo yeye kuwapo.

Katika hati ya mashtaka, kampuni ya Green Miles Safaris, ambaye ni mlalamikaji, kupitia kwa kampuni ya Law Associates Advocates, inasema, kauli alizotoa Mwaisumbe dhidi ya kampuni hiyo kuwa imeshindwa kutoa dola za Marekani 5,000 kila mwaka kuchangia shughuli za maendeleo kwa vijiji vinavyozunguka kitalu chao cha uwindaji siyo za kweli na zimechafua kampuni na masoko.

Kutokana na kuchafuliwa jina la kampuni na masoko yao, mlalamikaji anataka alipwe fidia dola za Marekani 230,000 kwa kuwa kauli za mlalamikiwa zimesababisha Green Miles Safaris kupata hasara katika biashara zake za uwindaji kwa mwaka 2019.

Aidha, imetaka mlalamikiwa kulipa fidia ya usumbufu ilioupata baada ya kutolewa kwa kauli hiyo katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Katika hatua nyingine, mlalamikaji pia anamtaka mlalamikiwa kuacha kabisa kuendelea kuizungumzia kampuni hiyo katika vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na blogu.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Mwaisumbe, aliagiza kusakwa na kukamatwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Uwindaji wa Kitalii, Awadhi Ally Abdullah, kwa kushindwa kulipa vijiji vinavyozunguka kitalu chake kiasi cha Sh. milioni 329.

Alitoa madai hayo wakati akizungumza na viongozi wa vijiji na kata vinavyozunguka kitalu hicho, Januari 15, mwaka huu.

# Wanawake wamwaga laana kwa waume zao

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

BAADHI ya wanawake wa Kijiji cha Ngereyani, Kata ya Tinga Tinga, Tarafa ya Enduiment wilayani Longido, wamelaani kitendo cha wanaume kuwaachia majukumu ya kifamilia kinyume na taratibu.

Akizungumza Maria Saningo mkazi wa kijiji hicho, alidai jamii ya kifugaji imekuwa ikiwatelekeza wanawake na majukumu ya kifamilia hali ambayo hulazimika kufanya biashara ya uuzaji wa mkaa ili waweze kuendesha familia zao.

Alisema wanawake wengi wa kifugaji wanatamani kuwa wajasiriamali, lakini kutokana na waume zao kuwanyima kufanya biashara wameishia kwenye uharibifu wa mazingira kwa kukata miti na kuchoma mkaa.

Alieleza wanawake wakipatiwa elimu na kuwezeshwa mikopo midogo midogo, wataweza kuondokana na adha ya uharibifu wa mazingira, kwa kuwa wanafanya hivyo kutokana na hali ngumu ya maisha wanayoishi.

"Hali ni ngumu na tumeachiwa majukumu, tunalazimika kuchoma mkaa, tulee familia zetu, naomba serikali itizame hili, watoto wanahitaji elimu, afya, chakula na mavazi twende wapi kama wanaume wanakwepa majukumu yao," alihoji Maria.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Ken ole Moloimet, alikiri kuwapo kwa tabia ya baadhi ya wanaume kuwaachia wanawake majukumu, nakuomba mashirika yenye uwezo wakuwawezesha wanawake hawa katika makundi ya ujasiriamali kujitokeza na kuwaunga mkono

"Ni kweli sipingi jamii ya Kimaasai wanawake ndiyo wanaowajibika kwa asilimia kubwa kulea na kutunza familia zao," alisema Moloimet.

Lakini pia niwatake wawe wavumilivu katika kipindi hiki kigumu kwa sababu uharibifu wa mazingira unasababisha ukame lakini pia tutakosa watalii kuja kutembelea hifadhi ya Enduiment kwa sababu ya mazingira si rafiki.

# Kamati ya siasa CCM yaridhishwa na miradi

**Na Alla Isack,** ARUSHA

WAJUMBE wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi, wilayani Arumeru, wameridhishwa na kasi ya utekelezwaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Arusha DC, baada ya kutembelea na kukagua miradi minne ya afya, maji, elimu na ujenzi wa miundombinu kwenye halmashauri hiyo.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua miradi hiyo, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Arumeru, Simon Saning'o, alisema katika ziara hiyo, wametembelea miradi minne yenye thamani ya Sh. bilioni 12.5.

Alisema wameridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo, baada ya kubaini kuwa miradi hiyo imejengwa katika ubora wa hali ya juu huku ikitumia kiasi kidogo cha fedha.

Aliongeza miradi waliyotembelea ni ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa, ofisi ya mwalimu mkuu wa Shule ya Sekondari Lengijave, mradi wa maji wa vijiji kumi, ujenzi wa Kituo cha Afya Manyire na ujenzi wa ofisi ya shule mpya ya sekondari Manyire.

Aidha, aliwapongeza wananchi kwa michango yao ya hali na mali mpaka kukamilika kwa miradi hiyo licha ya serikali na wafadhili kuchangia fedha kidogo.

"Niwapongeze wananchi wa halmashauri hii kwa kutambua umuhimu wa kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye maeneo yenu, juhudi hizi zimeonyesha uwezo wa taifa letu kuanzi harakati za kujitegemea na kuacha mpango wa kuwategemea wafadhili kutoka nje ya nchi," alisema Saning'o.

Licha ya kuzungumza hayo, Saning'o, alisema kamati ilibaini changamoto ya ucheleweshwaji wa miradi ya maji ya vijiji 10 inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, ambayo hadi sasa bado haijakamilika.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Angela Mvaa, alisema miradi hiyo ya maji ilianzishwa mwaka 2013, na ilisimama kwa muda mrefu, lakini kwa sasa serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi hiyo, japokuwa wanakabiliwa na changamoto ya mabadiliko ya tabia ya nchi wakati wa utekelezwaji wa miradi hiyo.

Aliongeza licha ya changamoto hizo, wameshakamilisha miradi ya vijiji vitano kati ya kuni na wananchi wameshaanza kutumia huduma ya maji na miradi mingine iliyobaki ipo katika hatua za mwisho za kukamilika.

Alieleza kuwa ujenzi wa miradi hiyo, imetekelezwa kwa fedha kutoka serikali kuu, mapato ya ndani ya halmashauri, michango ya wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi, mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na michango na nguvu za wananchi.

Mvaa aliitaja miradi iliyotembelewa na kamati hiyo ni ujenzi wa Kituo cha Afya Manyire, ujenzi wa maktaba na ukarabati wa bwalo la chakula katika Shule ya Sekondari Mlangarini, ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Sekondari Manyire.

Miradi mingine ni ujenzi wa madaraja katika Kata ya Laroi na Kijiji cha Mirongoine, ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Sekondari Kiranyi, ujenzi wa madarasa matatu katika Shule ya Sekondari Lengijave, miradi ya maji ya vijiji vijano maarufu kama WaterAid na mradi wa maji wa Loovilukuny na kivuko Matevezi.





# Askofu azungumzia kuwekeza kwa wenye mahitaji maalum

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ASKOFU mstaafu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Martin Shao, amesema uwekezaji kwa wenye mahitaji maalum ni huduma yenye faida kwa mtendaji na watendewa na kuifananisha kama benki isiyofilisika.

Dk. Shao alikuwa akizungumza na wadau mbalimbali wa maendeleo, wafanyabiashara, wanataaluma, viongozi wa dini na serikali pamoja na wanasiasa katika mkutano mkuu wa kwanza wa Taasisi ya Askofu Martin Fuatael Shao Foundation (BMFS).

"Tuwekeze katika benki hii kwa kutenda mema kwa sababu benki ya Mungu haifilisiki hasa kwa wanaowekeza kwa watu wenye mahitaji maalum ambayo ni huduma ya faida/baraka kwa mtendaji na mtendewa. Amhurumiaye maskini humkopesha Bwana (Mungu) naye atamlipa kwa tendo lake jema," alisema.

Katika taarifa yake kwa wadau hao, Dk. Shao ambaye ni mwasisi wa taasisi hiyo ameeleza kuwa mkutano huo wa kwanza unalenga kuwatafakarisha kuhusu wito wa kumfanya mwanadamu mwenzao aishi kwa furaha, amani, upendo na akijenga tumaini lenye uzima hapa duniani na hatimaye uzima wa milele baada ya maisha haya.

Kwa mujibu wa Askofu Shao, malengo makuu matatu yaliyomsukuma kuanzisha taasisi hiyo ni kusaidia wasiojiweza kufikia gharama za matibabu ya magonjwa ya moyo ikiwa ni pamoja na watoto wanaozaliwa na magonjwa ya moyo.

Malengo mengine ni kusaidia yatima na wahitaji kulipia gharama za huduma za afya na matibabu kwa kushirikiana na hospitali au vituo vinavyotoa huduma ya afya na ili kufikia malengo yao ya kielimu kwa kutoa udhamini kwa wanafunzi kuwawezesha kulipa gharama mbalimbali za masomo.

Mkutano huo pamoja na mambo mengine ulikuwa na lengo la kujikita zaidi kuona yaliyofanyika, changamoto zilizopo na kuchangia kwa mawazo kuhusu nini kifanyike katika kutunza malengo hayo makuu matatu ya taasisi hiyo.

Askofu Dk. Shao ameeleza zaidi kuwa katika utekelezaji wa wito huo, changamoto walizokutana nazo ni wazazi au walezi kutojali afya za watoto wao ambapo wanashindwa kukua vizuri.

Alisema watoto wana kua wakiwa na maradhi mbalimbali kwa sababu ya kutopimwa afya zao.

Jumla ya gharama zilizotumika katika matibabu kwa wahitaji hao kati ya mwaka 2016 hadi 2018 ni Sh. milioni 10,433,800.

Mpaka kufikia sasa, wanafunzi zaidi ya 3,035 wa Shule za Msingi katika Wilaya za Moshi, Siha na Hai mkoani Kilimanjaro ambao ni wanufaika wakuu wa huduma ya uchunguzi wa magonjwa ya moyo na afya kwa ujumla wake, wameiweka Taasisi ya Askofu Martin Fuatael Shao (BMFSF) katika orodha ya taasisi zinazoongoza kwa huruma katika mikoa ya kanda ya kaskazini.




Mkurugenzi wa Shirika la Connect Autism Tanzania na mwasisi wa Shule ya Kiwoce Open, Grace Anna Lyimo, akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro juzi, kuhusu namna ya kuwalinda watoto wenye usonji. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Serikali za mitaa zadaiwa vinara wa rushwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imesema serikali za mitaa katika Mkoa wa Kilimanjaro zinaongoza kwa kulalamikiwa kwa vitendo vya rushwa, baada ya kuripotiwa mara 35 katika muda usiozidi siku 90.

Sekta binafsi inafuatia kwa kuwa na kesi 12, idara ya mahakama kesi nane, idara ya afya kesi saba, ardhi kesi saba, idara ya elimu kesi sita, Jeshi la Polisi kesi tano, vyama vya ushirika tatu, mashirika ya umma mbili, chama cha walimu moja na vyama vya siasa moja. Hayo yamo katika taarifa ya Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Kilimanjaro, Holle Makungu, aliyoitoa kwa umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu.

"Takukuru imepokea taarifa na kuendesha mashauri 87 katika kipindi cha Januari hadi Machi 2019. Mashauri 37 yanahusu mashtaka dhidi ya ya rushwa na uhujumu uchumi katika baadhi ya wilaya za mkoa wa Kilimanjaro," alisema.

Mbali na mashauri hayo, Takukuru imejinasibu kufanikiwa kufanya udhibiti wa vitendo vya rushwa vilivyokuwa vikifanywa na baadhi ya watumishi wasio waadilifu katika Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida).

Alisema katika kipindi hicho Takukuru ilifanya udhibiti Nida, baada ya watumishi wake wasio waadilifu kushinikiza wananchi wasio na vyeti vya kuzaliwa wapeleke viapo (affidavit) kama kigezo cha kupata vitambulisho. "Walikuwa wanawaelekeza mawakili wasio waadilifu ambao huwajazia viapo bila hata ya kuwapo anayeemwapia, kisha wanajipatia fedha ambazo hatimaye Ofisa wa Nida anayehusika hupata mgawo wa fedha hizo kupitia wakili," alifafanua Mkuu huyo wa Takukuru.

Takukuru imesisitiza kuwa tayari uchunguzi umeanzishwa dhidi ya waliojihusisha na ulaghai huo na hatua za kisheria kwa wote waliohusika zitachukuliwa.

Kwa sasa wananchi wa Kilimanjaro hawahitaji tena kuwa na kiapo cha wakili kwa ajili ya vitambulisho vya taifa.

## Watu 115 wadakwa kwa kusafirisha dawa za kulevya

**Na Paul William,** MOSHI

WAFANYABIASHARA na wasafirishaji wa dawa za kulevya aina ya mirungi na bangi wapatao 115 wamekamatwa mkoani Kilimanjaro katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Hamisi Issah, amesema katika kipindi hicho jumla ya kilogramu 1168.1 za dawa za kulevya zimekamatwa.

Hali hiyo ni tofauti na kipindi kama hicho mwaka 2018, ambapo kulikamatwa watuhumiwa 139 wakiwa na jumla ya kilogramu 408.2

"Tumekuwa tukifanya misako ya mara kwa mara katika maeneo yote ya mkoa wetu ili kuwabaini wale wote wanaohusika kufanya biashara ya dawa za kulevya, ambapo juhudi hizo zimezaa matunda kwa kuwakamata wahusika pamoja na dawa hizo," alisema Kamanda Issah.

Alisema jeshi hilo kwa sasa limekuwa na morali ya kufanya operesheni kwa nguvu kubwa baada ya kuona viongozi wa serikali nao wamekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi za kupambana na biashara hiyo ambayo imekuwa ikishamiri.

Aidha, Issah alisema kwa sasa wameanza kufanya vikao na viongozi wa vijiji, vitongoji na kata ili kushirikiana kwa pamoja kutoa taarifa zitakazoweza kukomesha biashara hiyo kwa kuwa wao ndio wapo karibu zaidi na wananchi na wanawatambua wanaofanya biashara hiyo.

Katika hatua nyingine, kamanda huyo aliwataka wananchi kutoa taarifa pale wanapoona askari polisi wamewakamata wafanyabiashara hao wa dawa za kulevya na kuwaachia ili waweze kuchukuliwa hatua stahiki za kisheria.

Katika taarifa hiyo ya miezi mitatu inaonyesha kuwa kesi 81 za dawa aina ya mirungi zimefunguliwa Polisi, huku dawa zenye uzito wa kilogramu 904.9 zikiwa zimekamatwa na kwa upande wa bangi kesi 51 zimefunguliwa na dawa zenye uzito wa kilogramu 263.2, zikiwa zimekamatwa.



Ukurasa 14

Mfuko wa Ubunifu ulivyoanika mahali kona ya maendeleo iliko



Ukurasa 19

SIDO yakusanya wahitimu kwa mazito ya ujasiriamali


# BUFE

Ijumaa Aprili 5, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA





## Chuo Utalii chabuni mradi uliobeba sura tatu za neema

Ukurasa 18



# Utalii wa Utamaduni ulivyosafisha ujangili Mikumi, ukakaribisha uchumi mpya vijijini

**Ashton Balaigwa,** Morogoro

UJANGILI ni changamoto inayoikabili sekta ya utalii nchini na athari yake imepunguza baadhi ya wanyama kama tembo na faru ambao kihisitoria ni vivutio vikubwa vya biashara nje na ndani ya nchi.

Hiyo imeifanya serikali kuchukua hatua kuweka mikakati ya kuanzisha operesheni maalumu za kuwabaini wanaojihusha na ujangili. Unaelezwa ni matokeo ya vijana kukosa kazi ya kukimu maisha yao, hivyo wanahamia katika kuua wanyama.

Mikumi ni moja ya hifadhi tatu za Kanda ya Kusini iliyopo wilayani Kilosa kati ya 16 zinazosimamiwa na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Hifadhi hiyo iliyopo mkoani Morogoro, ilikuwa ikikabiliwa na tatizo la ujangili kutokana na kupitiwa na barabara kuu ya Dar es Salaam hadi Zambia kipande cha kilomita 50 unaotoa mwanya kwa majangili wanaotoka vijiji jirani na hifadhi hiyo.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Takwimu za Biashara Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

**Kielezo**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

## Biashara

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

| | |
|---|---|
| Mauzo | 109,584,255.00 |
| Hisa | 58,317 |

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

UCHUMI

# Mfuko wa Ubunifu ulivyoa mahali kona ya maendeleo

• Ole Nasha: Ubunifu kiwandani kuchochea muhimu • Costech: Hizi njia 30 zina kopita mabilioni ya ufadhili • DC Handeni achambua mtaji ulivyojificha kijijini

**Na Salome Kitomari**

UBUNIFU unatajwa kuwa suluhisho la matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii, iwapo kinachobuniwa kitakuwa ni kwa ajili ya kutatua changamoto zilizopo kwa wakati husika.

Maendeleo yaliyopo duniani kwa sasa, mengi yanaelezwa yametokana na ubunifu wa watu kwa kutumia teknolojia. Wamerahisisha maisha, kujibu changamoto zilizopo na kujibu maswali ya jamii husika.

Ubunifu unatajwa kuwezesha uwepo wa nyenzo za usafiri; ndege, magari, simu na vingine vingi ambavyo kwa kushirikiana na teknolojia, vimewezesha mawasiliano ya watu katu ya eneo moja na jingine kwa rahisi zaidi na kurahisisha maendeleo.

Hayo yote, yanatajwa kuwa ni matokeo ya binadamu kufikiri, baada ya kukutana na changamoto za kutafuta utatuzi.

Kama ilivyokuwa kwenye huduma za fedha kwa njia ya simu, ambayo kwa sasa ni maarufu barani Afrika, mtu anaweza kutuma fedha kokote na kwa wakati wowote, akatoa fedha benki na kufungua akaunti, tofauti na zamani zilitumika huduma za posta kusafirisha kwa mabasi na ndege.

Katika historia ya magazeti, inamrejea Johannes Gutenberg, aliyebuni mashine ya kutoa nakala mwaka 1468 katika mji wa Mainz nchini Ujerumani.

Huo ndio ukawa mwanzo wa kuzalisha vitabu, magazeti na machapisho mengine na kufikia mapinduzi ya mawasiliano kwa watu kirahisi na haraka zaidi.


Hata machapisho ya maandiko ya kiimani kama Bibilia na kisha yakafuatia maandiko mengine kama vitabu vilivyotumika kwenye shule na vyuo.

Wafanyakazi wa viwandani walitumia machapisho mbalimbali ya



Wanafunzi wakiendelea na kazi za ubunifu, katika moja ya kumbi za Tume ya Sayansi na Tekonolojia (Costech), jijini Dar es Salaam.

> **Kwa kweli tumejipanga sana labda wafugaji na wakulima washindwe kuja kuzikopa fedha hizo ili kujiendeleza.**



BIASHARA
Utalii wa Utamaduni ulivyosafisha ujangili Mikumi, ukakaribisha uchumi mpya vijijini
Ukurasa 16


UCHUMI
Chuo Utalii chabuni mradi uliobeba sura tatu za neema
Ukurasa 18

BIASHARA
SIDO yakusanya wahitimu kwa mazito ya ujasiriamali
Ukurasa 19

# anika
# o iliko

a-





kupaza sauti dhidi ya ukandamizaji, lakini yote yalifanikiwa kutokana na ubunifu wa Gutenberg.

**HDIF**

Mfuko wa Ubunifu na Maendeleo ya Binadamu (HDIF), kwa mwaka wa tano mfululizo sasa, unaandaa maadhimisho ya wiki ya ubunifu inayowaleta pamoja wabunifu mbalimbali wanaoonyesha kazi za kibunifu na kushindanishwa na baadaye kupewa zawadi ya fedha, inayowawezesha kuendeleza mawazo yao.

Maadhimisho hayo yanayokwenda sambamba na uzinduzi wa ripoti ya wekeza kwenye ubunifu wa kijamii na teknolojia Tanzania, ikiangazia ukuaji wa ubunifu kwa miaka mitano ambayo mashindano hayo yanafanyika.

"Ripoti yetu inaelezea kwa kina ukuaji wa mawazo ya kibunifu na jinsi ya kuijenga sekta ya ubunifu Tanzania. HDIF imekuwa ikiandaa programu za ubunifu zinazopewa Paundi milioni 40 (sawa na Sh. bilioni 124) ikiwa ni msaada kutoka Shirika la Maendeleo ya Ubunifu UKAid), katika maeneo ya elimu, afya na huduma za maji na usafi wa vyoo," anasema kiongozi wa HIDF, David McGinty.

Kiongozi huyo anasemna, HDIF itaendelea kusaidia shughuli za kibunifu nchini, ikiwamo kutoa maoni katika ripoti ya miaka mitano, ambayo itawapa mwongozo wanapowekeza, kubuni na kutekeleza miradi.

McGinty anaema, wanafanyakazi kwa karibu na serikali kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costech) na wadau wengine, kuhakikisha ubunifu unakuwa ni chachu ya maendeleo ya taifa.

Akitoa mfano, msaada wa UKAid imeshaipa serikali kupitia Costech, Sh. bilioni 1.3 kusaidia wabunifu wa chini na mshindi wa kwanza ni aliyekuwa na andiko la mwaka 2018.

**KUTOKA COSTECH**

Mkurugenzi Mkuu wa Costech, Dk. Amos Nungu, anasema tuzo ya HDIF itakwenda kwa miradi 30



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Tekonolojia, Willium Ole Nasha, akizungumza na wabunifu mbalimbali wakati wa ufunguzi wa wiki ya ubunifu jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: SALOME KITOMARI.**

kati yake 15 ni kwa wabunifu wa chini na 15 iliyopo kwenye kitovu cha ubunifu.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Tekonolojia, Willium Ole Nasha, anasema serikali inachukulia kwa uzito masuala ya ubunifu na ndiyo maana imeweka katika orodha ya mambo yanayopewa kipaumbele.

Anasema, Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa, umeweka viwanda kama kichocheo cha maendeleo ya uchumi wa kati na ili kufanikiwa katika eneo hilo, ni lazima shughuli za ubunifu zipewe kipaumbele.

"Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kufikia uchumi wa kati kupitia viwanda na mafanikio hayo hayawezi kufikiwa iwapo wabunifu wataachwa nyuma, ni lazima washiriki ili kutatua changamoto za mazingira ya Watanzania," anasema.

Ole Nasha anaeleza kuwa ni vyema kuwa na tekonolojia zinazoendana na changamoto za mazingira ya Watanzania, kwa kuwa nchi ikifanikiwa kuwa na viwanda vingi, ni lazima vizalishe bidhaa zinazitatua matatizo ya wananchi.

Anasema kwa kutambua umuhimu wa ubunifu, serikali imeongeza fedha za ubunifu kupitia Costech na wameanzisha dirisha maalum la wabunifu lililoleta pamoja vikundi 30 vinavyotumia tekonolojia, kufanya mambo mbalimbali.

"Katika kutambua umuhimu wa ubunifu Tanzania, tupo katika hatua za mwisho za kukamilisha sera ya sayansi, tekonolojia na ubinfu," anabainisha.

Aidha, anataka kujumuishwa watu wa kawiada kwenye maadhimisho hayo, ili kuondoa dhana kuwa ubunifu upo kwa ajili ya wenye elimu ya juu pekee, kwani hata watu wa kawaida wanatumia shida zao za kila siku kubuni vitu vya kutatua.

**INAENDELEA UK.20**

# Ijue saluni inayotembea



Darren Tenkorang, akiwa nje ya Saluni inayotembea. **PICHA: MTANDAO.**

KWA Waingerezeza wengi weusi, saluni za kiume ni mahali pa kubarizi, kupiga porojo na kukutana na marafiki. Baadhi hupoteza sana muda, jambo lililowafanya vijana wawili kuanzisha mtindo mpya, saluni ya kinyozi inayoendeshwa, ambayo unaomba huduma mapema kwa kutumia programu ya mtandao.

Basi dogo lililochorwa kwa rangi za kuvutia, linaendeshwa taratibu barabarani, yenye makazi ya watu eneo la Norwood, Kusini mwa London. Kijana mmoja akatoka nje akitizama simu yake ya mkononi , akampungia mkono dereva, ambaye aliegesha gari lake.

Walisalimiana, halafu akasukuma mlango wa basi dogo. Mara kikaonekana kiti cha kinyozi cha rangi ya chuma kinachong'ara, kioo kipana na kifaa cha kukausha nywele.

Kijana aliyekuwa amevaa vazi la kuzuia uchafu, akachomeka simu kwenye kipaza sauti ili kupata muziki.

Dereva ambaye kwa sasa ndiye kinyozi, Darren Tenkorang, anafanya kazi katika eneo dogo. Mlango bado uko azi, ili kuwezesha mwanga wa jua.

Kwa sasa ana mabasi madogo aina hiyo mawili yanayofanya kazi Kusini mwa London.

Darren anaamini anafanya kitu cha maana, akitamka: "Usafi wa mwanaume ni sehemu muhimu sana ya utamaduni wangu.Watu wa rika yangu kwa ujumla wanathamini mambo yanayofanyika kwa wakati na haraka zaidi ya kila kitu unaona."

Darren amekulia Brixton, Kusini mwa London, ambako mama yake alifanya kazi za usafi na baba yake mlinda usalama.Walifika London kutoka nchini Ghana miaka ya 1980 na alikuwa na ndoto ya kufanya kazi benki, wakili au mhasibu.

Alipenda sana kusoma chuo kikuu, lakini muda ulipowadia, hakuwa na uhakika taaluma ipi ingemfaa. Ni saluni ya kunyoa nywele iliyomsaidia kuamua.

"Inasikika kama kitu cha ujinga, lakini ukweli kwamba kulikuwa na saluni ya Waafrika na Wa -Caribbean niliyoiona mara moja nilipokuwa nikishuka kwenye kituo cha treni cha Brighton, kutembelea Chuo Kikuu cha Sussex. Ilinifanya nifikirie mara moja, ninaweza kuwa sawa hapa , Ninaweza kujihisi niko nyumbani,'" anasema Darren.

Nywele za Waafrika wa Caribbean ni tofauti na nywele za Wazungu wa Ulaya na inahitaji utaalamu fulani kuzikata vizuri.

Darren anakiri matokeo mazuri ya kazi yake, kwa kuwa na vinyozi ambao wamebobea kwa kazi hiyo.

**Makala hii ni kwa mujibu wa Mtandao.**

**BEI YA MAZAO >>** MCHELE 184375/- | ULEZI 142642.9/- **FEDHA >>** RAND 162.20 | KSH 22.82 | USH 0.61

UCHUMI

# Utalii wa Utamaduni ulivyosafisha ujangili Mikumi, ukakaribisha uchumi mpya vijijini

• Wahalifu zamani sasa wadau wa usalama • Wasimulia siri za ujangili wao zama hizo • Ajira za sasa katika utalii mpya hifadhini

**INATOKA UK.13**

### HATUA ILIYOCHUKULIWA

Katika jitihada za kumaliza changamoto hiyo Hifadhi ya Taifa Mikumi, iliaanzisha Utalii wa Utamaduni, kwa kuhusisha wananchi vijana jirani, ambao wanaanzishiwa ajira mbadala wa ujangili.

Mratibu wa Utalii wa Utamaduni katika Hifadhi ya Mikumi (Mikumi Eco and Cultural Tourism Enterprise), Makene Ngoroma, anasema kuanzishwa utalii huo ni kuwaondoa vijana jirani katika ujangioli na kuhamia utalii utamaduni.

Anasema, awali waliua wanyama na bidhaa zao kuuzwa katika mikoa ya Morogoro, Dar es Salaa, Pwani, Iringa na Dodoma.

Ngoroma anasema, kundi la vijana wastani 25 kutoka vitongoji vya Kwalaza, Magoma,Tambuka Reli na Mikumi katika Kata ya Mikumi, wengi waliojishughulisha na bodaboda, usiku walihamia katika ujangili.

Anasema, kutokana na kushamiri vitendo hivyo, kituo hicho cha Utalii wa Utamaduni kilianza kuhamasisha uanzishwaji utalii huo baada ya kuona kuna fursa nyingi halali zinawazunguka vijana.

"Tuliwafuata hawa vijana katika vitongoji vyote vya Mikumi hasa kwenye maeneo ya bodaboda na kuwaelimisha, kuhusu madhara ya ujangili na kuwaelezea fursa zilizopo katika utalii wa kitamaduni kwa kutumia Hifadhi ya Mikumi, wengi walituelewa sana na kukubali kuacha vitendo hivyo vya ujangili," anasema Ngoroma.

Mratibu huyo anataja sababu nyingine ni kuwawezesha wananchi jirani kufaidika na utalii utamaduni, ili waone faida ya wanyamapori hasa tembo wanaovamia mashamba yao.

Anataja mambo wanayoyahusisha na Utalii Utamaduni ni vivutio asili vya maporomoko ya maji, mila, desturi, njia za watumwa na maeneo ya kihistoria yanayopatikana Mikumi, ikiwamo kwenye matambiko ya makabila mbalimbali.

Mengine anayataja ni makabila yanayohifadhi asili zao akitoa mfano Wavidunda,Wasagara,Wakaguru na Parakuyo Masai, wanaopatikana Mikumi, huku chombo hicho cha usimamizi kikiwa karibu nao zaidi.

Ngoroma anataja baadhi ya maudhui ya mila hizo ni vyakula kama mihogo, ngoma za 'saga rhumba' na nguo za asili; kaniki.




Mandhari ya barabara iliyoko katika Hifadhi ya Taifa Mikumi na wanyama wanavyopatikana. **PICHA ZOTE: MAKTABA**.

> **"Tuliwafuata hawa vijana katika vitongoji vyote vya Mikumi, hasa kwenye maeneo ya bodaboda na kuwaelimisha kuhusu madhara ya ujangili na kuwaelezea fursa zilizopo katika utalii wa kitamaduni.**



Watalii wakifurahia Utalii wa Utamaduni kutoka jamii ya Kimasai.

Pia, watalii wanapelekwa kuuona mti wa mnazi ambao ndio chimbuko la jina la Mikumi, kutoka mti uliojulikana kiasili na kabila la Vidunda kama Mkochi, uliobadilishwa kutokana na utamkaji wa neno Mkochi na kuwa Mikumi.

Anasema katika eneo hilo, mtalii anapata fursa na sehemu za matambiko na miti wa kuogopwa maarufu kama Mkuyu, unaopatikana katika kitongoji cha Kotam, ambako kuna historia ya watu wa kale walikotambika, kutoa sadaka,kutahiri wanawake na kuwapa mafunzo.

Pia, ni eneo linaloaminika kwa uchawi na "uwanja wa kurusha ndege za kichawi (ungo)."

Shughuli nyingine zinazofurahishwa na watalii katika kivutio hicho, ni ufyatuaji matofali ya udongo, eneo la kuzikia maarufu kwa jina la Lukande na hoteli ya kwanza Mikumi, ambayo sasa ni Ofisi ya Mtendaji Kkata ya Mikumi.

Mratibu huyo anasema, katika eneo hilo mtalii anapata nafasi kutembelea kikundi cha ngoma kilichoanzishwa mwaka 1974 cha Kisamasi Vitua Ngoma kinachoongozwa na msanii wa zamani maarufu, Kabembele Kabembele, chenye uwezo wa kucheza ngoma za makabila tisa nchini.

Ngoroma anataja vivutio vingine, ni maporomoko ya maji Chizua, yanayopatikana katika Kijiji cha Udughu, Kata ya Vidunda.

Pia, kinamama wa Kimasai hawapo mbali, wanaohamasishwa kutengeneza urembo kama shanga, bangili, viatu, gauni, shuka, pia maziwa yanayozalishwa kwa ngombe zao, nyama ambazo mtalii akifika katika boma la Wamasai anazipata.

Ngorioma anasema, kipo kikundi cha kinamama cha kusuka ukili, mikeka na jamvi, ikiwa sehemu ya sanaa ya utamaduni.

Utalii wa Utamaduni, unashirikiana na Kikundi cha Hifadhi ya Mazingira kusafisha barabara kilomita 50 inayokatiza hifadhini Mikumi.

### UJANGILI ULIVYOPUNGUA

Ngoroma anasema, ujangili mkubwa uliofanywa dhidi ya wanyama waharibifu, hasa tembo, ambao wananchi waliwawekea sumu, pia kuwaua kwa mikuki, umepungua .

Anaeleza mafanikio kwamba, majangili wa zamani sasa wameobadilika, akitaja wawili wametubu kuacha na sasa ndio wataalamu wanawaongoza watalii wanaopenda kuzunguka kwa kutumia baiskeli.

Mratibu utamaduni huyo, anataja vijiji vya Mikumi vilivyokuwa juu katika matukio ya ujangili ni: Ihombwe, Kijiji cha Mhenda, Kijiji cha Kitundueta, pia vitongoji vya Kikwalaza, Tambuka Reli, na Magoma, huku wazazi walitekwa na hofu vijana wao kuangukia mikononi mwa dola kwa uhalifu wa ujangili.

### USHUHUDA

Mwongoza watalii wa utamaduni, Kelvin Damian, anasema vijana waliofanya ujangili walishindwa kukaa sehemu moja wakihofu kukamatwa, baada ya tembo watatu kuwekewa sumu katika maandazi na mwingine mmoja kuuawa, mwaka 2016.

Anatoboa siri, kuwa mwaka uliofuata 2017, ujangili ulikuwa mkubwa zaidi hasa dhidi ya tembo, mnyama waliomuamini ni mharibifu shambani, ingawa anasema katika sura ya pili ilichangiwa na kilimo kufanyika jirani na hifadhi.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mikumi, Jeremiah Mnyau, anakiri kuwa vijana wengi walijishughulisha na ujangili hivi sasa wameacha, wakihamia katika shughuli mbalimbali za kuwaingizia kipato, ikiwamo Utalii wa Utamaduni, kikundi cha usafi na shughuli za ujasirimali.

Kuhusu mchango wa Utalii wa Utamaduni, anasema wilaya inanufaika kuhifadhi mila na tamaduni za makabila makuu yanayopatikana wilayani Kilosa na vivutio vilivyoko katika Tarafa ya Mikumi, vimefaidika kwa kutambuliwa na kuendelezwa.

### WANUFAIKA

Seleman Omary, ni kijana aliyejishughulisha na ujangili na kuuza nyamapori, anasema ameacha ujangili na sasa na anawaongoza watalii wa kitamaduni, sambamba na kufanya kazi katika kikundi cha usafi wa mazingira.

Anataja manufaa aliyoyaopata hivi sasa amejenga nyumba yake na anasomesha watoto wake, baadhi wakiwa katika elimu ya sekondari na chuo cha ufundi.

Salome Saleh na Nasaliani Toroka kutoka kabila la kifugaji, nao kikia mmoja anakiri Utalii Utamaduni, umewanufaisha, kupitia bangili wanazouza.

### MKUU ULINZI MIKUMI

Mkuu wa Kitengo cha Ulinzi Katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Davis Mushi, anasema ujangili ulikuwa tatizo kubwa lililowasumbua sana hifadhini katika kipindi cha nyuma kutokana na vijana wengi kujiingiza huko, hata walilazimika kufanya doria kwa saa 24.

Anasema, hifadhi kwa kushirikiana na wadau wengine, wameimarisha ulinzi kwa kutumia vifaa vya kisasa na miradi ya ujirani mwema na vijiji. Mushi anatoa mfano wa takimwimu, kutokana na doria katika kipindi cha mwaka 2016/17 walifanikiwa kukamata bunduki mbili, zikiwemo aina ya Ak 47 na shotgun;risasi 43; mitego ya waya 560;misumeno 19; shoka 13; 'Chain Saw' tano; pikipiki mbili); gari moja; na baiskeli 10 .

Anasema, mwaka 2017/18 walikamata mifugo 20,080; nyaya 128; magobole 41; shotgun saba; pikipiki 15; gari moja; misumeno ya mikono 27; 'chain saw' mbili, ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia kupunguza matukio ya ujangili hifadhini.

Kuhusu Wanyama waliouawa na majangili, hadi kipindi cha mwaka 2017/18 matukio hayo ya ujangili ni kama yamekwisha, hivi kwani waliuawa kwa wanyama watatu tu aina ya swalapala.

### MHIFADHI MKUU

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Godwell Ole Meing'ataki, anasema wanatarajia kujenga milango katika baadhi ya vijij ili kuhamasisha Utalii Utamadunii.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, akizungumzia mikakati ya kukuza utalii, anasema serikali imepata mkopo wa bilioni 345 kutoka Benki ya Dunia, kwa ajili ya kukuza utalii.

## Biashara katika picha



Mhandisi kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), Kitengo maalum cha ushirikishwaji wanawake katika kazi za barabara, Salome Majala, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kibakwe, wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma, ili kuwahamasisha kusoma masomo ya Sayansi na Hisabati.



Mchuuzi wa miwa akisaka wateja katika eneo la Mazense Uzuri, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mstahiki Meya wa jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita (kushoto) akimkabidhi Mwalimu mkuu wa Shule ya Sekondari ya Kambangwa, Elesina Chanafi, kompyuta mpakato 6 Kati ya 20 zilizotolewa msaada na TBL kwa ajili ya shule za sekondari za Kambangwa , Minazi Mirefu na Kitunda ambapo Kila moja ilikabidhiwa msaada wa Kompyuta mpakato Sita (6) Katikati ni Meneja wa Masuala endelevu wa TBL Irene Mutiganzi na (kushoto) ni Mwenyekiti wa kamati ya maadili wa halmashauri ya jiji la Dar es Salaam,Songoro Mnyonge. **NA MPIGAPICHA WETU**

BEI YA MAZAO >> MAHINDI 52625/-| MAHARAGE 170000/-

UCHUMI

UTALII UTAMADUNI

# Chuo Utalii chabuni mradi uliobeba sura 3 za neema

• Wanachuo, wanakijiji katika kicheko



**Na James Lanka,** Moshi

WAKATI huenda kuna baadhi ya watu wanaona vitu vya asili vinavyowazunguka ni vya kawaida na haviwezi kuwa na tija yeyote katika uchumi wao wa kawaida, wataalamu wa masuala ya utalii wana mtazamo tofauti na hilo.

Katika hilo, wanasema mambo mengi na vitu vingi vya asili, ikijumuisha mila na desturi ni lulu kwa jamii, iwapo tu vitatumika katika kukuza utalii nchini.

Wadau wa utalii wakizungunza na Nipashe, wanasema vitu vya asili vikiwemo vyakula, vinywaji, mavazi, mila na desturi, vina thamani kubwa sana ikiwa vitatumiwa vyema katika sekta zinazohusiana na utalii, katika sura ya utalii wa utamaduni.

Mkufunzi wa Chuo cha Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyamapori Mweka (CAWM), Richard Kisasembe anafafanua kwamba, ikiwa vitu vya asili kama vyakula, vinywaji, mavazi na michezo mbalimbali kama ngoma za asili, vitatumiwa vyema katika sekta ya utalii, vitasaidia wanakijiji wengi kupata ajira itakayowaingizia kipato na fedha nyingi za kigeni.

"Mimi nimekuwa nikiwafundisha wanachuo wetu hapa Mweka masuala mbalimbali ya ujasiriamali, ikiwamo suala la kujiajiri kwa kuanzisha hizi 'Cultural Tourism Enterprise' (Utalii wa Kitamaduni) katika maeneo wanayotoka, kwani ni fursa nzuri sana ya kujiajiri na kutoa ajira kwa wananchi wengine wa sekta mbalimbali," anafafanua mkufunzi huyo.

> **"Mfano, viazi vikuu, magimbi, mbege na hata vyakula vya asili kama machalari, mtori, kiburu navyo vinapatikana kirahisi, katika mazingira yetu, hivyo ni rahisi kuwekeza.**



Watalii wakiangalia na kupata ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali ya kitamaduni, kupitia mradi wa Mweka Cultural Tourism. **PICHA ZOTE: JAMES LANKA.**

Kisasembe, ambaye pia ni Mratibu wa Utalii wa Kiutamaduni ambayo mwaka jana walipewa kibali na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), anafafanua kuwa inasaidia ajira kwa wanavijiji jirani katika kata ya Mweka, iliyoko tarafa ya Kibosho, wilaya Moshi Vijijini, Kilimanjaro.

Pia, ni mradi unaosaidia mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wake, huku akifafanua: "Kupitia mradi huu wa Mweka Cultural Tourism, wananchi wa vijiji mbalimbali vya Mweka wananufaika na kuuza vyakula vyao vya asili ya Wachaga wa Kibosho, kama Ng'ande, Kiburu, Machalari, viazi vya asili na pombe ya asili aina ya Mbege kwa Watalii mbalimbali na kujiingizia kipato."

Kisasembe, anafafanua kuwa, mradi huo pia unasaidia kwa kiasi kikubwa kutangaza vitu mbalimbali vya asili vinavyopatikana katika maeneo yao, zikiwemo handaki zilizotumika wakati wa vita, chemchem za asili, maporomoko ya maji na vivutio vingine kwa utalii endelevu.

Kwa mujibu wa mkufunzi huyo, mbali na kutoa ajira kwa mamia ya wananchi katika maeneo ya vijiji mbalimbali vya Mweka, pia mradi umekuwa sehemu muhimu ya kujifunzia kwa vitendo kwa wanafunzi wa Chuo cha Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori Mweka, ili wanapomaliza masomo yao waweze kujiajiri na kutoa fursa za ajira kwa wananchi wengine.

"Mradi huu wa Utalii wa Kitamaduni Mweka, kama ilivyo miradi mingi ya aina hii, uko chini ya malezi ya Bodi ya Utalii nchini Tanzania," anafafanua Kisasembe.

## ATAMKA MNUFAIKA

Mmoja wa wanufaikiaji wa utalii wa kitamaduni, Linus Laswai, ambaye pia ni Mratibu wa Mkuu Cultural Tourism, iliyopo wilayani Rombo mkoa Kilimanjaro, anafafanua kuwa yeye na wenzake wamekuwa kwenye sekta ya utalii kwa muda mrefu, lakini wana mafanikio kidogo kimaisha, tofauti ni kwa sasa wameweza kujikwamua kiuchumi, kutokana na mageuzi hayo.

"Kupitia mradi wetu wa Mkuu Cultural Tourism, tumefanikiwa kimaisha kwa kuuza vitu ama vyakula na vinywaji ambavyo tunawauzia watalii, vinapatikana katika mazingira yetu ya kila siku hapa Rombo.

"Mfano, viazi vikuu, magimbi, mbege na hata vyakula vya asili kama machalari, mtori, kiburu navyo vinapatikana kirahisi, katika mazingira yetu, hivyo ni rahisi kuwekeza," anafafanua Linus Laswai.

Aidha, Mzee John Chuwa, mkazi wa Kibosho anafafanua kwamba kupitia mradi wa Mweka Cultural Tourism, amekuwa akinufaika kwa kutengeneza na kuwauzia watalii kinywaji cha asili cha Wachaga aina ya mbege, kwa bei nzuri hasa wakati wa msimu wa watalii, ujulikanao kama 'high season.'

"Mimi mwenyewe ni mnufaikaji wa Mweka Cultural Tourism, kwani nimekuwa nikitengeza na kuwauzia watalii kinywaji aina ya mbege na kuwauzia kwa bei nzuri," anafafanua Mzee Chuwa.

**FEDHA >>** USD 2,300.95| Pauni 3,029.66| Euro 2,584.88

UCHUMI

UCHUMI MPYA DODOMA

# SIDO yakusanya wahitimu kwa mazito ya ujasiriamali

- Meneja asema ni matokeo ya tafakuri
- Wahusika wakiri 'taa mpya' kwa mkoa

**Na Renatha Msungu,** Dodoma

VIJANA wa jiji la Dodoma, wameangukiwa na neema baada ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (Sido), kuanzisha umoja wa wahitimu wa mafunzo ya ujasirimali, kwa ajili ya kuendeleza kile walichokisomea wakiwa mahali hapo.

Moja ya kazi ambazo vijana hao wamekuwa wakifundishwa kwa ajili ya kujiajiri, ni pamoja na kutengeneza viatu vya ngozi, mikanda na pochi za fedha za kiume maarufu kama waleti, ambazo zina wateja wengi wa nje na ndani ya nchi.

Meneja wa SIDO mkoani hapa, Sempeho Manongi, anasema ofisi yake iliamua kuanzisha umoja huo, kwa vijana wanahitimu wa masomo, ili watumie mashine zao binafsi kwa ajili ya kutengeneza bidhaa hizo, ambazo zinauzwa ndani na nje ya nchi.

Kutokana na hilo, imekuwa fursa kwa vijana hao ya kujiingizia kipato, pale watakapofikia hatua ya kwenda kuanzisha biashara zao, wakishapata mitaji kupitia umoja huo.

Manongi anasema, kitu hicho kilibuniwa na Sido, baada ya kubaini kuna vijana wengi wanahitimu mafunzo, lakini hawana uwezo wa kununua mashine za kufungua viwanda vidogo kwa ajili ya kutengeneza viatu, waleti (pochi za hela za kiume) na mikanda, bidhaa ambazo zina soko kubwa nchini.

Anasema, hilo ndilo liliwasukuma kuanzisha umoja wenye mtazamo wa kuwa na manufaa makubwa baadaye, kutokana na vijana wengi kuchomoka ndani ya umoja na kwenda kujitegemea katika biashara zao.

Meneja huyo anasema, bado kuna changamoto kwa wengine wakuwapo katika umoja huo, huku wakitakiwa kujitokeza kujiunga kwa ajili ya kupata msaada huo.

Kwa mujibu wa Manongi, wameamua kufanya hivyo ili kuwasaidia vijana wa mkoani hapa kupiga hatua na wanawachukua vijana wadogo na wakubwa, kupitia umoja ulioundwa hapo.

"Kwa kweli tumefanikisha kwa kiasi kikubwa, lakini bado inatubidi kuendelea kutafuta ambao hawana mahali pa kuendeleza vipaji vyao," anasema Manongi.

Meneja huyo anafafanua kuwa Dodoma kunahitajika kuwapo vijana wenye uwezo wa kujiendesha wenyewe kimaisha na kijasiriamali, kutokana na msingi wa mafunzo waliopewa.



Mkufunzi wa utengeneza bidhaa za ngozi, Shaban Lukandamila, akimuonyesha aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Rehema Nchimbi, bidhaa za ngozi zilizotengenezwa na vijana wajasiriamali wa Manispaa ya Dodoma, baada ya kupatiwa mafunzo na Sido, Dodoma. **PICHA: MTANDAO.**

> **"Kwa kweli tumefanikisha kwa kiasi kikubwa, lakini bado inatubidi kuendelea kutafuta ambao hawana mahali pa kuendeleza vipaji vyao.**

Manongi anasema, mtazamo mkuu ni kuwainua vijana wa Dodoma kibiashara kuwezesha kuanzishwa viwanda vidogo.

Anakiri kuwapo mwitikio mzuri wa vijana ndani ya jiji wanaojiunga kozi za ufundi za SIDO, ambazo zina faida kubwa kwao, pia inawasaidia kujipatia kipato na kuendesha familia zinazowazunguka katika maeneo wanayoishi.

Anakosoa mtindo wa vijana wengi wa Dodoma kuendekeza tabia ya kukaa vijiweni, akiwataka wabadilike kwa kufanya kazi, ili kuhakikisha wanashiriki mafunzo yanayotolewa na SIDO kila wakati.

**WANUFAIKA WANENA**

Mshiriki wa mafunzo hayo anayejitambulisha kwa jina la Rosemary, anasema ameanza mafunzo hayo akiwa kijana mdogo zaidi na kupitia mafunzo ya Sido, hadi sasa anamiliki biashara inayomuingizia kipato kikubwa.

Anasema, kwa sasa anafanya biashara ndani ya nchi za Afrika Mashariki na anaamini atapiga hatua kuzifikia nchi nyingi za Afrika. Rosemary anafafanua: "Najivunia Sido Dodoma kwa sababu imenikuza kibiashara."

Pia, mwanamke huyo anawahimiza vijana wenzake wa Dodoma, wasibweteke na badala yake wajitokeze kupata mafunzo ya Sido.

Juma Bakary, ni mnufaika anayesema Sido Dodoma, imesaidia sana kutokaa vijiweni, kutokana na kwamba ina fursa nyingi ambazo wanaweza kuzipata.

Anasema kwa sasa, ana malengo ya kuwa mfanyabiashara mkubwa baadaye, kutokana na ujuzi aliyoupata kutoka mafunzo ya Sido.

Mkazi mwingine wa mjini hapa, Ibrahim Aman, anasema shirika hilo, limewasaidia sana vijana wa Dodoma, kwani kutokana kwa sasa wengi wamejiajiri kupitia ujuzi huo.

Ibrahim anasema, awali walikuwa wakitegemea kuuza viatu vya Kimasai kutoka Arusha, lakini sasa vinatengenezwa mkoani Dodoma, kutokana na elimu na fursa hiyo ya Sido. Anasema, zaidi ya kuwa bidhaa zinazotengenezwa kuwa bora, pia zinauzwa katika nchi jirani.

Anawashauri vijana kuchangamkia fursa za kuhudhuria kozi hizo, badala ya kupoteza muda vijiweni kama ilivyo ada ya vijana wa mjini, muda mrefu wakijadili anachokitaja kuwa: "mambo ya mpira badala ya kwenda katika mafunzo."

"Naomba vijana mtumie fursa hiyo adimu kwa sababu haiji Mara mbili ",anasema Aman.


# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Aprili 1, 2019

| Mkoa | Arusha | D'Salaam | Dodoma | Geita | Morogoro | Kagera | Kilimanjaro | Kigoma | Lindi | Manyara |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 57000 | 70000 | 53000 | 57000 | 48000 | 60000 | 40000 | 45000 | 80000 | 60000 |
| Mchele | 200000 | 210000 | 195000 | 130000 | 165000 | 185000 | 180000 | 160000 | 200000 | 200000 |
| Mtama | 40000 | 60000 | 35000 | 180000 | 71000 | 100000 | 80000 | 100000 | 150000 | 42000 |
| Uwele | 40000 | 60000 | 34000 | 180000 | 71000 | 110000 | NA | 100000 | NA | 100000 |
| Ulezi | 72000 | 140000 | 75000 | NA | 155000 | 150000 | 180000 | 150000 | 200000 | 120000 |
| Ngano | 87000 | 130000 | 160000 | 180000 | 163000 | NA | 98000 | 150000 | NA | 120000 |
| Maharage | 150000 | 220000 | 170000 | 170000 | 185000 | 150000 | 180000 | 140000 | 200000 | 130000 |
| Viazi Mviringo | 70000 | 80000 | 66000 | 70000 | 82000 | 75000 | 50000 | 90000 | 100000 | 60000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia Machi 6, 2019

| MKOA | DSM | Arusha | Pwani | Dodoma | Geita | Iringa | Kagera (Bukoba) | Katavi | Kigoma | Moshi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petroli | 2,098 | 2,191 | 2,102 | 2,157 | 2,263 | 2,162 | 2,313 | 2,306 | 2,329 | 2,181 |
| Dizeli | 2,131 | 2,195 | 2,135 | 2,189 | 2,296 | 2,195 | 2,346 | 2,339 | 2,362 | 2,185 |
| M'Taa | 2,096 | 2,286 | 2,101 | 2,155 | 2,262 | 2,161 | 2,312 | 2,304 | 2,328 | 2,276 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Aprili 3, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,483.00 | +0.00 |
| DSEI | 2,061.30 | -1.49 |

| | |
|---|---|
| Thamani za Hisa (bln) | 19,868.45 |
| Mauzo | 2,318,750.00 |
| Hisa | 14,066 |

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| JHL | 9,250 | -0.54% |
| NMG | 1,380 | -2.82% |
| EABL | 4,740 | -0.42% |
| KA | 110 | -4.35% |
| ACA | 5,950 | +1.71% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,591.28 | 2,617.65 |
| USD | 2,268.07 | 2,290.76 |
| KES | 22.38 | 22.56 |
| GBP | 2,947.82 | 2,977.52 |

## Bei za hisa hadi kikao cha Aprili 3, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| ACA | 5,950.00 | 5,850.00 | 1.71 |
| CRDB | 125 | 125.00 | 0 |
| DCB | 340 | 340 | 0 |
| DSE | 1,300 | 1,300 | 0 |
| EABL | 4,740.00 | 4,760.00 | -0.42 |
| JHL | 9,250.00 | 9,300.00 | -0.54 |
| KA | 110.00 | 115.00 | -4.35 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| MBP | 490.00 | 490.00 | 0 |
| MCB | 500.00 | 500.00 | 0 |
| MKCB | 800.00 | 800.00 | 0 |
| MUCOB | 400.00 | 400.00 | 0 |
| NICO | 170.00 | 170.00 | 0 |
| NMB | 2,340.00 | 2,340.00 | 0 |
| NMG | 1,380.00 | 1,420.00 | -2.82 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| PAL | 400.00 | 400.00 | 0 |
| SWALA | 490.00 | 490.00 | 0 |
| SWIS | 1,700.00 | 1,700.00 | 0 |
| TBL | 11,400.00 | 11,400.00 | 0 |
| TCC | 17,000 | 17,000.00 | 0 |
| TCCL | 600.00 | 600.00 | 0 |
| TICL | 385 | 385.00 | 0 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 2,263.46 | 2,281.56 |
| UGANDA SHS | 57.66 | 61.75 |
| RWANDAN FRANC | 251.97 | 254.93 |
| BURUNDI FRANC | 218.12 | 219.77 |
| USD | 227,816.83 | 230,095.00 |
| POUND STG | 299,943.64 | 302,966.09 |
| EURO | 255,861.08 | 258,488.72 |
| CANADIAN $ | 171,007.98 | 172,666.22 |
| SWITZ. FRANC | 228,685.84 | 230,879.99 |
| JAPANESE YEN | 2,044.12 | 2,064.19 |
| SWEDISH KRONOR | 24,549.76 | 24,787.24 |
| NORWEG. KRONOR | 26,609.14 | 26,865.82 |
| DANISH KRONOR | 34,287.04 | 34,624.70 |
| AUSTRALIAN $ | 162,068.89 | 163,735.60 |
| INDIAN RPS | 3,329.68 | 3,362.49 |
| PAKISTAN RPS | 1,531.68 | 1,620.39 |
| ZAMBIAN KWACHA | 18,670.42 | 18,969.08 |
| MALAWIAN KWACHA | 290.39 | 311.04 |
| MOZAMBIQUE-MET | 3,537.53 | 3,567.36 |
| ZIMBABWE $ | 42.63 | 43.49 |
| SDR | 315,751.85 | 318,909.37 |
| GOLD (T/O) | 294,079,635.35 | 297,197,604.85 |
| S. AFRICAN RAND | 16,067.09 | 16,220.55 |
| UAE DIRHAM | 62,028.11 | 62,636.45 |
| SINGAPORE $ | 168,366.59 | 169,987.44 |
| HONK KONG $ | 29,025.32 | 29,314.45 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 60,746.30 | 61,352.12 |
| KUWAIT DINAR | 748,535.67 | 755,747.88 |
| BOTSWANA PULA | 21,300.87 | 21,697.96 |
| CHINESE YUAN | 33,957.91 | 34,291.87 |
| MALAYSIA RINGGIT | 55,878.55 | 56,382.01 |
| SOUTH KOREA WON | 201.05 | 202.7 |
| NEWZEALAND | 154,619.28 | 156,257.51 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **3/Apr/2019** | **1.60** | **2,313.00** | **2,298.60** | **2,300.95** |
| **2/Apr/2019** | **1.80** | **2,315.00** | **2,298.60** | **2,300.91** |
| **1/Apr/2019** | **1.30** | **2,311.00** | **2,298.50** | **2,300.95** |
| **29/Mar/2019** | **2.00** | **2,313.00** | **2,298.50** | **2,300.87** |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **3/Apr/2019** | **37,500** | **6.00** | **4.75** | **5.20** |
| 2/Apr/2019 | 42,750 | 6.00 | 4.75 | 5.48 |
| 1/Apr/2019 | 66,250 | 6.00 | 4.50 | 5.33 |
| 29/Mar/2019 | 32,100 | 6.50 | 5.00 | 5.19 |
| 28/Mar/2019 | 55,000 | 6.00 | 5.00 | 5.15 |
| 27/Mar/2019 | 57,000 | 5.50 | 5.00 | 5.07 |

# Mfuko wa Ubunifu ulivyoanika mahali kona ya maendeleo iliko



Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe.

"Kazi za ubunifu zitumike kutatua changamoto zilizopo kila siku.Watu wasibuni kujifurahisha, wabuni kutokana na changamoto zilizopo nchini ili kupata soko la kazi zao. Wakifanya hivyo serikali itakuwa tayari kuwasaidia wabunifu wenye ubunifu unaoondoa changamoto zilizopo," anasisitiza.

**DC HANDENI**

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe, anashauri wawekezaji wasiangalie eneo la mjini pekee, pia wafike vijijini, kwa kuwa zipo changamoto nyingi zinazohitaji ufumbuzi kupitia ubunifu.

"Ubunifu wowote unajumuisha tekonolojia yenye mfumo wa nje na wa ndani. Changamoto iliyopo ni kama tunaposhughulikia mifumo hiyo kwa kuangalia mazingira ya Watanzania na nani mwenye jicho halisi la kuangalia changamoto za Watanzania wa kawaida,"anasema.

Gondwe anaongeza: "Kwa sasa tuna mifumo mingi ya ndani (software), bado wabunifu wanaangalia mjini pekee, lakini tukiamua wabunifu waje vijijini waone changamoto ambazo kwao ni fursa ya kubuni njia bora ya kutatua matatizo yaliyopo kwenye eneo husika."

Anasema zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wako vijijini na wanapaswa kuunganishwa kwenye ubunifu unaotatua matatizo yao ya kila siku kwa mazingira yao.

"Unapozungumzia vijijini, unazungumzia kilimo, madini. Mkulima anataka kupata taarifa za masoko ya ndani na nje, ikiwamo kuwasiliana vizuri na mteja, anataka kupata tekonolojia ya bei rahisi ya kutumia umeme kuchakata muhogo, mahindi au mazao mengine," anasema.

Anarejea aliko Handeni, kuna mazao ya kimkakati kama mihogo na alizeti na kwa mwaka huu yamezalishwa kwa wingi, lakini hakuna teknolojia rahisi ya kutumiwa na mkulima kukausha na kuuza kwenye masoko ya nje.

"Soko la Kimataifa kwa China wanahitaji mhogo uliokaushwa chini ya asilimia 10 na baada ya hapo Mtanzania ataweza kuuza nje.

"Soko liko wazi kabisa na kwa sasa Afrika nchi zilizoingia mkataba huo ni Ghana, Madagascar, Tanzania na Nigeria," anasema.

"Kupata ubunifu wa kutengeneza mashine katika eneo hilo bado ni tabu. Tunawaomba wabunifu waliopo mjini waje vijijini. Leo Tanzania inaagiza mafuta ya kupikia nje kwa asilimia 50, lakini kilimo kiko vijijini ambako hakuna mashine ndogo ndogo na rahisi za kutumia jua."

Anasema, wabunifu wanatakiwa kwenda vijijini kuangalia changamoto hizo na namna bora na rahisi ya kuwasaidia kutatua changamoto zilizopo vijijini ili kutatua na kusukuma maendeleo.

"Lengo la ubunifu ni kuzalisha huduma bora ambayo itathaminiwa ndani na nje ya nchi, utazalisha mchakato bora ambao utaweza kumsaidia Mtanzania kutoka saa 2 hadi sekunde kuzalisha huduma bora," anasema Gondwe.



# RC Chalamila awapiga mkwara watendaji wake

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewawashia moto wakurugenzi na waganga wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kuhusu usajili wa wanachama wa mfuko wa jamii iliyoboreshwa (ICHF), ambapo amewataka wahakikishe wanatekeleza maagizo yote yaliyotolewa.

Chalamila aliwasha moto huo jana asubuhi alipokuwa anazindua usajili wa wanachama wa ICHF, huku akibaini kuwa baadhi ya viongozi hao hawajatekeleza maagizo maalumu waliyopewa ikiwamo ununuzi wa simu kwa ajili ya vituo vitakavyotumika kuandikisha. Vilevile alisema baadhi ya halmashauri bado hazijawasilisha mchango walioagizwa kwa ajili ya kuwezesha zoezi hilo kukamilika ambapo aliwataka watendaji hao wajieleze. Alisema kati ya halmashauri zote saba za mkoa huo, tatu pekee ndiyo ambazo zimeshawasilisha michango hiyo na kukamilisha ununuzi wa simu na hivyo akawataka viongozi hao kila mmoja atoe ahadi muda watakaokuwa wamemaliza vitu hivyo.

Baada ya maelezo hayo, wakurugenzi wote wa halmashauri walitoa ahadi zao na ndipo Chalamila akawaagiza wakuu wa wilaya hizo kuwaandikia barua wakurugenzi kuwasisitiza kuhusu ahadi hizo.

"Nataka muwaandikie barua za kusisitiza kile walichoahidi wakurugenzi na nakala mniletee mimi, nikishapokea barua hizo nitawajibu na nakala za barua hizo nitazipeleka kwa Waziri wa Tamisemi pamoja na Katibu Mkuu ili ambaye hatatekeleza achukuliwe hatua," alisema Chalamila.

Aidha, aliwaagiza wakurugenzi na wenyeviti wa halmashauri zote kuhakikisha ajenda ya bima ya afya inakuwa ya kudumu kwenye vikao vyao na kuhakikisha wananchi wanaelewa kuhusu masuala hayo na kujiunga na bima hiyo.

Awali akiwasilisha taarifa ya ICHF Mkoa wa Mbeya, Selina Mtenya, alisema katika utekelezaji wa zoezi hilo tayari baadhi ya kazi zimeshafanyika na kwamba hatua zingine zinaendelea kwa hatua mbalimbali. Alisema baadhi ya hatua ambazo zimetekelezwa ni pamoja na Katibu Tawala wa Mkoa kumteua mratibu wa mfuko huo ngazi ya mkoa pamoja na wakurugenzi watendaji wa halmashauri kuteua waratibu wa CHF na maofisa Tehama.

Alisema tayari watoa huduma 230 na wajumbe wa kamati za afya 229 wameshapatiwa mafunzo ya uandikishaji wa wanachama na kwamba mafunzo hayo yaliwezeshwa na Tamisemi.

Vilevile alisema maofisa waandikishaji wa vijiji na mitaa 768 wameshapatiwa mafunzo pamoja na wasimamizi 16 wa tarafa na kwamba tayari taarifa muhimu zinazohusu mfuko huo zimeshaingizwa kwenye mfumo.

"Changamoto zinazotukabili kwenye utekelezaji wa zoezi hili ni pamoja na baadhi ya vituo kuchelewa kununua simu ambapo mpaka sasa vituo 79 kati ya 236 bado havijanunua simu, lakini pia baadhi ya halmashauri bado hazijatoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa," alisema Mtenya.

Alisisitiza kuwa endapo kila kinachohitajika kwenye halmashauri na vituo kitapatikana kwa wakati, Mkoa wa Mbeya utafanya vizuri katika zoezi hilo na kwamba huenda ukawa mkoa wa mfano.



Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya, James Kasusura (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya (wa kwanza kulia) wakipokea vitendea kazi kwa ajili ya usajili wa wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ulioboreshwa (ICHF) kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila wakati wa uzinduzi wa zoezi hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Tanzania yazinduka kuwekeza katika kilimo

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

TANZANIA imeanza kuwekeza katika elimu, ujuzi na mbinu za kuzalisha mazao mengi ya chakula kwa wakulima wadogo nchini ili kuongeza tija ya uzalishaji kwa lengo la kujiwekea usalama wa chakula.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo (Tari) cha Uyole mkoani Mbeya, Dk. Tuloler Bucheyeki, aliyasema hayo jana kwenye maadhimisho ya siku ya wakulima katika Kijiji cha Iwalanje, Kata ya Magamba wilayani Mbozi.

Alisema kutokana na lengo la serikali la kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda, pia imeona haja ya kuwekeza kwenye elimu na teknolojia za kisasa kwenye kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa kutumia ujuzi na mbinu za kisasa.

"Tumeamua kuwekeza elimu na ujuzi kwa wakulima wadogo ili kuongeza uzalishaji hasa wa mazao kwa lengo la kuweka usalama wa chakula kwa taifa letu, tunatambua kuwa serikali ina sera ya taifa ya kuelekea kwenye uchumi wa viwanda, hii itasababisha vijana wengi kwenda kufanya kazi viwandani hivyo wale wachache watakaobaki kwenye kilimo ni lazima wawe na elimu na ujuzi ili wazalishe chakula cha kukidhi mahitaji ya taifa," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema kuwa pamoja na kuweka usalama wa chakula, pia mazao hayo yatatumika kama malighafi za viwanda vinavyoendelea kujengwa nchini ili kuyaongeza thamani na kuyauza kwa bei nzuri.

Dk. Bucheyeki alisema kuwa mahitaji ya mazao viwandani pamoja na mahitaji ya chakula cha wananchi, ni dhahiri kuwa uzalishaji wa mazao hasa ya chakula na biashara unatakiwa kuongezeka mara dufu na bila uwepo wa elimu, ujuzi na teknolojia za kisasa kwa wakulima inawezekana, wakulima wakashindwa kukidhi mahitaji.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo, Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia uchumi na uzalishaji Mkoa wa Songwe, Vanciar Kulanga, alisema serikali inasisitiza kilimo cha kibiashara ili kuwakwamua wakulima kiuchumi.

Alisema kuwa kilimo cha kibiashara ndicho kitakachowasaidia wakulima kujikwamua na umasikini kwa vile watayatumia mazao wanayolima kwa chakula na ziada wataiuza kwa watu wengine wenye uhitaji wa chakula na viwandani kwa ajili ya kuongezwa thamani, huku wao wakulima wakijipatia fedha kwa ajili ya mahitaji yao mengine.

Kulanga aliwataka wakulima wilayani Mbozi kuweka kumbukumbu za taarifa za uzalishaji wa mazao ili iwe rahisi kwa serikali kuwatafutia soko la mazao.

"Lipo tatizo la kutokuwapo kwa taarifa za kiasi cha mazao yaliyozalishwa mkoani Songwe, hii inasababisha serikali kutokuwa na takwimu sahihi za mazao ya ziada yaliyopo kwa wakulima na hivyo kushindwa kuwatafutia soko la mazao yenu," alisema Kulanga.

Diwani wa Kata ya Magamba, Wilson Mwashilindi, aliwataka wakulima kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa kilimo ili waweze kuzalisha mazao kwa tija.

Alisema kitendo cha wakulima kulima mashamba makubwa na kupata mazao kidogo kimepitwa na wakati na badala yake wanatakiwa kulima eneo dogo ambalo litawapatia mazao mengi.

"Mkulima unalima ekari tatu unapata magunia matatu ya mahindi, wewe utakuwa sio mkulima ni afadhali uache kulima na shamba lako umkodishie mtu mwingine alime kisha mgawane mazao yatakayopatikana, maana yeye atalima hizo ekari tatu atapata magunia 60 ambayo mkigawana utapata magunia 30 ambayo yatakusaidia kuliko kuendelea kulima wewe mwenyewe na kupata magunia matatu," alisema Mwashilindi.

Mtafiti wa Kilimo kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo Uyole cha mkoani Mbeya, Mlowe Fredrick, alisisitiza wakulima kuzingatia matumizi sahihi ya mbolea ili waweze kuongeza tija katika uzalishaji.

# Dereva bodaboda auawa kinyama

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wasiojulikana wanadaiwa kumuua kijana mmoja ajulikanaye kwa jina la Aidan Chongola (27), mkazi wa mtaa wa Hayanga jijini Mbeya ambaye alikuwa dereva wa bodaboda kisha wakatokomea kusikojulikana na pikipiki yake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 2:00 usiku katika eneo la Ituha Relini.

Alisema watu hao ambao wanadaiwa walikuwa wawili walimkuta kijana huyo akiwa na pikipiki yenye namba za usajili MC 557 BBT aina ya Kinglion yenye rangi nyeusi katika kituo chake cha kazi cha Ilomba na wakamkodi ili awapeleke Ituha.


Alisema kijana huyo alikubali kuwabeba na walipofika eneo la Ituha Relini, walimgeuka na kumchoma na kitu chenye ncha kali sehemu ya tumbo na kisha wakamtelekeza na kuondoka na pikipiki.

"Mwili wa kijana huyo uliokotwa ukiwa umetelekezwa kando ya reli ya Tazara na ulichukuliwa na kuhifadhiwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, tunaendelea kuwasaka wahusika hao na endapo watakamatwa watachukuliwa hatua kali za kisheria," alisema Kamanda Matei.

Kamanda Matei aliwataka madereva bodaboda kuwa makini wanapowachukua abira wasiowafahamu hasa nyakati za usiku kwa kuwa ni hatari kwa maisha yao.

Vilevile aliwatahadharisha wahalifu wanaoingia katika mkoa huo kwa ajili ya kufanya uhalifu, kuwa jeshi hilo liko makini na litawashughulikia wote watakaopatikana wakitekeleza matukio yoyote ya uhalifu.

Hata hivyo aliwataka wananchi wa mkoa huo kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za uhalifu ili kuhakikisha wahalifu wote wanakamatwa na kudhibitiwa ili mkoa uendelee kuwa salama.





# ALAT yajitosa mashindano ya tuzo za serikali za mitaa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUMUIYA ya Tawala za Mitaa nchini (ALAT) kwa kushirikiana na Umoja wa Majiji na Serikali za Mitaa Afrika (UCLG Africa), wameanza kutekeleza mradi wa tuzo za viongozi wa serikali za mitaa (Mayors Award Scheme-MAS), kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa Mwenyekiti wa ALAT, Gullamhafeez Mukadam, alisema mradi huo wa MAS 2018/19 ulizinduliwa rasmi katika mkutano mkuu wa 34 uliofanyika Dodoma mwaka jana na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Alisema lengo la mradi huo ni kuwatambua viongozi hao wa halmashauri na kutoa tuzo kwa mamlaka za serikali za mitaa.

Alisema utaratibu wa kushiriki katika utoaji wa tuzo hizo umebainishwa katika miongozo ya mradi na vigezo vyake vimebainishwa.

Alivitaja vigezo vya kushindaniwa kuwa ni maendeleo ya uchumi, hali ya utoaji wa huduma, ujumuishaji wa makundi maalum katika mpango wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, usimamizi wa rasilimali fedha pamoja na utawala bora. "Halmashauri zote 185 zitashiriki katika kuwania tuzo kwa kujaza fomu za maombi na kuziwasilisha ALAT, kwa ajili ya uchambuzi ili kumpata mshindi, pamoja na fomu za maombi wananchi watapata fursa ya kuzipigia kura halmashauri kupitia ujumbe wa simu ya mkononi pamoja na tovuti maalum," alisema Mukadam.

Aidha, alisema kuwa pia utaratibu huo utatumiwa na halmashauri kuwatambua wadau mbalimbali, asasi za kiraia pamoja na vyombo vya habari ambavyo vinastahili kupata tuzo hiyo.

Alifafanua kuwa utaratibu wa kuwapata washindi utafanywa na jopo la majaji huru walioteuliwa kutoka katika uwakilishi wa taasisi za taaluma, asasi za kiraia, sekta binafsi na tasnia ya habari.

Mratibu wa mradi huo wa tuzo za viongozi wa serikali za mitaa (MAS) Wilman Ndile, alisema hii ni awamu ya ya tatu toka kuanza kutolewa kwa tuzo hizo.

Ndile alisema awali utoaji wa tuzo hizo ulikuwa ukihusisha baadhi ya halmashauri nchini tofauti na mwaka huu ambapo halmashauri zote 185 zitashiriki katika kinyang'anyiro hicho.



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile (kushoto), akijadiliana jambo na Makamu wa Rais wa Mfuko wa Abbott Tanzania, Andy Wilson (katikati), pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa mfuko huo, Natalia LoBue, walipofika ofisini kwake jijini Dodoma jana, kumpa taarifa ya mradi wa ujenzi wa makao mapya ya taifa ya watoto yanayotarajiwa kujengwa jijini humo hivi karibuni. **PICHA: WIZARA YA AFYA**

## Watupwa jela miaka 23 kwa nyara za serikali

**Na Renatha Msungu,** SINGIDA

WASHTAKIWA sita wa kosa la uhujumu uchumi wamehukumiwa kwenda jela miaka 23 kila mmoja baada ya kukutwa na meno ya tembo nane.

Watuhumiwa hao walikamatwa katika kijiji cha Naguro, kilichopo wilayani Chamwino mkoani Dodoma.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu wa Wilaya ya Manyosni mkoani Singida, Stella Kiama.

Waliotiwa hatiani ni pamoja na Aloyce Magawa, Jonas Julias, Anton Magoma, Andason Wami, Matayo Rorgan na George Joseph.

Akitoa hukumu hiyo, hakimu Kiama alisema adhabu hiyo ni fundisho kwa jamii ili kuacha kuiba nyara za serikali.

Alisema lengo ni kukomesha wizi wa nyara hizo ambazo ni mali ya serikali.

Kosa la kwanza kwa washtakiwa wote miaka 20 kila mmoja, huku kosa la pili kwa mshtakiwa wa 5 peke yake miaka 20, wakati kosa la tatu kwa washtakiwa wote faini au miaka 3 kila mmoja.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza 2016 na hatimaye hukumu yake ilitolewa juzi baada ya kupatikana na hatia.

# Maonyesho ya ujenzi kufanyika Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAONYESHO ya wadau wa sekta ya ujenzi yajulikanayo kama Dodoma Builders Expo kwa ajili ya kuhamasisha viwanda, yamepangwa kufanyika Juni 7 hadi 8 jijini mwaka huu.

Katika maonyesho hayo, kampuni 100 zinatarajia kushiriki pamoja na watazamaji 12,000 wakitarajia kuhudhuria.

Akizungumza jana jijini hapa Mkurugenzi wa Dodoma Builders Expo, Atatenda Nyawo, alisema hayo ni maonyesho ya pili kufanyika, ambapo yanatarajia kushirikisha wadau mbalimbali.

Tatenda alisema jumla ya wadau 100 watashiriki maonyesho hayo huku akiwataka watu kujitokeza katika maonyesho hayo.

Alisema onyesho hilo litasaidia kuonyesha mtazamo chanya kwa Watanzania hasa katika kuimarisha viwanda vya ndani na bidhaa zake kwa ujumla.

Alifafanua kuwa maonyesho hayo yataleta faida kubwa kwa Watanzania kwa sababu vijana wengi watafanikiwa kupata ajira. Alisema inafahamika Dodoma ni makao makuu, kwa hiyo wanaungana na serikali kuijenga.


Naye mratibu wa maonyesho hayo, Albert Makoye, alisema yatawasaidia wadau wa ujenzi kuzitangaza bidhaa zao kwa jamii.

Alisema mwaka huu kutakuwa na maboresho makubwa na washiriki wengi wanatarajia kushiriki katika maonyesho hayo.

Aliwataka wakazi wa Dodoma na mikoa mingine wajitokeze kushiriki katika maonyesho hayo ambayo hufanyika kila mwaka.

Aliongeza kuwa sekta ya ujenzi ni muhimu ndiyo maana wameamua kuwaandalia maonyesho ili kujitangaza.

Haya ni maonyesho ya pili ambapo mwaka jana yalifanyika mkoani Dodoma na kushirikisha watu 6,000.








Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Ziwa, Abraham Augustino (kulia), akimkabidhi Naibu Waziri wa Tamisemi, Mwita Waitara (kushoto), msaada wa vifaa vya ujenzi ikiwamo mabati 130 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Msingi Iramba iliyopo Tarime mkoani Mara. Wa kwanza kulia ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Apoo Castro Tindwa na Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Francis Kabeho. **PICHA: NMB**

# Walimu waicharukia serikali kuchelewesha ruzuku shuleni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UMOJA wa Walimu Wakuu Zanzibar, umeiomba wizara kutoa ruzuku kwa wakati kwa shule za sekondari ili kuweza kutekeleza majukumu yao na kuepuka kuwachangisha wanafunzi.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa umoja huo, Fadhil Mshamba, wakati alipozungumza kuhusu suala la michango kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

Mshamba alisema kitendo cha wizara kuchelewesha kutoa ruzuku kwa shule za sekondari kwa kiasi kikubwa kimesababisha wanafunzi kutoleta michango.

"Wakati mwingine walimu hulazimika kuwachangisha wanafunzi fedha kwa ajili ya kutayarisha mitihani ya majiribio na si vyenginevyo," alisema.

Alisema yapo mahitaji mengi yanayohitajika katika shule ambapo fedha za ruzuku zingetumika kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi mahitaji hayo.

Alizitaja fedha zinazohitajika katika kuendesha shughuli za harakati za shule ikiwamo utayarishaji na uchapisha mitihani ya majaribio, pamoja na madawati.

"Zipo fedha nyingi zinahitajika kwa ajili ya shughuli za kila siku za maendeleo ya shule ambazo hazipatikani kwa wakati," alisema.

# Waziri asifu benki kuwainua wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imesifu mchango mkubwa unaotolewa na taasisi za kifedha nchini katika kuwainua wafanyabiashara wadogo ili waweze kukuza mapato yao na kuchangia uchumi wa nchi.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mohammed Ahmada Salum, amesema serikali zote mbili, ya Zanzibar na Bara zinaamini kuwa mchango wa benki mbalimbali ni muhimu kwa ustawi wa wajasiriamali na taifa kwa jumla.

Akifungua mkutano wa mafunzo kwa wanachama wa klabu ya biashara ya benki ya NMB Zanzibar (NMB Business Club) visiwani Zanzibar, alisema mafanikio ya wafanyabiashara kwa maisha yao, pia yanaongeza mapato ya serikali kupitia kodi wanazolipa.

Alieleza kuwa, hatua ya NMB kuwaandalia mafunzo wajasiriamali wa klabu hiyo wapatao 300 kuhusu kodi na jinsi ya kutunza fedha, ni muhimu kwa kuwa inawajengea wananchi uwezo ili wawe na mazoea ya kulipa kodi badala ya kukwepa.

Aidha, alisema kuwapatia mafunzo, kunawajengea uwezo na kuona umuhimu wa kuimarisha uhusiano na wadau na taasisi mbalimbali zinazotoa huduma, kutakuza uelewa wa kufanya biashara zao kitaalamu zaidi. Alisema kuwaunganisha wateja ambao ni wajasiriamali ili wawe na muundo mzuri wa upashanaji habari utakaounganisha wanachama wa klabu na NMB, ni jambo la msingi kwa kuwa katika ulimwengu wa sasa mtu hawezi kupata ufanisi kwa kujitenga na kufanya mambo peke yake.

"Katika hili hata pale mteja anapokosa nafasi ya kwenda benki kuelimishwa jambo linalohusu biashara au mabadiliko, ataweza kupata elimu hiyo kupitia wanachama wenzake na hivyo kukuza uelewa wa biashara na masuala ya benki," alibainisha.

Aidha, Naibu Waziri huyo alisema mkutano huo ni fursa kubwa kwa wajasiriamali hao kupata elimu bila ya malipo, ambayo pahala pengine wangelazimika kuilipia kwa gharama kubwa. Ahmada alieleza matumaini yake kuwa elimu watakayopata wajasiriamali hao itakuwa na manufaa makubwa kwa kuwa itawafundisha namna bora ya kutunza kumbukumbu za biashara, masoko, huduma nzuri kwa mteja, upangaji bei, sheria za biashara na mahesabu na maeneo mengine yanayofaa ikiwamo elimu ya kodi.

Alitumia fursa hiyo kuushukuru uongozi na wafanyakazi wa NMB kwa kubuni utaratibu huo, ambao alisema utawanufaisha sio tu wafanyabiashara wa Zanzibar, bali pia wa sehemu nyingine, na hivyo matokeo yake ni kuleta maendeleo ya kiuchumi nchini.

Aliihakikishia NMB pamoja na wafanyabiashara hao, kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea kushirikiana nao ili kuhakikisha wanaimarisha mazingira ya kazi zao ili hatimaye wapande ngazi na kuwa wamiliki wa biashara kubwa.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara katika benki ya NMB, Donatus Richard, alisema 'Business Club' ni mkusanyiko unaofanyika kwa lengo la kuwakutanisha wafanyabiashara wadogo na wa kati ili kuwapatia maarifa ya kujiendesha kitaalamu.

Aidha, alisema lengo lingine ni kuwawezesha kubadilishana mawazo juu ya njia tofauti za kuimarisha biashara zao, pamoja na kuishauri benki hiyo kuhusu namna bora zaidi katika kuwajengea uwezo.

Richard alisema klabu hizo kwa jumla ziliasisiwa mwaka 2012 ikiwa na wanachama 50, ambapo Zanzibar iliasisiwa mwaka 2015 na kwamba tangu hapo wamekuwa wakiongezeka kwa kasi ambapo sasa wamefikia wanachama zaidi ya 300 kati ya wateja 50,000 walionao Tanzania nzima.

"Mwamko ni mkubwa sana na hii inatokana na faida za 'Business Club' ikiwa pamoja na kuwasaidia wanachama kuwa wabunifu," alisema.

Aidha, alisema hadi sasa benki hiyo imetoa mikopo kwa zaidi ya wanachama wake 50,000 nchi nzima yenye thamani ya shilingi bilioni 600 inayotumika kuendesha biashara za aina mbalimbali ambazo zinachochea ukuaji wa uchumi kwa wateja, NMB na taifa.

Mkutano huo ulikwenda sambamba na maonyesho ya bidhaa za wajasiriamali mbalimbali, ambao walipohojiwa waliishukuru NMB kwa namna inavyowajali kwa kuwajengea mazingira mazuri ya kufanya biashara zao na kuzalisha bidhaa zenye viwango vinavyokidhi mahitaji ya soko.

# Waziri ataka wanafunzi kuwa wabunifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi kutumia taaluma wanayoipata kwa kubuni mambo mbalimbali ili waweze kujiendeleza katika maisha yao.

Akizungumza katika sherehe ya kuwakabidhi zawadi washindi wa utunzi wa insha kuhusu umuhimu wa bima katika ukumbi wa Shule ya maandalizi Kidutani mjini Zanzibar, alisema utungaji wa insha utawafanya wanafunzi kukuza elimu yao na kuwa watunzi bora wa baadaye.

Waziri huyo, aliwataka wanafunzi kutumia mbinu za watunzi wakongwe ili wakuze taaluma zao na kuwa wajanja wa kubuni kazi zao za utunzi.

Aidha, alilitaka Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) kutoa elimu kwa taasisi mbalimbali kuzikatia bima gari za serikali na kuendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kukata bima kutokana na majanga mabalimbali.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima Zanzibar, Abdulnasir Ahmed Abdulrahman, aliomba Wizara ya Elimu kuendelea kuwahamasisha wanafunzi kutunga insha na mambo mbalimbali ili waweze kukuza vipaji vyao na kukuza lugha ya Kiswahili.

Aidha, alisema zawadi walizozitoa kwa washindi hao zina lengo la kuhamasisha jamii inapata elimu kuhusu ukataji wa bima.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Michezo kutoka Wizara ya Elimu, Hassan Tawakali Khairallah, alisema idara yake inashirikiana na wadau mbalimbali kutanua wigo na kukuza vipaji vya wanafunzi.

"Mashindano ya insha ni mazuri kwani yanasaidia kukua kwa elimu ya utunzi kwa vijana na jamii nzima," alisema.

Mashindano hayo ya utunzi wa insha yalianza Mei 6, mwaka jana na yaliwashirikisha wanafunzi wa kidato cha tatu na nne kutoka shule 475 za serikali na binafsi kwa mada inayoeleza "Umuhimu wa huduma za bima kwa jamii".

Jumla ya washindi 10 kutoka shule nane za Unguja na mbili za Pemba kati ya washiriki zaidi ya 1000 wamechaguliwa, ambapo mshindi wa kwanza ni Yunus Khamis Ramadhan kutoka Shule ya Sekondari Uzini Unguja na kuzawadiwa kompyuta mpakato na vitu mbalimbali.

Mshindi wa pili na watatu katika mashindano hayo ni kutoka Shule ya Sekondari Chanjamjawiri Pemba ambao nao wamezawadiwa kompyuta na vitu mbalimbali.

HABARI KIMATAIFA

## Ripoti: Ndege ya Ethiopia ilitaka kuangukia 'pua'

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

RIPOTI ya uchunguzi kuhusu kuanguka kwa ndege ya Ethiopia Airlines mwezi uliopita imeeleza kuwa ndege hiyo ilitaka kuangukia 'pua' mara kadhaa kabla ya ajali hiyo.

Marubani walifuata maagizo yaliopendekezwa na Boeing kabla ya ajali hiyo kulingana na ripoti ya kwanza ya ajali hiyo.

Ndege hiyo aina ya ET302 ilianguka baada ya kupaa kutoka mji wa Adis Ababa na dakika sita baadaye ilianguka na kuua watu 157.

Ilikuwa ndege ya pili aina ya Boeing 737 kuanguka katika kipindi cha miezi mitano. Mwezi Oktoba mwaka jana ndege aina ya Lion Airflight JT610 ilianguka baharini karibu na Indonesia na kuwaua watu wote.

Waziri wa Uchukuzu wa Ethiopia, Dagmawit Moges akizungumza na waandishi wa habari alisema: "Licha ya juhudi zao, marubani walishindwa kuidhibiti ndege hiyo".

Alisema wafanyakazi wa ndege hiyo walijaribu kila mbinu walizoelezewa na mtengenezaji wa ndege hiyo lakini walishindwa kuidhibiti. Hata hivyo, Ofisa Mkuu wa Ethiopia Airlines, Tewolde Gebre Mariam alisema kuwa alifurahishwa na kazi ya marubani hao kujaribu kuidhibiti ndege hiyo.

Boeing, kampuni ambayo ilitengeneza ndege hiyo ilieleza kweye ukurasa wake wa kijamii wa Twitter kwamba inafuatilia kwa karibu juu ya kuanguka kwa ndege hiyo. **BBC**

## Marekani kupambana na bidhaa bandia

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump ameielekeza Wizara ya Usalama wa ndani kushirikiana na Mwanasheria Mkuu, Wizara ya Biashara na idara nyingine kwa pamoja kuchunguza uwapo wa bidhaa bandia.

Waraka huo ulisainiwa na Rais Trump siku ya Jumatano ili kupambana na uuzaji wa bidhaa bandia kupitia kwenye mitandao kama vile Alibaba, Amazon na eBay.

"Rais ameamua ni wakati wa kusafisha soko holela la bidhaa bandia na usafirishaji haramu," alisema Peter Navarro ambaye ni msaidizi wa rais na mkurugenzi wa ofisi ya biashara na sera za uzalishaji.

Licha ya kwamba hatua za Trump hazipelekei kuchukuliwa hatua mara moja dhidi ya watengenezaji wa wauzaji wa bidhaa za bandia, ambazo ni kuanzia dawa za binadamu hadi viatu vya michezo vyenye majina ya hali ya juu, inaelekeza idara hizo kwa pamoja kuchunguza tatizo hilo na kuwasilisha ripoti na mapendekezo ndani ya siku 210.

Hata hivyo, Navarro alisema hajui ni kiasi gani cha bidhaa bandia kinaendelea kuingizwa. **VOA**

# Mwanamke ajifungua mtoto juu ya mti

**BEIRA,** Msumbiji

MWANAMKE mmoja amejifungua mtoto akiwa juu ya mti wa mwembe alipokuwa akiyakwepa mafuriko katika eneo la kati nchini Msumbiji yaliyosababishwa na kimbunga Idai.

Mama huyo aitwaye Amélia alijifungua mtoto wa kike, Sara, alipokuwa juu ya mti pamoja na mtoto wake wa kiume mwenye umri wa miaka miwili.

Familia yao iliokolewa siku mbili baadaye na majirani, kufuatia dhoruba ambayo watu 700 walifariki nchini humo.

"Nilikuwa nyumbani na mwanangu wa kiume mwenye umri wa miaka miwili ambapo ghafla maji yalianza kuingia ndani ya nyumba yetu," Amélia aliliambia Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa Unicef.

"Sikuwa na njia nyingine ila kukwea mti, nilikuwa peke yangu na mtoto wangu wa kiume." Alisema Amélia.

**Nilikuwa najaribu kulia, kupiga mayowe. Wakati mwingine nilifikiri mtoto alikuwa anatoka, lakini wakati mwingine nikafikiri ilikuwa ni kwa sababu ya njaa.**

Amélia na familia yake kwa sasa wanaishi katika makazi ya muda ya msaada karibu na mji wa Dombe, wanaarifiwa kuwa katika afya nzuri.

Akizungumza na waandishi wa habari, Amelia alisema kuwa alikuwa na uchungu mkali sana.

"Nilikuwa najaribu kulia, kupiga mayowe. Wakati mwingine nilifikiri mtoto alikuwa anatoka, lakini wakati mwingine nikafikiri ilikuwa ni kwa sababu ya njaa," alisema Amelia na kuongeza:

"Watu wengi walipoteza kila kitu katika mafuriko, lakini walau mimi nilipata kitu".

Tukio hilo limetokea takribani miongo miwili baada ya mtoto mwengine kuzaliwa katika mazingira kama hayo.

Mtoto huyo, Rosita Mabuiango alizaliwa wakati wa mafuriko yaliyokumba maeneo ya kusini mwa Msumbiji.

Rosita ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 19, aligonga vichwa vya habari vya kimataifa baada ya yeye na mama yake Sofia kuokolewa na helikopta kutoka kwenye mti uliokuwa umezingirwa na maji ya mafuriko.

Rosita alisema kuwa ahadi za serikali ya Msumbiji za kumlipia masomo, na ahadi ya kumlipia gharama za safari ya Marekani iliyotolewa na serikali ya Marekani zote hazijatimizwa.

"Masomo yangu yamekuwa wakati wote yakigharamiwa na mama yangu, sijapokea chochote kutoka kwa serikali," alisema Rosita na kuongeza:

"Sawa, nyumba tulijengewa na serikali lakini kwa sasa haiko katika hali nzuri. Mvua inaponyesha, nyumba inavuja. Walau wangesaidia kuikarabati". **BBC**



Rais wa Congo, Felix Tshisekedi (Kushoto) akiwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo (kulia) alipofanya ziara ya siku mbili katika nchi hiyo. **PICHA: AFP**

# Rais Felix Tshisekedi azuru Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshisekedi yuko nchini Marekani kwa ziara ya siku mbili.

Ziara hiyo ni ya kwanza kwa Rais Tshisekedi nje ya bara la Afrika tangu alipochukuwa hatamu ya uongozi wa nchi.

Kwenye tarifa yake, Rais Tshisekedi alisema kwamba ziara yake inalenga kukuza hasa uhusiano wa kidiplomasia baina ya Congo na Marekani.

"Katika ushirikiano wetu, Congo inataka kuimarisha uongozi wake wa utawala bora ambao utachangia pia kuimarisha sekta ya elimu na afya. Kwa hiyo ziara yangu ni kutaka hasa kuwapo na uhusiano wa kirafiki baina ya nchi zetu mbili. Tunataka ushirikiano ambao kila upande utafaidika," alisema Rais Tshisekedi.

Hata hivyo, Rais Tshisekedi hataweza kukutana na Rais wa nchi hiyo Donald Trump.

Rais Tshisekedi atakutana na Waziri wa Mambo ya Nje, Mike Pompeo, pia anatarajia kukutana na Seneta Cory Booker, na anatarajia kufanya mikutano mingi yenye lengo kubwa kuhusu uwekezaji katika sekta binafsi.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Rais Tshisekedi anajua kwamba Marekani inaweza kuwa mshirika wake mkubwa dhidi ya mtangulizi wake Joseph Kabila.

Aidha, Lengo la Marekani ni kujaribu kumuunga mkono Rais Tshisekedi kwa njia nzuri na wakati huo huo kuweka shinikizo kwa serikali ya zamani ya Joseph Kabila.

Kabla ya kuhitimisha ziara hiyo, Rais Tshisekedi anatarajiwa kukutana na viongozi wa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF).

Mashirika hayo yalisitisha rasmi ushirikiano wa kifedha na Congo mnamo mwaka wa 2005 baada ya kuilazimisha Congo kuandaa uchaguzi wa kidemokrasia. **RFI**

# Serikali yatoa msimamo rushwa uchaguzi 2020

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema haitakuwa na msalie mtume na mtu, chama cha siasa ama kikundi chochote kitakachojihusisha na rushwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi wa serikali za mitaa, mwaka huu na Uchaguzi Mkuu 2020.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, wakati akifungua mkutano wa kujadili namna ya kudhibiti rushwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa 2019 jijini Dar es Salaam.

Alisema serikali ya Rais John Magufuli, inataka wananchi watambue kuwa imedhamiria kupambana na rushwa katika nyakati zake zote na sura zake zote.

"Sote tunafahamu mwaka 2019 tutakuwa na uchaguzi katika ngazi za serikali za mitaa, hivyo basi uchaguzi huo unapaswa kuendeshwa na kusimamiwa kwa uadilifu na umakini mkubwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili haki, usawa, uhuru na demokrasia viweze kustawi, kuendelezwa na kudumishwa, Takukuru kamwe isiwe na msalie mtume kwa yeyote atakayejihusisha na masuala ya rushwa."

Prof. Kabudi alisema rushwa katika uchaguzi ni zaidi ya udanganyifu wa hesabu za kura, kwa kuwa una madhara ikiwamo viongozi kukosa uwajibikaji, viongozi waadilifu, viongozi wazalendo, uwapo wa vitendo vya uvunjifu wa amani kutokana na migogoro ya mara kwa mara ya kisiasa, uchumi wa taifa kudidimia kwa kukosa mipango ya maendeleo na viongozi kufanya maamuzi ya kisera yenye maslahi kwa wachache.

Aidha, aliipongeza Takukuru kwa kuandaa warsha hiyo katika wakati mwafaka na kusisitiza, pamoja na sheria na kanuni zilizopo bado kuna wajibu mkubwa wa kuhakikisha jamii inashirikishwa na kuelimishwa kuhusu madhara ya rushwa katika uchaguzi.

Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Diwani Athumani, alisema rushwa katika uchaguzi ni hatari na inaweza kuleta madhara kwa taifa kwa kuwa viongozi wala rushwa au watoa rushwa hawataweza kuisimamia nchi kwa misingi ya haki, usawa, uwazi, uwajibikaji na uzalendo na vilevile wananchi wapoka au watoa rushwa hawawezi kuhoji masuala mbalimbali kwa viongozi wao.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano wa kutosha na taarifa bila woga kwa wale wote watakaojihusisha na masuala ya utoaji ama upokeaji rushwa ili sheria ziweze kufuata mkondo wake na baadaye kuwa na taifa lenye usawa katika nyanja zote.

Warsha hiyo ya wadau kujadili namna ya kudhibiti rushwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa imehudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini, vyama vya siasa, vyama vya kiraia na vyombo vya ulinzi na usalama.



Mkurugenzi Mkuu wa T-Marc, Tumaini Kimasa, akizungumza wakati wa kufunga mradi wa Hakuna Wasichoweza mkoani Lindi. Mradi huo ulianzishwa mwaka 2012 na kampuni ya T-Marc na kudhaminiwa na Vodacom Tanzania Foundation kuhakikisha wanafunzi wa kike Lindi na Mtwara hawakosi shule kutokana na uhaba wa taulo za kike.
**NA MPIGAPICHA WETU**

# Zimamoto yatoa tahadhari mafuriko

**Na Romana Mallya**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limewatahadharisha wananchi wanaoishi mabondeni na kandokando ya mito, wamiliki wa vyombo vya usafiri na wasafirishaji kuchukua tahadhari ya mvua zinazoendelea huku likitoa namba ya dharura kwa tukio lolote.

Kamishna wa Operesheni wa kikosi hicho, Billy Mwakatage, alitoa tahadhari hiyo jana jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa wamejipanga na wapo imara na watahakikisha wanatoa huduma bora, sahihi na kwa wakati katika kipindi chote cha athari za mvua.

"Wananchi mnapoona hatari yoyote tafadhali toeni taarifa mapema kwa kupiga namba ya dharura 114," alisema Kamishna Mwakatage.

Alisema endapo maji yatajaa kwenye madaraja au vivuko na kusababisha kutoonekana, wasijaribu kuvuka kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa kuwa madaraja yakawa yamesombwa na maji.

"Kutokana na utabiri uliotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) kuwa kutakuwa na mvua kubwa zinazotarajia kunyesha na baadhi ya maeneo zimeshaanza, lazima wananchi wachukue tahadhari hasa wanaoishi maeneo hatarishi kama mabondeni," alisema.

Pia Kamishna Mwakatage aliwatahadharisha madereva kuchukua tahadhari kwa kutoyaegesha magari yao chini ya miti mikubwa kwa sababu mvua hizi ni kubwa na zinaambatana na upepo.

Alisema kutokana na mvua hizo kuna uwezekano wa mawe makubwa au udongo kuporomoka kutoka milimani au miti kuanguka na kuziba barabara lazima wananchi wachukue tahadhari.

"Ninawataka madereva wote kuwa makini kwa kuendesha magari yao kwa mwendo unaokubalika ili kuepuka ajali zisizo za lazima," alisema.

# Kampeni kupunguza vifo uzazi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WATAALAMU wa afya, watumishi wa serikali, viongozi wa dini pamoja na wadau wametakiwa kushirikiana kuhakikisha vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga vinapungua na kumalizika.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kitaifa yenye lengo la kuzuia vifo vya wajawazito na watoto wachanga yenye kaulimbiu "Jiongeze tuwavushe salama".

Alisema ni vema wote kwa pamoja wakaongeza kasi na uwajibikaji katika masuala ya afya hususani afya ya uzazi na watoto kuanzia miaka sifuri mpaka miaka mitano na kwamba wajawazito wahimizwe kuhudhuria kliniki na ukifika wakati wa kujifungua wawahi mapema hospitali au katika vituo vya afya.

"Vifo vitokanavyo na uzazi bado ni changamoto kubwa hapa nchini hususani katika mkoa wa Mwanza. Mwaka 2017 kinamama waliofariki kutokana na uzazi ni 195, huku mwaka 2018 vifo vikiwa 152 na mwaka huu kuanzia Januari mpaka Machi vifo hivyo ni 46. Hili ni tatizo, maneno sasa basi, ni vitendo tu," Mongela alisema.

Alizitaja sababu zinazochangia vifo hivyo kuwa ni kutokwa na damu nyingi kabla na wakati wa kujifungua, upungufu wa damu, shinikizo la damu, magonjwa mengineyo kama malaria na Ukimwi pamoja na kifafa cha mimba/uzazi.

Pia aliagiza kampeni hiyo ifike mpaka kwenye vitongoji kupitia kwa wenyeviti ili kuwafikia wananchi wa chini waishio vijijini ili wawe na uelewa wa masuala ya afya ya uzazi na jinsi ya kujilinda ili kuzuia vifo hivyo kabla, wakati au baada ya kujifungua.

"Nitafurahi sana kampeni hii ya 'Jiongeze Tuwavushe Salama' ikifika mpaka kwenye vitongoji kupitia kwa wenyeviti wa vitongoji maana wao ndiyo wana nafasi ya kumuona mjamzito kuanzia mimba ikiwa ndogo mpaka anapofikia wakati wa kujifungua," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Phillis Nyimbi, aliwasihi wakuu wenzie wa wilaya waache kukaa ofisini na badala yake watoke na kuwafikia wananchi na kuwahamasisha kwa kutoa elimu ya afya ya mama na mtoto kwa kushirikiana na wataalam na kwa kufanya hivyo itasaidia kupunguza ukubwa wa tatizo hilo.

"Tutoke ofisini na twende saiti, kule tukatoe elimu juu ya suala hili sambamba na wataalam na kwa kufanya hivyo elimu itawafikia wananchi wengi na hivyo tutaokoa maisha ya mama na mtoto kupitia elimu tutakayokuwa tumeitoa," alisema.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA, VIWANJA VINAUZWA CHANIKA** mita 100 kutoka stendi mpya ya Chanika. Umeme upo Bei kuanzia Mil.2. Kwa Mawasiliano: 0714 187555/ 0755 288879

## NAFASI ZA KAZI


**NAFASI ZA KAZI UALIMU /** certificate au diploma /english/ mathematics /SST na science 0656490706/0655628640


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## CHETI KIMEPOTEA



**ANDREW MALANGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.131/61** kilichotolewa na mazengo SEC.SHOOL mwaka 1982. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.taarifa ya polisi: **MIS/RB/538/2016.**

215159502

## CHETI KIMEPOTEA



**JACQUELINE F. SWAI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.224/0048** kilichotolewa na **KIFUNGILO GIRLS SEKONDARI** mwaka 1997. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/197/2019.**

215159002

## KUPOTEA KWA CHETI



**Doreen Angelo** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index **namba S0534/0009** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 1999 katika shule ya Sekondari St. Antony's.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: SRB/B/1319/13**

215158002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No; 86/2019

Ombi la **JULIUS DISMAS MAYAYA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **CHRISTIAN DISMAS MAYAYA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/04/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

Tarehe 03/04/2019

115157602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

04/04/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 06/04/2019 kampuni ya M.E CO.Ltd itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa Kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea Mahenge , gari hilo lenye namba za usajili:**T866 AVC HORSE/T539 CJM**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu -mita 22.00**
   **Kimo -mita 4.80**
3. Njia itakayotumika Dar es salaam hadi Mahenge kupitia Morogoro Road. gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115158202

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi No.18/2019**

**Ombi la ZAHARA HASHIM MWANO kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu MOSHI ALLY JUMANNE**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 18/4/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe14/3/2019

115159702

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi No.20/2019**

**Ombi la ZAINABU KAISI MOHAMED kuteuliwa**

**Msimamizi wa mirathi Marehemu MOHAMED KAISI CHALLA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 24/4/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 4/4/2019

215159602

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI.**
**WILAYA YA MOSHI**

**MAOMBI NA. 39/2018**

**ALPHONCE EPHIRAIM LYARUU............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**EMMANUEL LYIMO**
**WILLIAM CRISOPH SHAO**
**ONESMO CRISTOPH SHAO...............WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: ONESMO CRITOPH SHAO**
**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa Mleta maombi ameleta maombi ya kesi na yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi. Shauri limepangwa kutajwa tarehe 8/5/2019 saa mbili na nusu (2:30) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti P.MAKWANDI,hivyo unatakiwa kufika mahakamani wewe au wakili wako.
**ANGALIA:** Kama hamtahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04 mwezi, April 2019.

115160202

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI.**
**WILAYA YA MOSHI**

**MAOMBI NA. 39/2018**

**EPHIRAIM HIPPOLITE LYARUU.............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**PASCAL CHARLES MOSHI**
**WILLIAM PASCAL MOSHI**
**EMMANUEL LYIMO.............................WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: PASCAL CHARLES MOSHI &**
**DONATA PASCAL MOSHI**
**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa Mleta maombi ameleta maombi ya kesi na yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi. Shauri limepangwa kutajwa tarehe 8/5/2019 saa mbili na nusu (2:30) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti J.Sillas, hivyo unatakiwa kufika mahakamani nyie au mawakili wenu .
**ANGALIA:** Kama hamtahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04 mwezi, April 2019.

115160202

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**FALHUM AMIR MSHANA** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari yake aina ya Corolla Namba **T 303 AVV.** Hivyo kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi **SO/RB/1940/2019.** Au apige simu namba **0754645322.**

115160402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe 05-04-2019 kampuni ya **HIGHLAND ESTATES LIMITED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **MBARALI kupitia SINGIDA,** gari hilo lenye namba za usajili:
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**T 935 DBQ / T 476 CBG**

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - mita | 20.00 |
| Upana | - mita | 3.20 |
| Kimo | - mita | 5.40 |

Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

115158802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

04/04/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya IJUMAA tarehe **05/04/2019** kampuni ya 4 **BROTHER'S & SISTER'S CONSTRUCTION LIMITED.** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa.

   Kutoka **DAR ES SALAAM(VINGUNGUTI) kuelekea MWANZA (IGOME NANE NANE) kupitia DODOMA,** gari hilo lenye namba za usajili:
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**T831 DMF/ T734 BTL**

| | |
|---|---|
| Urefu | -mita 17 |
| Upana | -mita 3.00 |
| Kimo | -mita 4.6 |

Gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115158302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Wisdom L. Maliki** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T790 CCP,** aina ya **SUZUKI CARRY** yenye chasis namba **DO51T643489,** engine namba **FGA6794244.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KJN/RB/1561/2019**

115158102

**CHANGE OF NAMES BY DEED POLL**
**Registration of Document Act (CAP 117)**

**BY THIS DEED, I** the undersigned **MIKE METHEW MLAY of P.O BOX 5362 TANGA, TANZANIA** do hereby absolutely renounce and abandon the use former name **MIKE LAIMER MLAY** and in lieu thereof do assume from the date hereof the name of **MIKE METHEW MLAY.**

**AND**

**IN PURSUANCE** of such change of my name I hereby declare that I shall at all times thereafter in all records,deed, and instruments,in writing in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all accessions.

**AND**

**I HEREBY AUTHORISE** and request all persons to designate, describe and address me by such assumed name of **MIKE METHEW MLAY.**

**IN WITNESS WHEREOF** Ihave hereunder signed my assumed name of **MIKE METHEW MLAY** in lieu of the relinquished names of MIKE LAIMER MLAY and set my hand this 19 Day of June 2018.

**BEFORE ME:**
**Name: EMMANUEL B. MALYA**
**Qualification: ADVOCATE**

115157702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Kati**ka mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;85/2019

Ombi la **SCOLASTICA P.KACHENJE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu PONCEOUS EDWIN Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/04/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

Tarehe 03/04/2019

115157502


*Kwa Habari Motomoto usikose*
*Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# COUTINHO, RAKITIC KUIINGIZIA BARCA EURO MILIONI 300

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inataka kuingiza kiasi cha euro milioni 300 kwa kuwauza wachezaji wake kipindi cha majira ya joto, wakati klabu hiyo ikitafuta fedha za kuimarisha kikosi chake.

Wachezaji kama Philippe Coutinho, Samuel Umtiti na Ivan Rakitic ni kati ya nyota ambao wanatajwa kuuzwa mwishoni mwa msimu huu ili kujiingizia fedha hizo.

Barca tayari imeshafanya usajili wa euro milioni 86 kwa kumtwaa kiungo wa Ajax, Frenkie de Jong ambaye atajiunga nao mwishoni mwa msimu huu.

Lakini tetesi zinaeleza kwamba, beki Matthijs de Ligt naye yuko mbioni kujiunga na kikosi hicho huku pia Luka Jovic na Antoine Griezmann wakitajwa kutua hapo Camp Nou.

Mtandao wa ESPN umeripoti kwamba Barcelona wanatarajia kupata kati ya eruo milioni 250 na 300.

Barca ilikubali kutoa kiasi cha euro milioni 160 kumsajili nyota wa Brazil Coutinho Januari mwaka jana kutoka Liverpool, lakini ameshindwa kuonyesha kipaji alichotarajiwa.

ESPN imedai kwamba, Barcelona ipo tayari kumtoa hata kwa euro milioni 100 ili iweze kuingiza fedha za kusajili wachezaji wengine.

# *Mandzukic aongezwa mwaka mmoja Juve*

**TURIN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Mario Mandzukic, amesaini mkataba mpya wa mwaka mmoja wa kuendelea kuichezea klabu hiyo ya hapa Turin na sasa atakaa hadi mwaka 2021 kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Croatia awali alijiunga na Bianconeri hao kutoka Atlético Madrid mwaka 2015, akitua hapo kwa euro milioni 21.

Mandzukic ameichezea Juventus jumla ya mechi 159 na kufunga mabao 43 na kutoa pasi za mwisho 24 katika michuano yote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, awali ilibainishwa kwamba huu ulikuwa ni mwaka wake wa mwisho kucheza hapo Juventus, lakini sasa imethibitishwa kuwa Mandzukic atacheza kwa mwaka mmoja zaidi.

Mchezaji huyo amekuwa mhimili mkubwa wa kocha, Massimiliano Allegri akiwa amecheza mechi 30 msimu huu na kuiwezesha kuongoza msimamo wa Ligi Kuu kwa tofauti ya ponti 18.




# Sanches: Sina furaha Bayern Munich

**MUNICH,** Ujerumani

RENATO Sanches amebainisha kwamba hana furaha kwa kutopata nafasi nyingi za kucheza katika klabu yake ya Bayern Munich, akidokeza kwamba yupo tayari kuondoka kipindi cha majira ya joto.

Kiungo huyo raia wa Ureno mwenye umri wa miaka 21, hana nafasi ya kucheza katika kikosi hicho na amecheza mechi 14 tu kwa msimu wote akiwa na miamba hao wa Bavaria.

Na sasa nyota huyo amebainisha wazi kwamba jambo hilo linamsononesha na hana furaha, hivyo anataka kuondoka na kuangalia changamoto mpya mwishoni mwa msimu huu.

"Sio maamuzi yangu. Nasubiri nafasi yangu ya kutaka kucheza," amesema mchezaji huyo.

"Bila shaka, nataka kucheza zaidi. Msimu bado haujaisha. Kwa miezi miwili kila kitu kinawezekana, lakini sijui."

Baada ya kuwa na kipindi kigumu akiwa anacheza kwa mkopo pale Swansea msimu wa 2017/18, Sanches alirudi Bayern, lakini akajikuta akianza katika mechi nne tu kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Mkataba wa sasa wa Sanches unamalizika kipindi cha majira ya joto mwaka 2021, lakini sasa nyota huyo amesema hana furaha kuendelea kucheza chini ya kocha, Niko Kovac.

"Hapana, hana msaada kwangu. Lakini ni kwa maamuzi yake, sio yangu," ameongeza.

Mchezaji huyo wa zamani wa Benfica amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na Manchester City ya England, huku timu yake hiyo ya zamani ikionekana kumnyatia pia.



# Guardiola: City msiwe na tamaa ya mataji manne



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amewaambia wachezaji wake kusahau suala la kushinda mataji manne msimu huu.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England, EPL, tayari wameshinda taji la Carabao na juzi wameichapa Cardiff.


Na sasa watakabiliana na Brighton katika nusu fainali ya Kombe la FA siku ya Jumamosi na baadaye Totenham katika awamu ya kwanza ya robo fainali ya Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya Aprili 9, mwaka huu.

"Katika wiki moja ama siku tatu tunaweza kupoteza mataji yote matatu," alisema Guardiola akinukuliwa na Sky Sports.

Kocha huyo wa zamani wa Barcelona ameshinda mataji mawili ya ligi na Kombe la Ligi ya Uingereza msimu uliopita tangu alipojiunga na Man City mwanzo mwa msimu wa 2016.

Bado anabakia kukata tamaa ya kushinda mataji manne msimu huu: "Nimewaambia wakati mwingi kwamba niulizeni mwisho wa msimu."

# POGBA ATAONDOKA MAN UNITED - INCE



**MANCHESTER,** England

GWIJI wa zamani wa timu ya Taifa ya England na Klabu ya Manchester United, Paul Ince hafikirii kama kiungo Paul Pogba atabaki katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu.

Ince amenukuliwa na Gazeti la Daily Mail akisema kuna uwezekano mdogo mno wa Pogba kubaki Manchester United mwishoni mwa msimu kwani ni wazi kwamba anaonekana anataka kuondoka.

"Namwamini Paul Pogba, Ole anatakiwa kumshawishi kubaki Manchester United, kwa kuwa anamtegemea kuunganisha timu kwenye safu ya ushambuliaji, lakini silioni hili kama likitokea," amesema Ince.

"Kiukweli sifikirii kama Paul Pogba atabakia Old Trafford msimu ujao, namuona kabisa akiondoka."

Imeripotiwa kuwa kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Pogba kuna uwezekanao mkubwa wa kutoendelea kuichezea Man United msimu ujao, kwa tetesi zinazoendelea kudai kuwa atahama klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu.

Ince amesema pamoja na Pogba kiwango chake kimeimarika chini ya kocha Ole Gunnar Solskjaer ukilinganisha na hali yake ilivyokuwa chini ya Jose Mourinho, anaamini kuwa anaweza kwenda kujiunga na Real Madrid.

Ince ambaye aliwahi kucheza Man United kwa miaka sita (1989-1995) ameweka wazi kuwa kitakuwa sio kitu kizuri kama Man United hawatomaliza nne bora msimu huu.

Ince ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 51, amesema iwapo Man United itashindwa kumaliza kwenye nne bora ni wazi kwamba, uwezekano wa Pogba kubaki kwenye kikosi hicho itakuwa ni vigumu.



# *Kinda Juve lawamani kuchochea ubaguzi*

**TURIN,** Italia

BAADA ya mshambuliaji kinda wa Klabu ya Juventus na raia wa Italia, Moise Kean kurushiwa maneno ya kibaguzi na kutoa ishara ya kunyosha mikono, kocha wake, Massimiliano Allegri amemlaumu kwa kitendo hicho.

Kean ambaye alitolewa maneno ya kibaguzi kutoka maeneo ya mashabiki wakati wa mechi ya ligi ya Serie A dhidi ya Cagliari Jumanne, alionyesha ishara ya kujibu.

Kinda huyo mwenye umri wa miaka 19 alishika mikono yake juu baada ya kuifungia Juve bao la pili katika ushindi wa 2-0 akijibu sauti alizokuwa akisikia kutoka maeneo ya mashabiki.

Baadaye aliandika katika mtandao wake wa Instagram: "Njia mwafaka ya kujibu ubaguzi wa rangi".

Lakini kocha Massimiliano Allegri na beki Leonardo Bonucci walisema kuwa Kean anapaswa kulaumiwa kutokana na ishara hiyo na si bao lake.

"Asingesherehekea namna alivyofanya," alisema Allegri. "Ni kijana mdogo na anafaa kupata funzo, lakini pia kuna baadhi ya vitu ambavyo mashabiki pia hawafai kufanya."




# HERRERA, MASTAA 6 KUPIGWA PANGA UTD

## ●●● Mata safari ya Barca yaiva, Sanchez ategemea huruma ya Solskjaer huku...

**Manchester,** England

MANCHESTER United inajiandaa kupitisha panga kali majira ya joto ambalo halijawahi kufanyika kwa kipindi cha miaka minne kwa wachezaji takriban sita wenye majina makubwa kuruhusiwa kuondoka Old Trafford, Sky Sports News linaundani wa mchakato huo.

Panga hilo ambalo litajumuisha nyota wakubwa wenye vipaji, litakuwa ni mara ya kwanza kufanyika tangu majira ya joto mwaka 2015 wakati Louis van Gaal alipowafungulia mlango wa kuondoka wachezaji maarufu akiwamo Angel Di Maria, Robin van Persie na Javier Hernandez.

Sky Sports News inatambua kwamba kiungo Ander Herrera tayari ana makubaliano binafsi ya kujiunga na Paris Saint-Germain, wakati Juan Mata yupo katika mazungumzo ya kujiunga na Barcelona.

Alexis Sanchez amekuwa akihaha kurejea katika kiwango chake tangu alipojiunga na United akitokea Arsenal Januari mwaka 2018 kwa uhamisho uliomhusisha Henrikh Mkhitaryan kutua upande wa pili, Mchile huyo akifunga mabao matano katika mechi 41 alizocheza hadi sasa.

**Inaeleweka kocha Ole Gunnar Solskjaer atakuwa na kauli ya mwisho kuhusu mustakabali wa Sanchez hapo United, ingawa suala la mshahara linaweza kuthibitisha kuwa kikwazo kwa klabu zinazotaka kumnunua.**

Antonio Valencia anatarajiwa kuondoka United majira ya joto baada ya klabu hiyo kuamua kutomuongeza mkataba, wakati beki mwenza Marcos Rojo ameruhusiwa kujifua na miamba ya Argentina, Estudiantes.

Rojo mara ya mwisho kuichezea United ni kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya walipochezea kichapo cha mabao 2-1 ugenini dhidi ya Valencia Desemba mwaka jana na amecheza jumla ya mechi tatu tu msimu huu.

Matteo Darmian, ambaye alihusishwa na kurudi Serie A Januari mwaka huu, hajaichezea United tangu walipopata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Brighton Januari 19, na wakati Ashley Young na Diogo Dalot wakiwamo pia katika orodha hiyo.

Lakini mazungumzo kuhusu kipa David de Gea yanaendelea, na United inatumai makubaliano yanaweza kufikiwa kuhakikisha Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 28, anapewa mkataba wa muda mrefu.

De Gea, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu ujao, amekuwa akihusishwa na kujiunga na Real Madrid pamoja na PSG katika miezi ya hivi karibuni.

## ZISIKUPITE

### HUDSON-ODOI, SANCHO SHIDA

MANCHESTER United inaamini lengo la kuwasajili mawinga wawili wa kimataifa wa England - anayeichezea Borussia Dortmund, Jadon Sancho, 19, na wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, 18 , kunaweza kupata kizuizi kutoka kwa klabu zao kutotaka kuwauza. ***(Mail)***

### BARCA KUINGIZA MIL. 300

BARCELONA inatumai kuingiza kati ya euro milioni 250 na 300 kwa kuuza wachezaji wake majira haya ya joto ili kupata uwiano mzuri katika akaunti yao majira haya ya joto na kuweza kusajili bila kuingia matatizoni ya kukiuka kanuni za usajili kifedha. ***(ESPN)***

### DE GEA AITEGA MAN UNITED

MANCHESTER United haitalazimishwa kumuuza kipa Mhispania David de Gea, 28, majira haya ya joto - hata kama watashindwa kukubaliana naye mkataba mpya na ataendelea kubaki ili kuingia mwaka wake wa mwisho, ili kuongeza uwezekano wa yeye kuondoka akiwa huru mwishoni mwa msimu ujao. ***(Mirror)***

### KOVACIC ANOGEWA CHELSEA

KIUNGO Mcroatia Mateo Kovacic, 24, angependa kubaki Chelsea, anapocheza kwa mkopo, kuliko kurejea klabu yake ya Real Madrid msimu ujao. ***(Goal)***

### OVERMARS BADO LULU ARSENAL

ARSENAL inaendelea kufanya usaili wa nafasi ya mkurugenzi wa ufundi, na mkurugenzi wa Ajax, Marc Overmars - ambaye ni winga wa zamani wa 'Gunners' - pamoja na mkurugenzi wa Marseille, Andoni Zubizaretta wakielezwa kuwa miongoni mwa wanaowindwa. ***(Mail)***

### REAL, JUVE, PSG MBIO MOJA

REAL Madrid, Juventus na Paris St-Germain zote zinamfuatilia kipa wa Man Utd, David De Gea. ***(Express)***

### NIGUEZ, HERNANDEZ WAWINDWA

MANCHESTER United imejiunga katika mbio za kumsajili kiungo wa Saul Niguez, 24, wakati Manchester City yenyewe ikibainisha kuwa mchezaji mwenza wa Atletico Madrid, kiungo Rodri Hernandez, 22, kama mbadala sahihi kwao. ***(ESPN)***

### VARANE AANZA KUULIZIWA PSG

PARIS St-Germain na Manchester United zimeulizia uwezekano wa kumpata beki wa kimataifa wa Ufaransa na Real Madrid, Raphael Varane, 25. ***(Independent)***

### SCHURRLE KURUDI DORTMUND

MSHAMBULIAJI wa Ujerumani Andre Schurrle, 28, atakuwa mchezaji wa kwanza kuachana na Fulham inayoshuka daraja kwa kurudi Borussia Dortmund mapema. ***(Sun)***

### ANUKIA TOTTENHAM

FULHAM ['The Cottagers'] inauwezekano wa kumpoteza winga Ryan Sessegnon, 18, na Tottenham ikiwa tayari kumnasa mchezaji huyo anayethaminishwa na pauni milioni 50. ***(Mirror)***

### EVERTON KUJILIPUA KWA GUEYE

EVERTON imeambiwa ijipange yenyewe kuhusu uhamisho wa kiungo Msenegal Idrissa Gueye, 29, majira haya ya joto. ***(Liverpool Echo)***

## HABARI MICHEZO

## Taifa Jang'ombe mawazo Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Taifa Jang'ombe, Mohamed Seif, maarufu "King" amesema bado anaamini timu yake ina uwezo wa kurejea Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao licha ya kuwapo kwa upinzani kwenye Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja.

Akizungumza na gazeti hili jana, King alisema wachezaji na benchi la ufundi la timu hiyo wamejiandaa kuendelea kupambana kusaka ushindi katika kila mechi wanayocheza kwa sababu wanataka kurejesha heshima yao. King alisema pia wadau wote wa timu hiyo wamekuwa na "kiu" ya kurejea katika ligi hiyo ya juu visiwani hapa.

"Ninakiamini kikosi changu kinaweza kufanya maajabu kutokana na jitihada zinazofanywa na wachezaji wenyewe wanapokuwa mazoezini na uwanjani katika kila mechi, wamekuwa tofauti na wanaonyesha wazi kwamba wanataka kupanda daraja," alisema King.

Kocha huyo aliongeza kuwa timu hiyo itakapofanya vizuri, itasaidia kuvutia wadhamini na gharama za kuiendesha klabu yao zitakuwa nyepesi.

"Kila mchezaji anataka kuona Taifa Jang'ombe inarejea Ligi Kuu, wanajua wakifika hapo ndio nafasi yao ya kuuza vipaji vyao itapatikana kirahisi," aliongeza kocha huyo.

Ligi Kuu Zanzibar ndio hutoa mwakilishi wa visiwa hivyo katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na wakati bingwa wa Kombe la FA hushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 29 | 21 | 5 | 3 | 46 | 20 | 68 |
| 2. Azam | 29 | 18 | 8 | 3 | 48 | 18 | 62 |
| 3. Simba | 22 | 18 | 3 | 1 | 48 | 7 | 57 |
| 4. Lipuli | 32 | 12 | 11 | 9 | 28 | 26 | 47 |
| 5. Mtibwa Sugar | 30 | 12 | 6 | 12 | 31 | 24 | 42 |
| 6. KMC | 31 | 9 | 14 | 8 | 32 | 23 | 41 |
| 7. TZ Prisons | 31 | 10 | 11 | 10 | 26 | 25 | 41 |
| 8. Coastal Union | 31 | 9 | 14 | 8 | 28 | 30 | 41 |
| 9. Mbao FC | 32 | 10 | 9 | 13 | 20 | 30 | 39 |
| 10. Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 11. Alliance | 31 | 9 | 10 | 12 | 24 | 33 | 37 |
| 12. Ndanda | 30 | 9 | 10 | 11 | 20 | 30 | 37 |
| 13. Mwadui | 32 | 10 | 6 | 16 | 35 | 41 | 36 |
| 14. Kagera Sugar | 30 | 8 | 12 | 10 | 23 | 29 | 36 |
| 15. JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 19 | 27 | 36 |
| 16. Singida Utd | 31 | 9 | 9 | 13 | 22 | 31 | 36 |
| 17. Ruvu Shooting | 32 | 8 | 12 | 12 | 28 | 38 | 36 |
| 18. Stand Utd | 32 | 10 | 6 | 16 | 29 | 41 | 36 |
| 19. Biashara Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 22 | 29 | 33 |
| 20. African Lyon | 32 | 4 | 10 | 18 | 19 | 41 | 22 |

# MAJALIWA AITAHADHARISHA STARS AKIIPONGEZA SIMBA

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka viongozi, wachezaji na makocha wa Timu ya Taifa ya Soka (Taifa Stars), kufanyia kazi upungufu uliojitokeza katika mechi zake zilizopita ili kujiweka sawa kwa ajili ya michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 itakayofanyika Misri Juni mwaka huu.

**Vilevile, kiongozi huyo wa serikali, ameipongeza Klabu ya Simba ya jijini Dar es Salaam kwa kuiwakilisha vema Tanzania katika michuano ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika mwaka huu.**

Akiwasilisha hotuba yake bungeni mjini Dodoma jana kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake na Ofisi ya Bunge kwa mwaka ujao wa fedha, Majaliwa aliwataka wachezaji na watu wote wanaohusika na Taifa Stars kufanyia kazi upungufu uliojitokeza katika michezo iliyopita kwa kuwa timu hiyo inapaswa kwenda Misri kushindana na si kushiriki.

"Itakumbukwa kwamba imepita takriban miaka 39 tangu nchi yetu ishiriki kwa mara ya mwisho michuano ya mpira wa miguu kwa nchi za Bara la Afrika, maarufu Afcon.

"Hata hivyo, kusubiri huko kulikoma Machi 24, mwaka huu baada ya vijana wetu wa Taifa Stars kupata ushindi mnono wa mabao 3-0 dhidi ya jirani zetu wa Uganda. Ushindi huo unaipeleka Taifa Stars katika Afcon 2019 huko Misri.

"Nitumie fursa hii kuwapongeza wachezaji, viongozi, benchi la ufundi, kamati ya uhamasishaji ya ushindi, mashabiki na Watanzania wote kwa kutimiza ndoto yetu ya muda mrefu ya kushiriki michuano hiyo mikubwa kabisa barani Afrika.

"Nitoe wito kwa viongozi, wachezaji na walimu kufanyia kazi upungufu uliojitokeza kwenye michezo iliyotangulia ili kujiweka sawa na michuano ya mwezi Juni mwaka huu. Napenda mtambue kwamba lengo letu ni kwenda kushindana na si kushiriki. Niwatakie maandalizi mema na mafanikio katika michuano hiyo inayokuja," alisema.

Waziri Mkuu aliipongeza Klabu ya Simba kwa mafanikio iliyoipatia nchi msimu huu katika michuano ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika, akieleza kuwa kwa muda mrefu klabu za Tanzania zimekuwa hazifanyi vizuri katika medani ya michuano ya klabu barani Afrika.

"Katika msimu wa 2018/19, Klabu ya Simba ya Dar es Salaam imetutoa kimasomaso baada ya kufuzu hatua ya robofainali ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika.

"Kufanya vizuri kwa Klabu ya Simba kunaongeza uwezekano wa Tanzania kupatiwa nafasi nyingine mbili na kufanya jumla ya klabu nne zitakazoshiriki mashindano hayo makubwa barani Afrika katika msimu ujao," Waziri Mkuu alisema.

Majaliwa aliongeza: "Ushindi wa Taifa Stars na Simba una manufaa makubwa kwa nchi yetu ikiwamo kuitangaza vema nchi na kufungua fursa za ajira kwa vijana wetu hususan wanaojihusisha na soka.

"Nitumie fursa hii kuwapongeza wachezaji, viongozi, benchi la ufundi na mashabiki wote wa Klabu ya Simba kwa mafanikio hayo makubwa. Tupo pamoja nanyi.

"Napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza mwanamasumbwi wa kitanzania Hassan Mwakinyo kwa kuendelea kuwa mfano bora kwenye tasnia hiyo ya masumbwi. Machi 23, mwaka huu, Mwakinyo aliendelea kung'ara katika anga za masumbwi na kuipeperusha vema bendera ya Tanzania baada ya kumtwanga mpinzani wake Muargentina Sergio Gonzalez huko Nairobi.



Washindi wa Droo ya 'Masta Bata', Mganga Mkuu wa Jiji la Arusha, Dk. Simon Chacha (kushoto) na watoto wake pamoja na Dk. Einstein Ngao Stephen wa Hospitali ya Mloganzila wakiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dr es Salaam tayari kuelekea Dubai. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Twiga Stars kutupa karata muhimu leo*

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), inatarajia kuwakabili wenzao kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), katika mchezo wa kwanza wa kuwania tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Timu hizo zitacheza mechi ya marudiano Aprili 9, mwaka huu jijini Kinshasa na mshindi wa jumla atatinga raundi ya pili ambapo atakutana na Equatorial Guinea.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, alisema kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo na anaamini wataanza vema kampeni ya kuelekea Tokyo, Japan kwa kupata ushindi.

Shime alisema kuwa anawafahamu wapinzani wao kwa kuangalia baadhi ya mechi walizocheza na hivyo amewaandaa wachezaji wake kuwadhibiti wasipate nafasi ya kumiliki mchezo huo.

"Tuko tayari, tunajua kila mechi ni ngumu, tumeshawasoma na wao wameshatusoma, kwa kifupi tumejipanga kuanza vema michuano hii, utulivu na umakini ndio utatusaidia kufikia malengo," alisema Shime.

Aliongeza kuwa wachezaji wake wana uzoefu na mechi za kimataifa na wana morali ya juu kuhakikisha wanapeperusha vema bendera ya nchi.

Nahodha wa timu hiyo, Asha Rashid alisema wana deni la kuendeleza furaha kwa Watanzania katika mchezo wa soka baada ya kaka zao Taifa Stars kufanikiwa kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019.

"Tumejipanga na tunajua tunachotakiwa kukifanya, tunaahidi kujituma na kupata ushindi hapa nyumbani ili kurahisisha kazi katika mechi tutakayokwenda kucheza Congo," alisema mshambuliaji huyo ambaye anaichezea JKT Queens.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Wanawake Tanzania (TWFA), Amina Karuma, alisema maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na kueleza kuwa kikosi cha DRC kilitua nchini juzi pamoja na waamuzi na kamisaa wa mchezo huo ambaye anatoka Zambia.

Michezo
Ijumaa Aprili 5, 2019
Nipashe



Herrera, mastaa sita kupigwa panga Utd UKURASA 30



Leroy Sane (kulia) akiifungia Manchester City bao la pili wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Cardiff kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Etihad juzi usiku. Ushindi huo unairejesha kileleni mwa ligi hiyo kwa kuipiku Liverpool kwa pointi moja. **HABARI UK. 29**

# Simba, Mazembe zawashiana moto

## ●●● Kagere atoa yake, Mputu asema watavunja mwiko wa Msimbazi Taifa, Kidiaba aahidi...

**Na Somoe Ng'itu**

MABINGWA mara tano wa Ligi ya Mabingwa Afrika, TP Mazembe wamewasili nchini tangu juzi wakitokea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), huku wakitamba wamekuja "kuvunja mwiko" kwa kuwafunga Simba ikiwa nyumbani, wakati wenyeji hao wameahidi kuwa wamejipanga kumaliza mechi hiyo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Simba inatarajiwa kuikaribisha TP Mazembe ya mjini Lubumbashi kesho katika mchezo wa kwanza wa hatua ya robo fainali utakaochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini kuanzia saa 10: 00 jioni.**

Mshambuliaji wa Simba, Mnyarwanda Meddie Kagere 'MK 14', alisema jana kuwa yuko tayari kwa mchezo huo na yeye pamoja na wachezaji wenzake, wamejipanga kuonyesha soka la kiwango cha juu ili kuhakikisha wanapata ushindi. Kagere alisema Simba imefika katika hatua hiyo si kwa kubahatisha na wanataka kuendelea kuona wanasonga mbele katika michuano hiyo ya juu na yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

"Ni mechi ngumu kwa kila timu, tuna rekodi nzuri tukicheza nyumbani na TP Mazembe wana rekodi nzuri katika mashindano haya, ila tunasema 'Yes we can'," alisema mshambuliaji huyo ambaye amefunga mabao sita katika michuano hiyo hadi sasa.

Nahodha na kiungo mshambuliaji tegemeo wa TP Mazembe, Tressor Mputu, aliliambia gazeti hili kuwa wamekuja nchini kucheza soka la kiwango cha juu ili waweze kupata ushindi.

Mputu, ambaye anaichezea TP Mazembe kwa zaidi ya miaka 10 alisema kwamba wanafahamu Simba imekuwa na nguvu katika uwanja wake wa nyumbani, lakini wao itakuwa timu ya kwanza kuifunga na hatimaye kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

"Tumekuja kucheza kabumbu, tumejiandaa kucheza vizuri, tunajua mechi itakuwa ngumu, Simba inacheza kwa nguvu kwenye uwanja wake wa nyumbani, tutakuwa timu ya kwanza kuifunga Simba ikiwa nyumbani," alisema mshambuliaji huyo ambaye alishangiliwa zaidi na mashabiki waliofika Uwanja wa Ndege kuipokea timu yao.

Naye golikipa mkongwe wa timu hiyo, Robert Kidiaba, alisema kuwa wamejiandaa vema kwa mchezo huo na wanaamini wataibuka na ushindi katika mechi hiyo.

Kidiaba ambaye kwa sasa ni Mbunge wa Jimbo la Katanga, alisema bado ana kiwango bora, huku akiitaja ile staili yake ya kushangilia mabao kwa kurukaruka akiwa amekaa hajaiacha na itaonekana endapo watafunga mabao hapo kesho.

# Yanga yavutwa shati Nangwanda

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Yanga imedondosha pointi nyingine mbili kwenye kinyang'anyiro chake cha kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Bara baada ya kulazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Ndanda kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara.

Hii ni sare ya pili kwa timu hizo msimu huu kwani kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Novemba 4, mwaka jana Uwanja wa Taifa, zilitoka tena sare ya bao 1-1.

Kwa matokeo hayo sasa Yanga inakuwa na pointi 68 sita mbele ya Azam FC iliyopo nafasi ya pili kufuatia kila moja kucheza mechi 29, lakini pia ni sare ya tano msimu huu kwa timu hiyo ya Mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam. Sare hiyo si salama sana kwa Yanga, kwani inatoa mwanya kwa watani zao, Simba ambao wapo mechi saba nyuma, wakiwa na pointi 57.

Straika hatari wa Ndanda, Vitalis Mayanga alifunga bao dakika ya 19 kutokana na makosa yaliyofanywa na beki Kelvin Yondani.

Beki huyo alishindwa kuzuia mpira mrefu uliopigwa kutoka upande wa mashariki ya uwanja na mfungaji akauwahi, kabla ya kumlamba chenga kipa Klaus Kindoki na kuuzamisha kimyani.

Amissi Tambwe aliikosesha Yanga bao dakika ya 29, alipokosa mkwaju wa penalti uliotoka pembeni mwa goli, huku kipa Said Mohamed akiwa ameshapotea kwa kwenda upande mwingine.

Penalti hiyo ilitolewa baada ya Baraka Majogolo kumuangusha Heritier Makambo ndani ya eneo la hatari.

Mayanga aliikosesha Ndanda bao la pili, alipoukosa mpira wa krosi akiwa yeye na lango, huku mabeki wa Yanga na kipa wao Kindoki wakiwa wamepoteana.

Yanga ilisawazisha bao dakika ya 61 kupitia kwa Pappy Tshishimbi aliyeruka na kupiga kichwa akiwa peke yake bila kubughudhiwa na mabeki wa Ndanda, hivyo akimalizia krosi kutoka winga ya kushoto iliyopigwa na Yondani.

Pamoja na timu zote kufanya mabadiliko kadhaa, hakuna iliyoweza kubadili matokeo hadi dakika 90 za mchezo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042